**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TANO**

**Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 14 Novemba, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM I. KHATIB):** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Dhamana ya Uwekezaji Tanzania kwa Mwaka Ulioishia Tarehe 30 Juni, 2005 *(The Annual Report and Accounts of The Unit Trust of Tanzania for the Year ended 30th June, 2005)*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 138

**Ujenzi wa Daraja la Mto Bubu**

**MHE. DAMAS PASCAL NAKEI** aliuliiza:-

Kwa kuwa ujenzi wa daraja la mto Bubu mpakani mwa Babati na Hanang, sehemu ya Udagat ni ahadi ya Serikali kwa muda mrefu; na kwa kuwa Serikali iliahidi ingepeleka Wataalam kuangalia hali ya daraja ili kufanya usanifu na hatimaye ujenzi wenyewe:-

(a) Je, ni lini sasa ahadi hiyo itatekelezwa?

(b) Je, wataalam hao wameshafika kwenye eneo husika, kama bado ni kwanini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu napenda kujibu Swali la Mheshimiwa Damas Pascal Naketi, Mbunge wa Babati Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inauelewa umuhimu wa ujenzi wa daraja kwenye mto Bubu kwa kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Babati, tathmini ya awali kwa ajili ya ujenzi wa daraja hili ulifanyika na gharama yake ni shilingi 100.87 milioni.

Kutokana na ufinyu wa Bajeti za Maendeleo katika sekta ya Barabara ukilinganisha na mahitaji halisi ndiyo sababu kubwa inayofanya ahadi nyingi zichukue muda mrefu kutekelezwa. Aidha, kwa sAsa *OWM-TAMISEMI* kupitia Mpango wake wa kitaifa wa Usafiri Vijijini *(NRTP),* inachambua miradi ya barabara ambayo inastahili kutekelezwa kupitia mpango huo. Namwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira kwani Serikali kupitia mpango huu itashirikiana na Halmashauri ya Babati kuangalia na kuona uwezekano wa daraja la mto Bubu kujengwa kupitia Mpango wa kitaifa wa Usafiri Vijijini *(National Rural Transport Program (NRTP).*

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2004 Wataalam kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, *TAMISEMI,* na Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa wa Manyara pamoja na Halmashauri ya Babati walifika katika sehemu hilo. Sehemu hiyo inapitika wakati wa kiangazi tu kwa sababu ni eneo linalokwamisha maji yaani *(swamp area).* Hivyo wakati wa mvua nyingi maji yanajaa sana, aidha wataalam walishauri kwamba sehemu hiyo inafaa kujengwa *vented drift* ambayo italala kwenye nguzo *(piles)* ambazo zitakuwa za chuma au mbao *(treated timber).* Hivyo, wakati ukifika wa kujengwa kwa daraja hilo utaalam uliotolewa utazingatiwa kama utaonekana bado unafaa.

**MHE. DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tatizo kubwa linaonekana ni fedha hazitoshi, na kwamba gharama ya daraja hilo ni shilingi milioni 100.

Je, anaweza kukubaliana nami kwamba kiasi hicho cha fedha kinaweza kutolewa kwa awamu na kwamba wangeliweza kuanza na sehemu ya usanifu, hivyo kuweza kui-*break down* katika awamu ya miaka mitatu mitatu. Hivyo kufanya daraja hilo likajengwa katika muda na ahadi ya Serikali itatekelezwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivysema kwenye jibu langu la msingi kwamba Serikali kwa sasa hivi ina mpango wa kuangalia barabara za vijijini na hilo suala la mto Bubu Serikali, inalifahamu, imeishafika *site* na kuangalia uwezekano wa kulijenga daraja hilo, ndiyo maana tumesema kwamba tutaunganisha katika mradi wetu wa barabara vijijni. Kwa hiyo, ninamWomba Mheshimiwa Mbunge aamini hivyo kwamba tutaliangalia kwa umuhimu wa daraja hilo.

Na. 139

**Barabara Kati ya Mererani Na KIA**

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wananchi wa Mji wa Mererani wanajishughulisha na biashara na uchimbaji wa madini ya *Tanzanite,* lakini wamekuwa wakipata taabu ya barabara kati ya Mererani na *KIA;* na kwa kuwa Rais wa Awamu ya Tatu na Awamu ya Nne walipoiona hali hiyo ngumu waliahidi kujenga barabara hiyo isiyozidi kilomita 20 kwa kiwango cha lami:-

Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kujenga barabara hiyo muhimu sana kiuchumi, kutimzia ahadi zilizotolewa na Ma-*Rais* hao.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, napenda kujibu Swali la Mheshimiwa Chrisopher Ole-Sendeka Mbunge wa Simanjiro kama ifuatavyo.

Mheshimwia Naibu Spika, barabara ya Mererani hadi *KIA* iko chini ya mamlaka za Halmashauri za Wilaya ya Simanjaro kwa urefu wa (km 5) na Halmashauri ya Wilaya ya Arumeru kwa urefu wa (km 13).

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kuishirikiana na Halmashauri zote mbili pamoja na Kampuni ya *Tanzanite One* zinaifanyia barabara hiyo mategenezo ya mara kwa mara kuhakikisha kwamba inapitika kwa muda wote wa mwaka. Halmashauri ya Simanjiro kwa mwaka 2006/2007 imetenga shilingi milioni tano kwa ajili ya matengenezo ya kawaida ya hiyo na Kampuni ya *Tanzanite One* imetoa ahadi ya kuendelea kuhakikisha kuwa barabara hii inapitika wakati wote wa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivi sasa Serikali haina mpango wa kutengeneza barabara hii kwa kiwango cha lami kwa sababu ya ufinyu wa Bajeti ya maendeleo ya ujenzi wa barabara. Hata hivyo, kwa sababu utekelelezaji wa ahadi za Mheshimiwa Rais, ziko katika muda wa miaka mitano, Serikali inaendelea kutafuta fedha ili barabara hii iweze kutengenezwa kwa kiwango cha lami.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu yasiyotoa matumaini makubwa ya Mheshimiwa Naibu Waziri, Serikali itakubaliana nami na hasa kwa kuwa Mawaziri wengi wakati wa kipindi cha masika, akiwemo Waziri Mheshimiwa Juma J. Akukweti, ambaye alipata nafasi ya kutembelea maeneo ya Mererani na maeneo ya Kata ya Shambarai na aliona mafuriko makubwa ambayo yalikuwa yanakwamisha wananchi kupita pale, akiwemo Waziri wa zamani wa Nishati na Madini (Mhe. Dr. Ibrahim Msabaha) alishuhudia matatizo yaliyoko pale na Waziri Mkuu, wakati alipokuja kutuendeshea harambe, alishuhudia mwenyewe barabara ilivyokuwa mbovu. Na kwa kuwa kwa kuzingatia hali hiyo Rais wa awamu ya tatu Mheshimiwa Benjamin Mkapa na Rais wa awamu ya nne Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kutambua uzito wa hali hiyo walitoa ahadi ya kutengenezwa kwa barabara hii.

Je, Waziri sasa haoni kwa kusema kwamba hakuna mpango kwa sasa wa kutengeneza barabara hiyo. Anapingana kwa namna moja au nyingine na maelekezo ya wale waliompa dhamana?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kwa kuwa Kampuni ya *Tanzanite One,* imeonyesha nia ya kushirikiana na Serikali pamoja na wadau wengine kutengeneza barabara hiyo ya uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro mpaka Mererani. Serikali, itakubali kutenga fedha za kuweza kutengeneza matuta sijui kama ni matatu kwa kiswahili fasaha, lakini kunyanyua eneo lile la bonde lililoko karibu na kijiji cha Majengo kati ya kijiji cha Majengo na kijiji cha Mesinye katika barabara hiyo inayoelekea Mererani, ili iwezze kupitika wakati wote, wakati tunasubiri fedha hizo zipatikane za kuweka lami, kama ahadi ya wakuu wa nchi ilivyotolewa?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBI (MHE DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kwanza napenda nimhakikishie kwamba umuhimu wa barabara hii unajulikana Serikalini na Wizara ya Miundombinu, ameamua kuanzia mwaka 2007, kupitia *TANROAD,* iichukue barbara na kuanza kuishughulikia, baadala ya kushughuikiwa na Halmashauri ya Wilaya. *(Makoif)*

Mheshimiwa Naibu Spika,kwa hiyo nataka kumhakikishia kwamba tunatambua umuhimu huo na ndiyo maana kuanzia mwakani, tutaanza kutengea fedha katika *TANROADs* ili barabara hii iweze kutengenezwa na baada ya muda mfupi, au miaka michache, basi ahadi hiyo ya kuwekewa lami, ichukuliwe hatua baada ya fedha kutengwa.

Kuhusu ushirikiano na *Tanzanite One,* Serikali iko tayari kushirikiana na Kampuni hiyo ili kuendelea kuboresha barabara hiyo kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa katika swali la msingi, imeonekana kwamba barabara hii ni moja ya ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wakati wa *campaign,* wakati ya Uchguzi Mkuu mwaka 2006. Lakini kwa nyakati tofauti pia hapa tumeelezwa Wabunge kwamba, ahadi za Mheshimiwa Rais, zitawekwa kwenye kitabu, ili pengine kila Mbunge aweze kugawiwa na tuweze kujua ni ahadi ipi itatekelezwa wakati gani na mahali gani. Na kila Mbunge anayehusika aweze kupata kijitabu hicho ili tuweze kuelewa badala ya Wabunge mmoja mmoja pengine kuuliza maswali ya ahadi za Rais katika Bunge hili. Ni lini tutapata ahadi hizo za Rais ili tuweze kuwa nayo katika maeneo yetu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi za Mheshimiwa Rais, zilikuwa zimewekwa katika hii *Kabrasha* ambayo tuliipata wakati wa Mkutano Mkuu uliopita wa Chama cha Mapinduzi, lakini ni kweli kwamba bado kuna makosa ambayo yalionekana au kuna *omission* zingine ambazo zilionekana katika kitabu kile kulingana na namna alivyotoa ahadi Mheshimiwa Rais.

Kitabu kile kinafanyiwa marekebisho na baadaye nadhani Waheshimiwa Wabunge wote watapata tena kile kitabu kilichotolewa kule Chimwaga, kikiwa kimerekebishwa na kuingiza ahadi alizozitoa Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba uniruhusu kwa dakika moja tu, kabla sijauliza swali langu Na. 140, ili niweze kutoa pole kwa uongozi wa Shule ya Sekondari Mbozi, pamoja na Walimu na Wazazi na Wanafunzi. Kwamba jana usiku wa kuamkia leo tarehe 14 Novemba, 2006, nilipaa taarifa kunako majira ya saa tatu usiku kwamba Shule hiyo, bweni moja la Wasichana, limeungua moto na limeteketea lote.

Lakini kwa bahati nzuri wakati huo wanafunzi wa Kidatu cha Pili walikuwa wameondoka, na kwa maana hiyo bweni hilo lilikuwa limegeuzwa kama *store* na walitunza magodoro, vyakula pamoja na masanduku yao ambavyo vyote vimeteketea.

Kwa hiyo ninawapa pole sana kwa tukio hilo na tunalifuatilia, baadaye tutatoa taarifa kamili Serikalini. Baada ya hilo ninaomba sasa swali lijibiwe baada ya kufanyiwa masahihisho kidogo.

Na. 140

**Muda wa Kutembeza Magari ya Serikali**

**MHE. GODFREY W. ZAMBI** aliuliza:-

Kwa kuwa mwaka 1998 Serikali ilitoa Waraka Na. 1 wenye Kumb. SHC/C.180/1/99 wa tarehe 10 Machi, 1998, ambao pamoja na mambo mengine ulisisitiza matumizi mazuri ya gari za Serikali ikiwa ni pamoja na kuagiza gari zote za Serikali ambazo hazipo safarini, au kazi maalum ziwe zimeegeshwa ifikapo Saa 12.00 jioni na kwa zile zitakazofanya kazi siku za mapumziko na kuwa safarini lazima ziwe na vibali vilivyotolewa na Makatibu Wakuu wa Wizara/Idara zinazohusika; na kwa kuwa bado gari nyingi za Serikali na Taasisi za Uma zinaonekana barabarani baada ya saa 12.00 jioni na siku za mapumziko:-

(a) Je, Waraka huo wa Serikali bado unafnya kazi?

(b) Kama jibu la sehemu “a” ni “ndiyo” Je, ni kwa kiasi gani Serikali inasimamia Waraka huo kuona kwamba maagizo yaliyotolewa kuhusu muda wa kutembea gari za Serikali unafuatwa?

(c) Je, ni kwa kiasi gani Askari wa Usalama Barabara wanahusika na ukaguzi wa gari za Serikali na za Mashirika ya Umma ambazo zinakuwa barabarani baada ya Saa 12.00 jioni na siku za mapumziko na ni madereva wangapi wamekamatwa kwa kukiuka Waraka huo na wamechukuliwa hatua gani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zambi (Mbunge wa Mbozi Mashariki) lenye sehemu a, b, na c kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kufanya hivyo naomba nimpe pole, nyingi sana yeye pamoja na wananchi wote wa Mbozi, kwa janga lililotokea jana kule Mbozi.

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Waraka wa Rais Na. 1 wa mwaka 1998 uliotoa maelekezo kuhusu hatua za kubana matumizi ya Serikali bado upo na unaendelea kutumika. Ibara ya 6 ya Waraka huo inatoa maelekezo juu ya matumizi bora ya magari ya Serikali.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Waraka huo, maafisa Wahasibu wamepewa mamlaka ya kusimamia matumizi ya rasilimali zote za Serikali na za Umma zilizo chini yao yakiwemo magari. Suala hili pia limesisitizwa katika Kanuni za Matumizi ya Fedha za Umma za mwaka 2001 kupitia Tangazo la Serikali *(Govenment Notice No.132 of 6th July, 2001).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uwingi wa kazi za Serikali baadhi ya magari hulazimika kuwekewa utaraitbu malum ili yatumike hata nyakati za mapumziko. Utaratibu unaohusika ni ule wa kila Afisa Muhasibu kutoa kibali maalum kwa magari ambayo yanatakiwa kuendelea kufanya kazi zaidi ya muda wa kazi wa kawaida na siku za mapumziko baada ya kuridhika kuwa kazi husika itahitaji huduma ya usafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kushirikiana na vyombo vya Ulinzi na Usalama wakiwemo Askari wa Usalama Barabarani, Serikali huhakikisha kuwa magari yote ya Umma yanayotembea barabarani nje ya muda uliowekwa na siku za mapumziko yana vibali maalum vilivyotolewa na Maafisa Wahasibu.

(c) Mheshimwia Naibu Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 62 kifungu kidogo cha 1 cha Sheria ya Usalama barabarani *(CAP 168 Revised Edition 2002)* Askari wa Usalama barabarani amepewa uwezo wa kukagua na kukamata gari yoyote ambayo inaendeshwa na dereva bila ya idhini ya mwenye gari hilo. Hivyo, kwa mujibu wa Waraka wa Serikali Na. SHC/C.180/1/99 wa tarehe 10 Machi, 1998 Serikali ilitoa agizo kwamba magari yotre ya Umma yawe yameegeshwa ifikapo saa 12.00 jioni kwa siku za kazi na siku za mapumziko. Hivyo, kutokana na agizo hilo Askari wa Usalama barabarani anawajibika moja kwa moja kukamata na kukagua magari ya Umma ambayo yataonekana barabarani baada ya saa 12.00 jioni na siku za mapumziko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi cha mwaka 2002 – 2005 jumla ya magari 18 yalikamatwa na madereva wa magari hayo walipewa adhabu mbalimbali sambamba na Idara husika kuandikiwa barua.

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi hii ni ndogo kutokana na Serikali kuwa makini zaidi sambamba na maofisa wanaotumia mgari hayo kuheshimu taratibu hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kutoa wito kwa Waajiri na Madereva kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Serikali za matumizi ya magari ya Umma.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba niulize kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiusoma Waraka wenyewe ni kweli unaagiza. Kuagiza na kutekeleza ni vitu viwili tofauti, mimi nimeshuhudia gari nyingi za Serikali hata baada ya saa 12.00 jioni unazikuta zimeengeshwa kwenye Ma-*Bar,* na Ma-*Guest Houses,* hapa Dodoma tunaona, pale *Chako ni Chako* ni maarufu, hata gari za baadhi ya Mawaziri unakuta zimeengeshwa pale usiku. Sasa hapo panaruhusiwa gari za Serikali kuegeshwa vipindi hivyo vya usiku, na Serikali iko tayari kuchukua hatua gani sasa. Kwa kuwa mimi nimefanya kazi Serikalini kwa kipindi kama cha miaka mitatu hivi, na kwa sababu nimesafiri na gari hizo, ni mara chache sana Askari wa Usalama barabarani kuzisimamisha hizo gari za Serikali na kuzikagua. Pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri amesema kwamba hizo gari zinakuwa na idhini na hao Ma-*Trafic* wamepewa uwezo wa kukamata hizo gari. Wanawezaje kuzikamata na kujua kama zina vibali, wakati hata kuzisimamisha wanaziongopa gari hizo. Serikali itatoa maagizo gani kwa ajiili ya Ma-*Trafif* hao ili waweze kuzisimamisha gari hizo na kuzikagua? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Naibu Spika, katika jibu la msingi nimesema kwamba kwa ajili ya uwingi wa shughuli za Serikali, mara nyingi magari mengi, hutumika hata baada ya muda uliotolewa kwenye Waraka wa Mwaka 1998. Haya ni magari ambayo pengine Waheshimiwa wanayaona hapa Dodoma yakiwa kwenye Mahoteli. Wakati huo ndipo Madereva wamekwenda kula chakula cha jioni. Mimi siamini kwamba Askkari wa Usalama Barabarani wanaogopa kutekeleza majukumu yao. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine ieleweke kwamba kuna baadhi ya magari ya Serikali hufanya kazi baada ya muda wa kazi bila hata vibali kwa sababu ya hali halisi ya majukumu ya Idara husika. Kwa mfano Magari ya Mawaziri, Magari ya Polisi, Magari ya *TRA,* Magari ya kubeba wagonjwa, magari ya Jeshi la Uhamiaji, Magari ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Magari ya Taasisi ya Kuzuia Rushwa, Magari ya Usalama wa Taifa na kadhalika. Lakini pia ikumbukwe, magari yote ya Serikali hutumia *Log Book.* Maofisa husika huweka sahihi wakati magari yanaanza kazi na magari yakimaliza kazi husika. *(Makofi)*

Na. 141

**Wimbi la Uuzaji wa Kaseti za Picha za Ngono Hapa Nchini**

**MHE. LUCY T. MAYENGA** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika miaka ya hivi karibuni kumezuka wimbi la uuzaji wa kaseti za picha za ngono hapa nchini ambazo zinatishia heshima na maadili ya jamii yetu:-

(a) Je, ni watu wangapi wamefikishwa Mahakamani na kuchukuliwa hatua za kisheria kutokana na makosa ya uingizaji na uuzaji wa mikanda hiyo haramu;

(b) Je, hadi sasa ni nini matokeo ya Serikali katika kupambanana tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. DANIEL N. NSANZUGWAKO)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Taarifa tulizonazo zinasema kwamba mpaka hivi sasa hakuna mtu yeyote aliyewahi kufikishwa Mahakamni na kuchukuliwa hatua za kisheria kutokana na makosa ya uingizaji na uuzaji wa mikanda haramu ya picha za ngono.

(b) Sina shaka kwamba katika sehemu ya pili ya swali lake, Mheshimwia Mayenga alikuwa na maana ya; ni hatua zipi mpaka saa zimechukuliwa na Serikali katika kupambana na tatizo hili. Nami napenda kuendelea kumjibu Mheshimiwa Lucy Mayenga kama ifuatavyo:-

Kutokana na hali halisi ya bidhaa yeneywe yaani (Mikanda ya ngono), ni dhahiri kwamba biashara hiii inafanywa kwa usiri mkubwa kati ya mtu anayeuza na anayeuziwa, na kuwa vigumu sana kwa watu hawa kushikwa kwa urahisi na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo napenda kulihakikishia Bunge hili tukufu kwamba hvi sasa kuna operesheni maalum, inayoendeshwa nchi nzima na Wizara yangu, kwa kushirikiana na Wizara ya Uslama wa Raia na vyombo vingine vya dola, yenye nia ya kukomesha biashara hii haramau ya picha za ngono. Operesheni hii, ambayo ni ya kudumu, tayari imekwishaanza kuzaaa matunda kwa kuwakamata watu wanane Jijini Dar es Salaam kwa makosa ya kuchapisha na kuuza vijarida vya ngono. Watu hawa wamefikishwa Mahakamni na kesi zao zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yangu kwamba, Waaalamu wetu wanaondesha operesheni hii watatumia uzoefu wao; na kubuni mbinu mbali mbali zitakazosaidia kuwanasa wale wote wanaouza mikanda hii ya picha za ngono. Lakini pia napenda kutoa wito kwa wananchi wote ambao wanawajua watu wanaofanya biashara hii haramu, au maduka yanayouza mikanda hii michafu wasisite kutoa taarifa kwa vyombo husika, ili hatua madhubuti ziweze kuchukuliwa. *(Makofi)*

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amethibitisha kwamba Serikali imekuwa ikifanya operesheni maalum katika kuhakikisha kwamba inapamba na tatizo hili. Maswali yangu ni kama hivi ifuatavyo. Je, Serikali, sasa iko tayari kufanya ukaguzi katika haya maduka ambayo huwa yanakodisha kaseti za kawaida ambapo baadhi ya watu ambao siyo waaminifu,

wamekuwa wakitumia nafasi hii, kuweza kukodisha na hata hizi kaseti nyingine ambazo zimekiwa zikichangia katika mmomonyoko wa maadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, je, Serikali iko tayari sasa kuongeza faini kwa watu wote ambao watakutwa na makosa ya kukutwa na hizi kaseti za ngono. Kwa sababu faini iliyopo hivi sasa ni faini ya shilingi 2,000/= ambayo kwa kweli hailingani kabisa na aina ya makosa amabyo mtu anaweza kukamatwa nayo?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. DANIEL NSANZUGWAKO):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika swali la msingi kwamba tumeanza kufanya ukaguzi na watu wanane (8) wametiwa mbaroni. Hizi ni juhudi zilizofanywa katika ukaguzi wa maduka hayo ambayo yanajulikana kwa kuuza na kukodisha mikanda mbali mbali. Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge ninamhakikishia tu kwamba kazi hii ndiyo msingi wa kuwakamata wale wanane katika ukaguzi wao, vinginevyo tusingeliwapata wale wanane. Katika maduka yote ambayo yanauza mikanda hii ya ngono katika miji mikubwa kama Dar es Salaam, Mwanza na Arusha, ukaguzi wa mara kwa mara unaendelea chini ya Sheria yetu hii.

Kuhusu faini, kuongeza faini, labda Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu, niwakumbushe tu kwamba, faini hii ya shilingi 2,000/= ni ya zamani na sheria imeisharekebishwa sasa faini yake sasa hivi ni Sh.200,000/= au kifungo cha miaka miwili (2) jela. *(Makofi)*

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii ili niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Naomba niulize swali hili kwamba kwa kuwa picha hizo za ngono huwa mara nyingi pia zinauzwa na hasa wafanyabiashara ndogo ndogo hasa wale wanaokaa kwenye makutano ya barabara wanaweka *cassette* za kawaida juu lakini kwa chini wanaweka hizo *cassatte* za ngono ukimuuliza bwana unayo *cassette* ya ngono anakwambia ninayo halafu anakuonyesha kwa nyuma. Je, Serikali iko tayari pia kuwashughulikia vijana hao wanaouza picha hizo za ngono barabarani?

(b) Kwa kuwa wakati huo pia mahoteli mengi yaliyokuwa katika Jiji la Dar es Salaam ukiingia kwenye vyumba vyao basi utakuta kuna picha za ngono zinazoonyeshwa ukibonyeza kwenye channel fulani na mimi nimeshuhudia katika picha hizo mpaka nikaenda kumwambia mwenye hoteli aizime sehemu hiyo. Serikali inasemaje kuhusu hilo. *(Makofi?Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza, kwa wale wafanyabiashara ndogo ndogo wanaouza *cassette* na chini yake wanaficha na kuuza kanda za ngono. Kama nilivyosema mwanzo kwamba watu hao wanafanya makosa na katika juhudi zetu hizi za kukamata machapisho na vijarida vya ngono

tumekuwa tukiwashughulikia katika ukaguzi wetu na ndiyo maana watu hao wanane wamekamatwa.

Lakini nikubaliane na yeye kwamba hatua hizi zinaendelea na pia niseme kwamba ndugu zangu suala hili si jepesi sana. Kwa sababu haya mambo yanafanywa kwa usiri na mnajua tena dunia hii nayo imekuwa na utandawazi sana. Kwa hiyo, mambo haya tunakwenda nayo kadri tunavyosonga mbele.

Kuhusu mikanda ya ngono vyumbani ambayo unalipia ili uone kwenye vyumba vya hoteli, ni kweli katika mahoteli mengi duniani hiyo inafanyika, lakini labda ndugu yangu Mheshimiwa Abdulkarim Shah tungefika mahali tukajua ni hoteli zipi hizo zinafanya mambo haya ili tuweze kujua ni hatua zipi muafaka tuweze kuzichukua kuhakikisha kwamba tabia hiyo tunaikomesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia niendelee kusema kwamba jamani Tanzania hatuko Kisiwani peke yetu, duniani leo katika mahoteli makubwa hayo ya kitalii *Five Star, Six Star Hotels* unakuta mambo hayo yanafanyika, lakini angalau basi katika hoteli hizo yanafanyika kwa usiri. Lakini tatizo letu kubwa ni biashara hii ya mikanda kama lilivyoulizwa swali la msingi ambayo inauzwa hadharani na hakika kukiuka maadili yetu katika Taifa letu.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kujibu swali hili kwa ufasaha zaidi. Lakini nataka niseme hili suala la televisheni katika vyumba vya mahoteli lipo dunia nzima na wanaotaka kuona lazima kwanza walipe, halafu kuna namba za siri, na kuna masharti kwamba waangalie watu wazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni jambo ngumu sana Serikali kuingilia mambo ambayo kuna televisheni za Kimataifa na kuwazuia watu. Nafikiri la msingi ni kwamba Waheshimiwa Wabunge sisi tuwe mfano kutoangalia filamu kama hizo. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 142

**Mashindano ya Uzuri**

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** aliuliza:-

Kwa kuwa nchi kuwa na utamaduni wake ni muhimu, na nchi kuiga utamaduni wa nchi nyingine ni vizuri pia ili mradi ule utamaduni unaoigwa ulete maendeleo katika jamii ya nchi husika na pia usivuruge mila na desturi za utamaduni wa nchi na sheria za nchi yetu:-

(a) Je, mashindano ya uzuri yanayoendelea nchini mwetu yana uhusiano wowote na mila, desturi na utamaduni wa nchi yetu, na kama upo unatokana na kabila gani na Mkoa upi?

(b) Kama ni lazima sana mashindano hayo yafanyike. Je, kwa nini yasiwe kama yale ya *Miss Bantu* ambayo vile vile ni utamaduni wetu unatangazwa na kuweza kuigwa na nchi nyingine?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwanawetu Said Zarafi, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, hapa nchini kwetu tunaendesha: “Mashindano ya Urembo” na siyo “Mashindano ya Uzuri”. Kila mtu ana uzuri wake kimaumbile, kulingana na yule anayemtazama. Baada ya ufafanuzi huo mfupi, sasa naomba nimjibu Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Mashindano ya Urembo hayana uhusiano wa moja kwa moja na mila na desturi za kabila lolote wala Mkoa wowote hapa nchini Tanzania.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haina tatizo, wala hioni ubaya wowote wa mashindano ya urembo kufanyika hapa nchini, ili mradi tu yafanyike kwa kufuata mila na desturi za nchi yetu; hasa tukizingatia kwamba mashindano kama haya, kwa namna moja ama nyingine, pia yanaitangaza nchi yetu kiutamaduni na kiutalii, pamoja na kuongeza ajira kwa vijana wanaoshiriki.

Hivyo basi, hata mashindano ya *Miss Bantu* si vibaya yakaendelea sambamba na mengine yaliyoanzishwa au yatakayoanzishwa katika nyanja tofauti kama vile Miss *Tanzania, Miss Tourism, Miss Environment*. na kadhalika. Mashindano haya yalianzishwa ili kutoa changamoto nyingine kwa wapenzi wa urembo ili waweze kushiriki kwa kutumia masharti, vigezo na vionjo vya Kitanzania, mbali na vile vya Kimataifa vinavyotumika katika mashindano mengine ya urembo.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa mashindano hayo licha ya kwamba yanatoa maadili, sikubaliani kwanza na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri moja kwa moja. Mashindano hayo ninavyofahamu yanatoka nje ya maadili kwa sababu hata yale mavazi yanayovaliwa pale siyo ya maadili na utamaduni wa nchi yetu. *(Makofi)*

Lakini kwa kuwa mashindano hayo vile vile yanaleta mafundisho kwa vile kunakuwa na maswali ambayo yanaleta mafundisho kwa jamii. Ni vigumu mashindano hayo kuyaondoa.

Lakini swali langu la nyongeza linakuja kwamba je, hatuwezi tukafanya mashandano yetu kulingana na utamaduni wa nchi yetu na mila na desturi za hapa

Tanzania? Halafu kwa wale wanaoshinda kwa mashindano hayo ya nje kama wanavyotaka utamaduni wao. Kwa nini wanapoenda huko nje wasiendelee na jinsi yanavyotakiwa kule nje baada ya kufanyika inavyotakiwa hapa kwetu Tanzania? *(Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO):** Mheshimiwa Naibu Spika, mashindano haya yanatoka nje ya maadili yetu. Mashindano haya ya urembo kama nilivyosema yanatangaza utamaduni wa Taifa letu, yanatangaza utalii katika nchi yetu na mashindano haya ya urembo ni mchakato mzima wa utandawazi katika dunia ya leo wala Tanzania hatuwezi kuwa Kisiwa peke yetu tu kwamba tutafanya ya kwetu peke yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hata hivyo, viko vigezo maalum ambavyo vinatumika katika mashindano hayo. Kwa mujibu wa sheria yetu ya Baraza la Sanaa mavazi yale ambayo hayapendezi na hayajengi heshima yamezuiliwa ikiwa ni pamoja na vichupi ambavyo havifai yanaendelea kuzuiliwa chini ya sheria hii. Je, hatuwezi kufanya mashindano ya kwetu peke yetu jibu ni ndiyo au hapana. Jibu ni ndiyo kwa maana ya kwamba tunafanya ya kwetu. Kwa mfano, yanapofanyika mashindano ya *Miss Ilala* kwa mfano, *Miss Kinondoni,* kwa mfano, *Miss Utalii* kwa mfano, yanatumia vionjo vya Kitanzania na yanatumia vigezo ambavyo vinawekwa kwa mujibu wa waratibu wa mashindano hayo.

Lakini washiriki hao warembo wanapokwenda kwenye mashindano ya Kimataifa lazima wafuate vigezo vilivyowekwa kwa mujibu wa mashindano yale ya Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine kama Mheshimiwa Mbunge kama anapenda naweza nikamweleza ni vigezo gani vinatumika katika mashindano ya nyumbani na vigezo vinavyotumika katika mashindano ya Kimataifa.

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mashindano hayo ya urembo kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri yanakwenda kufuatana na matakwa ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Serikali haioni kwamba jinsi washindani wanavyotokea kwenye jukwaa na namna wanavyokuwa wamevaa na hili hata ukirudisha kwenye swali la nyuma ni njia moja ya kuashiria kuonyesha vitendo vya ngono ambavyo vinaonyeshwa hadharani?

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO):** Mheshimiwa Naibu Spika, si kweli kwamba mashindano hayo yanaamsha utashi wa kupenda ngono, si kweli hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine hizi ni hisia kwa watu wanaokwenda kuangalia maonyesho hayo wakiwa wao wenyewe kiakili, kisaikolojia wanakuwa na matamanio yao wao wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kimsingi lengo ni kuendeleza mashindano hayo ili yaendelee kutangaza Taifa letu kwa kiutamaduni na kitalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mavazi kama nilivyosema mwanzo, suala la mavazi limejadiliwa na tunaendelea kulishughulikia kwamba yale mavazi ambayo hayapendezi kimsingi yamezuiliwa, na ni jukumu letu kama Serikali kuendelea kuhakikisha kwamba mashindano hayo yanakuwa ni kioo halisi cha Utamaduni wa Mtanzania.

Na. 143

**Kilimo cha Soya - Newala**

**MHE. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Tanzania inazalisha zao la Soya kwa asilimia kumi (10%) ya mahitaji yake na asilimia tisini huagizwa kutoka nchi za nje; na kwa kuwa yako maeneo ambayo Soya inastawi sana ikiwa ni pamoja na Wilaya ya Newala hasa Tarafa ya Chilangala na Kitangari ambako Serikali za Vijiji zilifanikiwa kununua malori kutokana na kilimo cha Soya katika mashamba ya vijijini; na kwa kuwa, kilimo cha soya Wilayani Newala kilisimama kwa kukosa soko la uhakika:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufufua kilimo cha Soya Wilayani Newala ili kupunguza suala la kuagiza Soya toka nchi za nje na kupunguza matumizi ya fedha za kigeni katika uagizaji huo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Capt. George Huruma Mkuchika, Mbunge wa Newala, napenda kutoa maelezo ya awali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, zao la Soya lina protini nyingi sana yenye bora wa hali ya juu kuliko iliyoko katika aina nyingine ya mazao ya mimea na hata kuzidi kiasi cha protini katika nyama, mayai na maziwa. Sifa nyingine za zao la soya ni pamoja na kuwa na mafuta yaisyokuwa na lehemu *(cholesterol),* na uwezo wa mmea wa soya kuongeza mbolea aina ya nitrojeni kwenye udongo, gharama ndogo za uzalishaji ukilinganisha na mazao mengine, wingi wa protini unaoweza kuondoa utamiamlo hususan kwa watoto na kinga kwa magonjwa ya kansa, shinikizo la damu na kuwaongezea nguvu wagonjwa wa UKIMWI na magonjwa mengine.

Aidha, uwezo wa soya kustawi katika maeneo yanayostawisha mahindi na maharage unamaanisha kwamba zao hilo linaweza kulimwa sehemu nyingi nchini Tanzania. Sifa hizo zimefanya zao la soya kuwa umuhimu katika chakula cha binadamu na mifugo na katika kutengeneza bidhaa mbalimbali za vyakula na madawa.

Katika miaka ya 1970, Wilaya ya Newala ilikuwa inazalisha soya kwa wingi lakini uzalishaji ulipungua baada ya Taasisi za *NMC* na *GAPEX* zilizokuwa zinanunua zao hilo kuzorota na kuwafanya wakulima kukosa soko. Pamoja na faida za soya, zao hili halifahamiki vizuri kama ilivyo kwa mazao mengine. Baada ya maelezo hayo ya awali, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kapteni Mkuchika, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa zao la soya, Wizara yangu imeanza kutoa elimu kwa wakulima, Maafisa Ugani na wadau wengine kuhusu kilimo bora cha zao la Soya. Aidha, katika mwaka wa 2006, Wizara yangu imechapisha kijitabu kinachoitwa: "Kilimo bora cha zao la Soya" kwa lengo la kuwafahamisha wadau faida zinazotokana na zao la soya. Wataalam wanaendelea kufanya utafiti wa zao hili na kati ya mwaka wa 2002 na 2004 aina nne za soya zinazojulikana kama *Uyole SOYI, Eximutunu, Ex-laela, Duicker* na Kaleya zilizotolewa na Vituo vya Utafiti kwa ajili ya kuzalishwa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada nyingine zilizokwishafanywa ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuanzia msimu wa 2003/2004, tani nane za mbegu bora za soya zilizalishwa na kusambazwa katika Mikoa ya Iringa, Mbeya, Ruvuma, Rukwa, Arusha, Kilimanjaro, Dodoma na Singida.

(ii) Wakulima 200 na wataalam 50 wamepatiwa tayari mafunzo juu ya kilimo bora, usindikaji na matumizi ya zao la Soya.

(iii) Katika mwaka 2005 warsha ya kuwahamasisha wafanyabiashara ilifanyika. Kutokana na warsha hiyo baadhi ya wafanyabiashara wa soya wameingia mkataba na wakulima 700 katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kununuaa jumla ya tani 500 za soya zitakazozalishwa katika msimu wa 2006/2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa 2006/2007 Wizara yangu itapeleka mbegu bora na kufundisha wananchi matumizi ya soya kwa ajili ya chakula cha binadamu na mifugo katika Wilaya za Newala, Nachingwea, Tandahimba na Kilwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kusema Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika imetoa kijitabu hiki nilichokishika kinaitwa: Kilimo Bora cha Zao la Soya. Kijitabu hiki kitagawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge wote leo hii ili waweze kuona umuhimu wa zao hilo. *(Makofi)*

**MHE. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Napenda nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri yaliyowapa matumaini wapiga kura wangu wa Newala kule Chilangala na Kitangari kwamba Serikali imo mbioni kufufua kilimo cha zao la soya katika Wilaya ya Newala.

Swali la msingi lilitaka kujua mipango ambayo Wizara inayo kwa Wilaya ya Newala. Mheshimiwa Naibu Waziri ametoa maelezo mazuri ya faida ya soya na mahali gani patasaidiwa. Lakini swali la msingi lilitaka kujua Serikali ina mpango gani madhubuti wa kufufua kilimo cha soya Newala.

Sasa swali kwa kutambua kwamba Newala hakuhitaji utafiti tena maana Wizara imethibitisha kwamba tunalima soya. Je, Wizara iko tayari kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Newala kuanzisha mpango maalum wa kilimo cha soya katika Wilaya ya Newala?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika majibu yangu ya swali la msingi tayari tumekwishaanza utaratibu wa kufufua zao hili la soya katika Mikoa hiyo na tumeanza na Mkoa wa Mtwara na Lindi na Newala ni Wilaya mojawapo ambayo tumeipanga kuendelea nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu yangu ya mwisho nimesema tuna mpango wa kupeleka mbegu bora kuwafundisha wananchi na nina hakika kabisa kwamba Wilaya ya Newala siyo ngeni katika zao hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Wilaya ya Newala nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutafanya utaratibu kwa kuwa wao wana uzoefu tutawafanya kama ndiyo *pilot* ili zao hili liweze kuenea katika maeneo mengine.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali moja ndogo la nyongeza. Wananchi wengi wakiwemo wananchi wa Mkoa wa Mbeya wameitikia wito sana wa kulima hayo mazao yajulikanayo kama *non traditional crops* ikiwemo soya, mbaazi na mbegu za mafuta ili waweze kuuza nje.

Je, Serikali iko tayari kukiagiza kitengo cha masoko chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kutafuta masoko ya uhakika na bei zake mapema na kuzitangaza kwa wakulima ili wenye nia ya kulima mazao hayo wawe na moyo wa kuweza kuyalima mara kwa mara wanapotaka? Ahsante sana. *(Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze na niwapongeze wakulima wa Mbeya kwa kuitikia

wito huo wa kuanza kulima mazao ambayo ni *non traditional* kwa sababu sisi wenyewe tunasisitiza jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali iko tayari na Wizara yangu itashirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kuwasaidia wananchi hao kutafuta masoko ya mazao hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niongeze tu kwamba baadhi ya mazao kama siyo yote kama hili la soya linapata soko kubwa zaidi baada ya kusindikwa. Zao la soya kwa mfano, ni kwamba ukilila lenyewe kama maharage hupati protini ya aina yoyote linatoka kama ulivyolila. Lakini ukishalisindika linatoa protini ile ambayo ni nyingi kuliko hata ile ya nyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge na tutashirikiana na Wizara husika kuweza kuwatafutia masoko na hasa kuhimiza usindikaji.

Na.144

**Vitendea Kazi kwa Askari Polisi na Traffic Police**

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD** aliuliza:-

Kwa kuwa Askari Polisi wa Doria na wale wa Usalama Barabarani; hasa wale wa Zanzibar wana upungufu wa vitendea kazi na kusababisha utendaji wao kuwa mgumu:-

Je, ni lini Serikali itawapatia vitendea kazi Askari hao ili watimize wajibu wao ipasavyo?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mbunge wa Jang'ombe, swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua upungufu mkubwa wa vitendea kazi unaolikabil Jeshi la Polisi vikiwemo vifaa kwa ajili ya Askari wa Doria na Askari wa Usalama Barabarani wa Zanzibar na Tanzania kwa jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetenga fedha katika bajeti yake mwaka huu wa fedha wa 2006/2007 kwa ajili ya kununua vifaa mbalimbali kwa Askari wetu.

Serikali itanunua magari, pikipiki , vifaa vya mawasiliano, virungu, unifomu kwa ajili ya Askari wa doria. Aidha, Serikali kwa mwaka huu wa fedha imepanga

kununua vifaa kwa ajili ya Askari wa Usalama Barabarani vikiwemo *Reflector, speed radar, Alcohol tester, Helmet*, *computer* kwa ajili ya kutunza kumbukumbu za uhalifu na wahalifu, makoti ya mvua, pikipiki na kadhalika pamoja na kupatikana kwa vitendea kazi hivyo, Jeshi la Polisi litaendesha mafunzo ya sheria za usalama barabarani kwa askari wote watakaokuwa wanajiunga na Vyuo ili kila askari aweze kuzielewa sheria hizo na kuzisimamia hata kama hayupo Idara ya *Traffic* ili aweze kutenda kazi kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na nia hiyo nzuri ya Serikali, lakini bado uwezo wa Serikali kifedha ni mdogo kuweza kununua vifaa vya kutendea kazi kwa askari wote nchini kwa wakati mmoja. Hivyo vifaa vitakavyopatikana vitapelekwa kwanza sehemu zenye upungufu mkubwa na sehemu nyingine zitaendelea kupata vifaa kadri hali ya fedha itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara yangu kupitia Jeshi la Polisi imekuwa inawashirikisha wadau mbalimbali wenye nia na uwezo kwa kulisaidia Jeshi la Polisi kuchangia vitendea kazi. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba wadau wengi wakiwemo Waheshimiwa Wabunge wameitikia wito wetu na wamechangia vifaa mbalimbali yakiwemo magari na pikipiki. Napenda kutumia nafasi hii kuwashukuru sana wadau wote hasa Waheshimiwa Wabunge waliochangia Jeshi la Polisi.

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nia ya Serikali ni nzuri na tunajua kwamba imo katika jitihada ya kutaka kufanikisha ili watendaji waweze kufanya kazi zao vizuri. Lakini ahadi zinakuwa nyingi na muda unakuwa mrefu. Je, ni lini watawapatia vifaa hivyo kwa Askari hao?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba kwa mwaka huu wa fedha 2006/2007 tayari Serikali imetenga fedha na imetenga shilingi bilioni 8 kununua vifaa hivyo. Namhakikishia kwamba mwaka huu wa fedha vifaa hivyo vitanunuliwa na Zanzibar vitapelekwa.

Na. 145

**Uhitaji wa Kituo cha Polisi Ngaramtoni**

**MHE. ELISA D. MOLLEL** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mji wa Ngaramtoni ya Juu una wakazi na wafanyabiashara wengi na unakua kwa kasi kubwa; na kwa kuwa, huduma za jamii hususan za usalama wa raia ni duni, hasa ikizingatiwa kuwa Mji huo una Kituo cha Polisi chenye chumba kimoja tu:-

Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi kitakachokidhi mahitaji na Usalama wa Raia wa Mji huo kulingana na ongezeko la watu?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, napenda kumjibu Mheshimiwa Elisa Mollel, Mbunge wa Amerumeru Magharibi, swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Elisa Mollel kuwa Mji wa Ngaramtoni unakua kwa kasi hivyo Kituo cha Polisi kilichopo ni kidogo, hali ambayo inafanya utendaji wa kazi za Polisi kuwa mgumu. Kutokana na hali halisi ya uwezo wa Serikali kifedha, kwa sasa Serikali haina mpango wa kujenga Kituo kikubwa katika eneo hilo. Hata hivyo, mara hali ya fedha ikiruhusu, Kituo cha Ngaramtoni ni kimoja katika vituo vinavyopewa kipaumbele katika mpango wa ujenzi wa Vituo vya Polisi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwa Mheshimiwa Elisa Mollel, atachukua hatua za kuhamasisha wananchi kujitolea katika ujenzi wa kituo kipya, Serikali itaunga mkono jitihada hizo.

**MHE. ELISA D. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa ruhusa ya kuuliza swali moja ndogo la nyongeza. Kwa kuwa moja ya majukumu ya Jeshi la Polisi ni kuzuia na kudhibiti uhalifu katika jamii. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba sasa wakati umefika wa kuongeza Vituo vya Polisi angalau kwa ngazi ya Kata ili kupeleka huduma hii muhimu karibu na wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakubaliana naye kwamba kazi kubwa ya Jeshi la Polisi ni kudhibiti usalama wa raia na mali zao, na jukumu hilo Serikali itaendelea kulifanya kupitia Jeshi la Polisi.

Aidha, nakubaliana naye kuhusu umuhimu wa kuwa na Vituo vya Polisi katika maeneo mbalimbali nchini yakiwemo ya Kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa hivi karibuni wakati nikijibu swali hapa Bungeni nilieleza kwamba sasa hivi Jeshi la Polisi lina mpango wa kufanya tathmini ya kina kwa maana ya *Master Plan* ya nchi nzima kujua mahitaji halisi ya Vituo vya Polisi kwa nchi nzima kwa kufuata vigezo vya Polisi na mazingira ya sasa.

Kwa hiyo, mara mpango huo utakapokamilika utawasilishwa Serikalini na hatua zingine zitafuata kwa mujibu wa uwezo wa Serikali ili tuweze kujenga Vituo pale ambapo vinahitajika.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Katika Mkutano huu Mheshimiwa Naibu

Waziri, alijibu swali kuhusiana na ujenzi wa Kituo cha Polisi Kalinzi na katika majibu yake ambapo swali lilikuwa kama hili alisema kwamba hakukuwepo na mpango wowote na wala hakukuwepo na vipaumbele kwa ajili ya Vituo vya Polisi. Sasa je, Serikali ina *double standard*?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nimhakikishie kwamba Serikali haina *double standard* na *Hansard* zipo na majibu yangu yapo nilieleza kabisa kwa uwazi kwamba Serikali itafanya tathmini ya kina kuona mahitaji ya Vituo vya Polisi nchini na hatua zitachukuliwa. Tutawasilisha mpango huo Serikalini na mara tutakapowasilisha tutasema kwamba tutapata utatuzi wa kudumu wa suala hili. Hivyo, namwomba Mheshimiwa Kabwe Zitto akasome *Hansard* ili aone majibu yangu yalivyo sahihi kwa siku ile. *(Makofi)*

Na. 146

**Hospitali za Wagonjwa wa Akili**

**MHE. ALI SAID SALIM** aliuliza:-

Je, kuna hospitali ngapi za Wagonjwa wa Akili hapa nchini na ni huduma gani zinazotolewa kwa wagonjwa katika hospitali hizo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ali Said Salim, Mbunge wa Ziwani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania Bara ina Hospitali Maalum za Wagonjwa wa akili mbili nazo ni Mirembe iliyoko Mkoani Dodoma ambayo ni mali ya Serikali na Lutindi iliyoko Korogwe Mkoani Tanga inayomilikiwa na Kanisa la Kilutheri. Aidha, katika Hospitali za rufaa za Muhimbili, Bugando na Mbeya na Hospitali za Mikoa za Iringa, Kagera, Kigoma, Kilimanjaro, Morogoro, Mtwara, Ruvuma na Tabora kuna wodi au vitengo maalum kwa ajili ya tiba ya wagonjwa wa akili. Kwa upande wa Tanzania Visiwani ipo hospitali ya Kidongo Chekundu Mjini Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za wagonjwa wa akili zinazotolewa katika hospitali hizi ni kama ifuatavyo:-

(i) Huduma ya tiba kwa kutumia dawa, aidha zikiwa kwa mtindo wa vidonge au sindano (*anti-psychotic drugs*).

(ii) Huduma ya tiba ya kutumia umeme (*Electro Convulsive Therapy*).

(iii) Ushauri (*Psychotherapy)* unaolenga kubadili tabia ambazo zinamkwaza mgonjwa kimaisha ili kujielewa zaidi na kujijengea mbinu ambazo zitamwongezea ufanisi wa kukabiliana na changamoto za kila siku.

(iv) Elimu ya kinga na mbinu za kuboresha afya ya akili.

(v) Usalama wa kiwango cha juu kabisa (*maximum security setting*) kwa wagonjwa ambao katika hali ya kuchanganyikiwa wamehusishwa na matukio ya kuua au kujeruhi.

(vi) Huduma ya utengamao *(Rehabilitation)* ambapo wagonjwa hupewa stadi mbalimbali za maisha kama vile ushonaji, ufumaji, ujenzi, kilimo, ufugaji, na kadhalika ili kuwawezesha kumudu maisha ndani ya jamii mara baada ya kuruhusiwa kurejea nyumbani.

(vii)Huduma kwa wathirika wa dawa za kulevya.

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize maswali kidogo ya nyongeza. Nitakuwa na swali moja tu la nyongeza, lakini litakuwa na sehemu (a), (b) na (c).

**NAIBU SPIKA:** Itakuwa (a) na (b) basi, maswali mawili. Tunaendelea.

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, basi baada ya masahihisho hayo, nitakuwa na maswali mawili ya nyongeza.

La kwanza, kwa kuwa kama alivyosema Naibu Waziri kwamba huduma inayotolewa hapa ni matibabu kama ni ya vidonge au ni ya sindano; Na kwa kuwa vidonge hivi au sindano hizi anapopewa mgonjwa zinahitaji chakula cha kutosha ili ziweze kufanya kazi vizuri mwilini na tafiti yangu inaonyesha kwamba huduma ya chakula inayotolewa katika hospitali hizi haikidhi haja ya mgonjwa kuweza kumudu kufanya kazi vizuri mwilini, hasa hospitali ya Milembe ambayo mimi binafsi nimeitembelea:

Je, Serikali haioni iko haja sasa ya makusudi kabisa ya kufikiria kuongeza chakula kwa ajili ya wagonjwa hawa ili dawa hizo ziweze kufanya kazi vizuri na baada ya muda mfupi waweze kutolewa na kuungana na Watanzania wengine katika shughuli za kimaisha?

La pili, baada ya utafiti wangu, inaonyesha kwamba huduma ya malazi katika hospitali hii ya Dodoma, pia hairidhishi kwa kuwa ndani ya vyumba wanavyolala, huduma ya wadudu wanaoambua mwili imekuwa ni ya kupita kiasi, kiasi ambacho mgonjwa baada ya kupona akili, hulazimika akitoka nje aende akatibu ugonjwa wa ngozi.

Je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba iko haja sasa ya kuanzisha utaratibu maalum na endelevu wa angalau kupuliza dawa za kuulia hawa wadudu katika vyumba hivi ili wagonjwa hawa watakapotoka waweze kuwa na afya nzuri?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba mbali na matibabu, vidonge na sindano, chakula ni muhimu. Lakini, napenda nisimkubalie Mheshimiwa Mbunge hasa aliposema kwamba chakula cha Mirembe kwa utafiti wake alioufanya, kwamba hakitoshelezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 10/11/2006 nimetembelea Mirembe na nilikuwa nimefuatana pia na Mheshimiwa Mbunge wa Dodoma Mjini, pamoja na Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Dodoma.

Chakula kilichoko pale nilichokiona ni chakula *standard*. Nimekuta chakula pale, wali na maharage ambayo Serikali imenunua ambacho chakula hiki, wali ni *carbohydrates* na maharage ni *protein*. Kwa hiyo hiki chakula kilishe kinatosheleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini si hivyo tu, wale ambao wanaonekana wana mahitaji ya ziada kuhusu chakula, huwa wanapewa maziwa na wanapewa na mayai. Kwa hiyo, tafiti zake alizozifanya, labda kama ataniletea tuje tuone. Lakini hiyo ndiyo hali halisi ambayo nimeiona tarehe 10/11/2006. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili, Mheshimiwa Mbunge anadai kwamba hali halisi ya malazi pale hospitalini Mirembe, haijaridhisha. Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nilieleze Bunge lako Tukufu kwamba tuelewe kwamba wagonjwa wanapokuja pale kutoka majumbani, wanakuja katika hali ngumu sana kwa sababu familia nyingi zimekuwa zikiwatenga. Kwa hiyo, wanakuja ni wachafu, wakiwa wamejaa chawa na kadhalika. *(Makofi)*

Wanapofika pale hospitalini, kuna utaratibu wa kumchukua mgonjwa na wagonjwa wale wanabadilishwa na wanapelekwa wodini.

Mheshimiwa Naibu Spika, inapofikia kwamba yule mgonjwa kabla hajafanyiwa usafi, tufahamu kwamba mgonjwa anapokuja pale anakuwa amechanganyikiwa na anakuwa *aggressive* kiasi kwamba huwezi ukamfanyia usafi. Kwa maana hiyo, pale mgonjwa inabidi kwanza umpe dawa ili aweze kutulia ndio usafi mwingine kwa mfano wa kukata nywele ambazo zinakuwa na chawa ndio unaweza kumfanyia, vinginevyo inakuwa tena ni athari kwamba mfanyakazi anaweza akaumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala hilo siyo hicho tu, hospitali ya Mirembe ina mashine kubwa sana ambayo ni *heavy duty* inafua nguo za wagonjwa halafu zile nguo wanazozitumia pale zinaua chawa ambao ni wadudu, wale chawa ambao siyo mayai. Ile mashine haiwezi ikaua mayai ya wale chawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini, napenda tu niwafahamishe Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla. Tuhakikishe kwamba wale wagonjwa wa akili tuwahudumie kama ni ndugu zetu, ni watoto wetu na kadhalika. Kwa sababu wanapokuja pale wanakuja katika hali ngumu sana kwa sababu siyo rahisi leo unafanya *fumigation*, kesho mgonjwa mwingine anaingia analeta chawa kutoka kule kwenye jamii halafu unafanya tena *fumigation.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mimi naomba tusaidiane, tunapoleta wagonjwa wetu wanapofanyiwa rufaa basi tusaidie kwa sababu huwezi kufanya *fumigation* leo na kesho mtu analeta chawa unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hali niliyoiona mimi juzi nilipoenda kutembelea, mashahidi Wabunge niliowataja. Mashuka ni masafi, mablanketi ni safi. Isipokuwa tatizo ni kwamba kuna msongamano tu mkubwa kwa hiyo hali inakuwa ni ngumu ukizingatia kwamba kuna uhaba mkuwa sana wa watumishi. Ahsante. *(Makofi)*

Na. 147

**Tatizo la Usafiri – Sekondari ya Mbeya**

**MHE. BENSON M. MPESYA** aliuliza:-

Kwa kuwa miongozini mwa shule kubwa zenye watoto wengi katika Jiji la Mbeya ni pamoja na Mbeya Sekondari ambayo inakabiliwa na tatizo kubwa la usafiri hasa usiku kwa wanafunzi wa *hostel* ambao ni wasichana: Je, ni lini Serikali itaipatia shule hiyo gari jipya?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima kabla ya kujibu swali, nakuomba unipe ruhusa kwa ndugu zangu wa Jimbo la Mkinga ambao wamepatwa na mafuriko katika mvua hizi zinazoendelea za Vuli. Kiasi cha watu 320 hawana mahali pa kuishi, chakula ni cha tabu na wana mahitaji makubwa. Naomba niwaarifu kupitia Bunge hili kwamba niko pamoja nao na tunaomba ndugu jamaa na wale wote wenye nia njema watusaide kuwapatia hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Benson M. Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ina jumla ya sekondari 1276. Kati ya hizo, ni shule 40 tu zina magari. Serikali inandaa utaratibu wa kutoa huduma ya usafiri katika shule za sekondari kwa kuteua shule moja ambayo itapewa gari litakalohudumia pia shule zilizo karibu. Kwa sasa shule ya Sekondari ya Mbeya inaweza kupata huduma ya usafiri kwa kutumia gari lililopo katika Shule ya Sekondari ya Loleza.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa mpango wa kuzipatia shule angalau gari moja kwa kila *catchment area*, ni mpango wa muda mrefu ambao Serikali ilitoa ahadi katika Bunge hili. Na kwa kuwa kumekuwa na malalamiko mengi ya wanafunzi pamoja na walimu. Je, ni lini basi Serikali itakuwa tayari sasa kutekeleza hili la angalau gari moja kwa kila *catchment area* ili tuondoe kelele na kero ambazo walimu wengi wamekuwa wakilalamika?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima kabla ya kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Benson M. Mpesya, naomba nitumie nafasi hii kutoa pole kwa wananchi wa Mbozi ambao wamepatwa na matatizo kwa kuunguliwa na bweni na kwamba baada ya Bunge hii tutajitahidi kutafuta wasaa twende tukaungane nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo naomba niseme kwamba shule ya Sekondari ya Mbeya inalo gari ambalo si zima sana lakini liko barabarani. Hivyo basi, tutajitahidi kwa kadri tutakavyoweza tupate gari tuwawekee kwenye hayo maeneo ambayo tumeyataja. Hii ndio nia ya Wizara yangu. Ninaami tutakapokuwa tumemaliza mikakati ya ujenzi wa madarasa ya MMES na kuhakikisha vifaa vimekamilika, jambo litakalofuatia litakuwa ni kuwapatia usafiri. Ni kweli tunafahamu umuhimu wa kuwa nao na tunaelewa uzito wa matatizo yaliyopo.

Na. 148

**Miradi Inayotekelekzwa na TANESCO**

**MHE. HERBERT J. MNTANGI** aliuliza:-

Kwa kuwa hali ya Shirika la *TANESCO* inaonyesha kudhoofika kiuwezo hasa kwa utekelezaji wa miradi ya usambazaji umeme nchini kutoka vyanzo vyake vya mapato nje ya michango ya wahisani au kutoka Serikalini.

(a) Je, miradi ya thamani gani ambayo *TANESCO* ilitekeleza kwa mwaka 2004, 2005 na 2006 kutoka katika vyanzo vyake vya mapato?

(b) Je, kwa Bajeti ya mwaka 2006/2007 *TANESCO* inatarajia kutekeleza miradi gani na ya thamani gani kutoka kwenye vyanzio vyake vya mapato?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mbunge wa Muheza, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2004 – 2005, *TANESCO* kama msimamizi wa utekelezaji wa miradi ya umeme nchini, ilitumia jumla ya shilingi bilioni 42.522. Kati ya hizo, *TANESCO* ilitumia shilingi bilioni 25.73 kutoka kwenye vyanzo vyake. Serikali ilichangia bilioni 2.384 na wafadhili walichangia shilingi bilioni 14.408. Miradi iliyotekelezwa ni pamoja na usambazaji umeme vijijini.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu kwenye sehemu ya kwanza ya swali, kazi ya kubwa ya *TANESCO* ni kusimamia utekelzaji wa miradi ya umeme ya Serikali. Ktika mwaka wa fedha wa 2006/2007, *TANESCO* inatarajia kusimamia miradi ya usambazaji wa umeme vijijini itakayogharimu jumla ya shilingi bilioni 39.39 kwa mwaka wa fedha wa 2006/2007. Vyanzo vya fedha hizo ni Serikali na Wafadhili. Hakuna fedha zitakazotumika kwenye miradi hiyo katika mwaka wa fedha 2006/2007 kutoka kwenye vyanzo vya *TANESCO* yenyewe.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, namshukuru Mheshimiwa naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyotoa. Hata hivyo nina

maswali madogo mawili ya nyongeza: Kutokana na maelezo aliyotoa Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba katika kipindi cha mwaka 2006/2007 *TANESCO* itakuwa haina uwezo wa kuwa na vyanzo vyake vya mapato katika shughuli zake za uendeshaji.

Je, ni matatizo gani ambayo yamefanya *TANESCO* kushindwa kuweza kujitegemea na kujiendesha hasa ukizingatia kwamba sasa hivi Menejimenti yake imewekwa mikononi mwa wageni?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kuna miradi ambayo *TANESCO* iliahidi kutekeleza kule katika Wilaya ya Muheza na *TANESCO* yenyewe ina mradi wa uzalishaji umeme pale Hare katika Mkoa wa Tanga.

Lakini kuna vijiji ambavyo viko jirani sana na eneo hili la uzalishaji umeme, lakini havina umeme na hivi karibuni Mheshimiwa Waziri Mkuu alipotembelea katika Kata hiyo ya Songa Kijiji cha pale Songa, aliulizwa maswali ni lini *TANESCO* itaweza kuwasaidia wananchi wanaoishi jirani na vyanzo hivi vya uzalishaji wa umeme vitaweza kupata umeme. Je Mheshimiwa waziri anaweza kutusaidia leo kujibu swali hilo kwamba ni lini tutawasaidia wale wanavijiji wanaokaa karibu na maeneo yanayozalishwa umeme, kupata umeme badala ya kuwaacha kuwa watazamaji wa mwanga wa umeme kwa muda mrefu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kuhusu matatizo yanayoikabili *TANESCO*. Ni kweli kwamba Shirika letu la *TANESCO* lina kabiliwa na matatizo makubwa ya uendeshaji. Waheshimiwa Wabunge watapenda kufahamu kwamba hadi sasa *TANESCO* inakusanya kwa mwezi shilingi bilioni 35, lakini matumizi yake ni shilingi bilioni 47 kwa mwezi. Matumizi haya yanatokana zaidi na ukweli kwamba gharama za uendeshaji peke yake na utawala zinatumika bilioni 29.5, gharama za kulipia mitambo ya *IPTL* inatumia bilioni 3.6, gharama ya kulipia mitango ya *SONGAS* ni bilioni karibu 5.4 na gharama zinazoitwa *energy charges*, gharama zinazotumika kununulia mafuta ni vipuli, ni bilioni 8.4. Kwa maana hiyo, tatizo kubwa linaloikabili *TANESCO* ni kwamba matumizi yake ni makubwa zaidi kuliko pato la shilingi bilioni 35. Serikali inajaribu kuangalia uwezekano wa kujaribu kupunguza gharama hizo kwa kuangalia Shirika kama la *IPTL* kujaribu kugeuza au kuikarabati mitambo yake itumie gesi zaidi kuliko mafuta ambayo yanasababisha malipo makubwa ya ruzuku kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la *SONGAS*: Ni kweli ahadi zimekuwa zimetolea mara nyingi na ni kweli Kijiji cha Songa kwa sababu ya ukosefu wa transfoma ya *TANESCO* ya kwenda Kijijini. Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imeiagiza *TANESCO* ifanye kila linalowezekana kufanya mambo mawili. La kwanza; Kuhakikisha kwamba ahadi zilizotolewa huko nyuma, zinatekelezwa kwa kutumia fedha za Mradi wa Maendeleo ya Umeme Vijijini. Mradi huu usiibue miradi mipya, utekeleze kwanza ahadi zilizowekwa na Serikali kwa wananchi au kuziba viporo vilivyobaki. Huo ndio msimamo wa Serikali na ni agizo kwa *TANESCO*. Lakini la pili; Naomba nimhakimishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kesi ya *SONGAs* tutafanya kila linalowezekana ili swali hili lisiulizwe tena Bungeni maana tutatoa agizo kwamba

transfoma ipelekwe Songa ili kutekeleza kilio walichomtolea wananchi Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Na. 149

**MGODI WA NYANG'HWALE – MSALALA**

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE** aliuliza:-

Kwa kuwa Mgodi wa Nyang'hwale jimboni Msalala ni pamoja na migodi mikongwe sana ya almasi lakini umetelekezwa kwa muda mrefu sana:

(a) Je, mgodi huo kwa sasa una hazina kiasi gani cha madini?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia vifaa wachimbaji wadogo wadogo wanaofanya kazi katika mgodi huo ili waendeleze uchimbaji?

(c) Je Serikali ina utaratibu gani mahsusi wa biashara ya madini kwa wachimbaji wadogo wadogo ambao wamekuwa wakilanguliwa madini yao kutokana na kutojua mahali lilipo soko la almasi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ezekiel M. Maige, Mbunge wa Msalala, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa utafiti na tathmini iliyofanywa na Kampuni ya *Williamson Diamonds Limited* kati ya mwaka 1959 na 1976, mgodi wa Nyang'hwale ulikadiriwa kuwa na mashapo ya tani 1,699,000 za miamba yenye almasi ambazo kati ya hizo Kampuni hiyo ilichimba tani 1,233,460. Hivyo hadi hapo ukadiriaji mwingine utakapofanyika, mgodi wa Nyang'hwale una tani 465,540 za miamba yenye almasi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Serikali wa kuwapatia vifaa wachimbaji wadogo wadogo wa madini ni kama ifuatavyo:-

- Serikali imehamasisha makampuni mbali mbali kama vile *SIDO*, *Mintek* ya *South Africa* kuleta vifaa vya wachimbaji wadogo wadogo hapa nchini.

- Pili, Chuo Kikuu cha Dar es salaam kupitia *Institute of Production Innovation* kinafanya utafiti wa vifaa mbali mbali vikiwemo vya uchimbaji mdogo wa madini kwa lengo la kutengeneza vifaa hivyo hapa nchini na kwa bei nafuu.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inafanya juhudi kubwa zinazolenga kuwanufaisha wachimbaji wadogo wadogo kupata soko la kuuza madini yao karibu na maeneo yao ya uchimbaji madini. Miongoni mwa hatua hizo ni utoaji wa leseni kubwa za

biashara ya madini *(Dealers Licence)* zaidi ya kumi Mjini Shinyanga kwa ajili ya ununuzi wa madini ya vito.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali imetoa leseni ndogo za biashara ya madini 35 kwa ajili ya kuwawezesha wachimbaji wadogo wadogo katika Kanda ya Kati Magharibi likiwemo eneo la Nyang'hwale, kuuza madini yao kwenye sehemu zilizo karibu na machimbo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa wito kwa wachimbaji wadogo wadogo kujenga tabia ya kuuza madini yao kwa watu wenye leseni za biashara ya madini. Pia Waheshimiwa Wabunge wawahamasishe wananchi wa maeneo yao kuuza madini yao kwa watu wenye leseni za bishara ya madini na si vinginevyo.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Kwanza, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema madini ya almasi yaliyobaki kwenye mgodi huu ni kidogo sana. Kwa mujibu wa taarifa ambazo zimekuwepo tokea Kampuni ya *Williamson Diamonds* iliposimamisha uchimbaji miaka zaidi ya 30 iliyopita, ni kwamba madini yalitobaki pale ni kidogo sana kiasi kwamba hayawezi yakakidhi uchimbaji mkubwa. Na kwa kuwa kumekuwepo matatizo makubwa kati ya wananchi na watu ambao wana vitalu vikubwa ambao ni wachimbaji wakubwa, katika umiliki wa eneo hilo.

Je, Serikali inaweza sasa ikalitangaza eneo hili la Nyang'hwale kuwa ni la wachimbaji wadogo wadogo tu ili wachimbaji wadogo wadogo wa Kata za Mlunga, Ngogwa na Busangi waweze kunufaika kwa sababu madini yaliyoko hayawezi yakahimili uchimbaji mkubwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili: Kwa kuwa kumekuwepo na migongano ya mara kwa mara kati ya wachimbaji wakubwa na wadogo sababu inayotokana na wachimbaji wakubwa kumiliki au kuhodhi maeneo makubwa ya vitalu.

Lakini hawajaviendeleza kwa zaidi ya miaka sita sasa, na matokeo yake yamekuwa ni wananchi wadogo wadogo wamekuwa wakichimba kwenye maeneo yao kwa kibali kutoka kwa hao wenye migodi au wenye vitalu ili wawauzie kwa bei wanayoitaka wao.

Je, Serijkali inatoa tamko gani kuhusu wachimbaji hao wakubwa ambao hawajafanya uwekezaji wowote?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba majibu yawe mafupi kabisa!

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ni kweli kwamba matatizo yapo kati ya wachimbaji wadogo wadogo pamoja na wachimbaji wakubwa wakubwa.

Serikali inakusudia kutuma timu ya uchunguzi ya Wizara ili kwenda kuangalia maeneo gani ambayo yanaweza kutengwa kwa ajili ya wananchi na yakatangazwa kwa mujibu wa Sheria inayomruhusu Waziri wa kutangaza maeneo hayo kuwa ya wachimbaji wadogo wadogo.

Kuhusu migogoro iliyopo kati ya wchimbaji wakubwa na wadogo, pia napenda kurudia kwamba Serikali itatuma tume yake ya uchunguzi kuangalia matatizo yanayozikabili Kampuni mbili kubwa za uchimbaji wa madini hayo pamoja na wachimbaji wadogo ili kutoa baadaye suluhisho la kudumu la kuwezesha kusuluhisha migogoro hii na kuwapa kipaumbele wachimbaji wadogo wadogo.

Na. 150

**Ufugaji wa Kisasa**

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Nne iliahidi kutilia mkazo ufugaji wa kisasa wenye tija kwa mfugaji kwa kuhakikisha kuwepo kwa maendeleo ya malisho, majosho pamoja na mabwawa ya kutosha na ya uhakika kwa mifugo na kuepuka umbali mrefu anaokwenda mfugaji kutafuta malisho kunakosababisha mifugo (ng'ombe) kutopata afya nzuri na mfugaji pia:-

(a) Je, Serikali imeandaa mipango ipi ya mpito katika kutekeleza kauli ya Mheshimiwa Rais aliyotoa kwa wananchi alipokuwa akiomba kura?

(b) Je, ni lini uchimbaji wa mabwawa ya maji ya mifugo yatakamilika katika vijiji vya Msansao, Ujungu kwa Mwanamajiku, Msombi, Madalawa, Mayanzani na Haila ili kuiokoa mifugo ya wapiga kura wa maeneo hayo ambao tayari wameipokea kauli ya Mheshimiwa Rais kwa mikono miwili.

(c) Je, ni taratibu zipi zimeandaliwa na Serikali juu ya kuwekeza kwenye ng'ombe wa kisasa ili kujipatia maziwa mengi, utaratibu ambao utawaondolea adha wapiga kura kwenye Jimbo langu kwa kuwa na mifugo wengi ili kupata maziwa mengi badala yake wawe na ng'ombe wachache lakini wapate amaziwa mengi na kwamba Serikali italeta lini mpango maalum wa kopa ng'ombe lipa ng'ombe katika Jimbo la Iramba Magharibi ili wananchi wapate fursa hiyo, kwani wapo tayari kwa Mpango huo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mbunge wa Iramba Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais kwa wananchi kuhusu ufugaji wa kisasa, Wizara yangu katika mwaka wa 2006/2007 imepanga kutekeleza yafuatayo:-

- Kuhamasisha uzalishaji wa malisho na kutoa mafunzo kuhusu matumizi bora ya maeneo ya malisho. Ili kukabiliana na mahitaji makubwa ya mbegu bora za malisho, Wizara yangu itaanzisha mashamba mapya ya mbegu huko Kizota, Kongwa, Buhuri, Mabuki, *Sao Hill* na Tengeru Mivumoni. Lengo ni kuzalisha tani 25 za mbegu.

- Kuchangia ujenzi wa mabwawa makubwa mawili katika Wilaya za Kishapu na Mwanga na malambo 20 katika Wilaya ya Lindi, Longido, Nachingwea, Handeni, Shinyanga Vijijini, Chunya, Misungwi, Kongwa, Bariadi, Mvomero, Manyoni, Urambo na Maswa.

- Kutoa ruzuku ya shilingi bilioni mbili kwa ajili ya dawa za kuogeshea mifugo na kukarabati majosho 84, mawili yakiwa katika Wilaya ya Iramba.

- Kuwapatia wafugaji 20,000 mafunzo ya ufugaji bora na kuanzisha mashamba darasa 20.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchimbaji wa mabwawa ya maji kwa ajili ya mifugo katika vijiji vya Msansao, Ujungu kwa Mwanamajiku, Msombi, Madaralawa, Mayanzani na Haila katika Wilaya ya Iramba, Wizara inashauri Halmashauri ya Wilaya ya Iramba kuingiza mpango huo katika katika mipango yao ya *DADPS* chini ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(ASDP)* ambapo Serikali inatuma fedha moja kwa moja Wilayani ili kutekeleza mipango kama hiyo.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, ili wananchi wengi waweze kuingia kwenye ufugaji wa ng'ombe wa maziwa, Wizara yangu inatoa elimu ya ugani kwa wafugaji ili waelewe vyema kanuni za ufugaji bora.

Baada ya kuandaliwa wafugaji hushauriwa kununua ng'ombe hao kutoka mashamba ya Serikali na yale ya binafsi, ama kutumia njia ya uhamilishaji.

Wizara itaendelea kuimarisha mashamba ya kuzalisha mitamba ya Mabuki, *Sao Hill* na Kitulo, Ngerengere na Nangaramo ili kutekeleza azma hiyo.

Aidha, ili wafugaji wa Jimbo la Iramba waweze kunufaika na mpango wa Kopa Ng'ombe Lipa Ng'ombe ambao unaendeshwa na Shirika Binafsi la *Heifer Project Tanzania (HPT)*, nashauri uongozi wa Wilaya ya Iramba uwasiliane na Shirika hilo ili kuanzisha mpango huo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Killimbah, swali la nyongeza naomba liwe fupi kabisa.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali dogo la nyongeza kama ulivyo nitaka niulize. Kwa kuwa maeneo niliyoyataja na ameyarudia Mheshimiwa Naibu Waziri, maeneo haya yana ng'ombe wengi sana, lakini tatizo kubwa linalosumbua maeneo hayo hasa wafugaji ni vifo vinavyosababishwa na wadudu kama ndorobo, mbung'o na kadhalika. Sasa kutokana na hali hiyo hakuna kituo chochote cha Mifugo ambacho kinafanya matibabu kwa ajili ya mifugo hii.

Sasa, Wizara ipo tayari kuanzisha kituo cha mifugo katika maeneo hayo ili wanafugaji wa maeneo hayo waweze kupeleka ng'ombe wao na kufanya tiba wanapaopata matatizo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nataka majibu mafupi!

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Singida uko katika kanda moja na Mkoa wa Dodoma ambapo kituo cha kuzuia magonjwa kilichopo Mpwapwa kinatoa huduma hizo. Namwomba Mheshimiwa Mbunge, awasiliane na Wizara, ili kusudi tuweze kuona ni namna gani tunaweza tukamsaidia ili kukakabiliana na tatizo la magonjwa. (*Makofi*)

Na. 151

**Mashamba ya Kilimo na Mifugo**

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA** aliuliza:-

Kwa kuwa mashirika mengi hapa nchini yamebinafsishwa na kwa kuwa mashamba makubwa ya kilimo na mifugo *(cattle ranches)* yamekufa kutokana na Serikali kushindwa kuyaendesha:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufufua mashamba haya ili yaweze kutoa ajira kwa vijana wengi wanaohitimu masomo katika vyuo mbalimbali hapa nchini pamoja na vijana wa vijijini waliokosa nafasi ya kuendelea na masomo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mbunge wa Viti Maalum, naomba nitoe maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mashirika ya umma yakiwemo ya mifugo katika miaka ya 1998 yaliingizwa kwenye Kamati ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma, ili yale yanayojiendesha kwa hasara yabinafsishwe na kuendeshwa na sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sera ya kubinafsisha mashamba na makampuni yaliyokuwa yanaendeshwa na Serikali inatoka na na kuanzishwa kwa mfumo wa uchumi wa soko ambapo Serikali imeiachia sekta binafsi kutekeleza shughuli za uzalishaji kama vile kuendesha mashamba ya ng'ombe wa nyama na viwanda vya kusindika nyama. Aidha, sekta binafsi ndiyo inayoshughulika na shughuli za uzalishaji, usindikaji na usambazaji wa mazao ya mifugo.

Serikali imebakia na jukumu la kuaandaa sera, kusimamia sheria na kuratibu maendeleo ya sekta ndogo ya nyama.

Katika zoezi la ubinafsishaji, Ranchi za Taifa pamoja na mashamba ya kuzalisha mifugo hayakupata wanunuzi mapema hadi pale ilipobainika kuwa mtindo huu ulikuwa hautoi fursa kwa wananchi wengi kuingia kwenye ufugaji wa ng'ombe wa maziwa na nyama. Hivyo mwaka 2002, Serikali ilibadilisha uamuzi wake wa kubinafsisha haya mashamba kupitia *PSRC*, baada yake Waraka wa Baraza la Mawaziri namba 2 wa mwaka 2002 ulitoa maelekezo mapya juu ya mustakabali wa mashamba pamoja na Ranchi za Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango huo baadhi ya maeneo ya Ranchi zilizo chini ya Kampuni ya Ranchi za Taifa (*NARCO*) ziligawanya katika vipande vya hekta 2,500 hadi 4,000 ambapo jumla ya vipande 124 vilipatikana na vyote vimemilikishwa kwa Watanzania.

Aidha, mashamba matano ya kuzalisha ng'ombe wa maziwa (*LMU's*) ya Mabuki, Sao Hill, Nangaramo, Ngerengere na Kitulo yamebakizwa chini ya Serikali kwa ajili ya kuendelea kuzalisha mitamba wa ng'ombe wa maziwa na kuwa maeneo maalumu kwa ajili ya kutunza vizazi vya mifugo bora nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ranchi ndogo ndogo 124 zilizokamilishwa kwa Watanzania, zinatarajiwa kuzalisha ng'ombe bora wa nyama takraban 100,000 kwa mwaka. Aidha, mpango huu ulilenga kuzifanya Ranchi hizi ndogo kuwa chanzo cha upatikanaji wa ng'ombe wa nyama walionenepeshwa na hatimaye kuchinjwa kwa ajili ya soko la ndani na la nje.

Ranchi za mfano zenye hekta 20,000 kila moja katika maeneo yaliyogawanywa pamoja na ranchi za Ruvu na Kongwa, zimeandaliwa mpango wa kibiashara ambao utasaidia kuziimarisha na kuzijengea uwezo wa kuzalisha mifugo bora ili iwe mfano kwa ranchi zingine na pia nazo kuwa chanzo cha upatikanaji wa ng'ombe walionenepeshwa kwa ajili ya kuchinjwa katika machinjio na viwanda vya nyama vilivyopo na vitakavyojengwa.

Baada ya maelezo haya naomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Sakaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, endapo mpango wa kuyawezesha mashamba ya Serikali na ranchi zilizo chini ya *NARCO* pamoja na ranchi ndogo ndogo

zilizomilikishwa kwa wananchi utaendeshwa na kuendelezwa kulingana na matarajio ya mpango, ajira kwa Watanzania wengi wakiwemo wataalamu wanaohitimu katika vyuo na wale wanaokosa nafasi ya kuendelea na masomo ya juu itapatikana. Mashamba na ranchi hizo zitaendeleza ufugaji wa mifugo bora wa kisasa unaozingatia tija na wa kibiashara, hivyo kutoa wigo mpana wa ajira kwa watalaamu wa mifupo na wengine watakaohusika na biashara nzima ya mifugo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umezidi na maswali yamekwisha. Matangazo ya mikutano kwanza. Katibu wa Chama cha Wanawake Wabunge, *TWPG* anawatangazia wanachama wa Wabunge Wanawake wote saa saba mchana kutakuwa na mkutano katika Ukumbi wa zamani wa Bunge, ukumbi wa Pius Msekwa. Wabunge Wanawake wa Bunge wote wanaomba wahudhurie. Halafu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ardhi, Mheshimiwa Gideon Cheyo, anawatangazia Wajumbe wa Kamati yake saa saba Mchana wakutane katika chumba na. 432 ghorofa ya nne Jengo la Utawala. Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, Mheshimiwa Mohammed Missanga, anawatangazia Wajumbe wa Kamati, yake wakutane leo saa tano asubuhi katika ukumbi Namba 133, ghorofa ya kwanza.

Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali, Mheshimiwa John Cheyo pia anaomba niwatangazie wajumbe wako wakutane leo saa saba mchana chumba 231. Halafu Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Mheshimiwa Anna Abdallah, anawatangazia Wajumbe wa Kamati yake wakutane saa sita mchana leo chumba 219 ghorofa ya pili. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Jenista Mhagama anawatangazia Wajumbe wa Kamati yake, Kamati ya Maendeleo ya Jamii, wakutane saa tano leo katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Mgana Msindai, anawatangazia wajumbe wake wakutane saa saba chumba Na. 133. Sasa wengine mtakuwa mnagongana huko huko kwa sababu mtajua mkifika huko maana yake naona mikutano mingi. Pia Mwenyekiti wa *TAPAC* naye anatangaza Wajumbe wa *TAPAC* wakutane saa saba katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Naona sasa kuna watu watatu hapa wakutana huko huko.

Sasa noamba nitambulishe wageni waliopo. Kwanza kabisa kwenye *Speakers Gallery* yupo mke wa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Juma Akukweti na watoto wake mnakaribishwa. (*Makofi*)

Halafu Mheshimiwa James Lembeli ana wageni wake kuna Mzee Edward Msoma, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Kahama, kuna Bou na Ventula Katibu Kata CCM, Kata ya Chambo.

Pia nina wageni wa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Mahiza, nafikiri mgeni ni wa sisi wote Mwenyekiti wa Baraza la Michezo na Skauti Mkuu, Mheshimiwa Kanali Idd Kipingu na yupo Msaidizi wa Mambo ya Nje katika Chama cha Skauti Bwana Majesa mnakaribishwa. (*Makofi*)

Pia nina wageni wa Mheshimiwa Herbert Mntangi, kuna Viongozi wa Dini na Mashehe saba (7) wa Wilaya ya Muheza. Naomba wote wasimame. Nina wageni wa Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji, mgeni wake ni Mwenyekiti wa Umoja wa Watu wenye Ulemavu wa Tawi la Jambiani Kikadini Zanzibar, naomba asimame. Ahsante karibuni sana wageni wetu kwenye Bunge letu hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, ana mgeni wake Katibu wa Idara ya Utawala na Fedha ya Umoja wa Vijana Taifa, Ndugu Francis Isaac, naomba asimame. Halafu Mheshimiwa Margreth Mkanga anatoa taarifa kuwa ana mgeni wake ni Mwalimu Mama Changu kutoka Morogoro.

Halafu nina wageni wa Mheshiminwa Spika wa Bunge letu. Hawa ni wanachuo 40 na walimu wawili wa Chuo cha Mipango, Mkoani Dodoma, naomba wasimame. (*Makofi*)

Halafu pia nina wageni tena wa Mheshimiwa Spika wa Bunge letu. Hawa ni viongozi wa Serikali ya Wanachuo wa Chuo cha Utalii cha Mjini Dar es Salaam, naomba pia wasimame. Sasa wote mnakaribishwa na siyo lazima kuomba ruhusa watu wanakaribishwa kusikiliza Shughuli za Bunge. *(Makofi)*

## KAULI ZA MAWAZIRI

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, leo tokea asubuhi yalikuwa maswali ya Wizara yangu kuhusu ngono sasa hivi najibu hoja kuhusu ngono sijui kuna nini leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mbunge wa Viti Maalum Mwanza kwa kuleta mbele ya Bunge lako tukufu, maelezo binafsi yanayohusu karata zenye picha za wanawake walio uchi ama nusu uchi zinazouzwa nchini. Katika maelezo yake hayo aliyoyatoa kwa mujibu wa kanuni ya 40 ukisoma pamoja na fasili ya 9 Kanuni ya 21 ya Kanuni ya Bunge, toleo la mwaka 2004 Mheshimiwa Nyawazwa, alisema katika ziara yake kutembelea Wilaya nane za Mkoa wa Mwanza, amefanya kuanzia tarehe 24 Agosti mwaka huu hadi tarehe 24 Septemba, alielezwa na baadhi ya wananchi kuwa kuna karata zenye picha hizo zinazouzwa kiholela madukani. Katika ziara hiyo.

Pia Mheshimiwa Mbunge, amesema alipokea malalamiko kutoka kwa wananchi mbalimbali, kuwa karata zenye picha hizo zilikuwa zinauzwa kiholela madukani na kwamba hata vijana wadogo wamekuwa wakizinunua na kuzicheza na kwamba kutokana na picha hizo zilizopo kwenye karata hizo maadili ya vijana wengi yamekuwa yakimomonyoka kwa kiasi kikubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kujulishwa na wananchi kuhusu suala hilo, Mheshimiwa Nyawazwa, amesema alifanya utafiti binafsi kuthibitisha kuwa ni kweli karata hizo zilizagaa madukani. Ili kupata ushahidi wa maelezo yake alinunua baadhi ya

karata hizo na kuja nazo hapa Bungeni kama vielelezo na mimi pia niliziona. Mheshimiwa Mbunge, alisisitiza kwamba picha zilizomo kwenye karata hizo zinawadhalilisha wanawake kwa ujumla na hususan wanawake wa Kitanzania ambao hawana tabia ya kukaa uchi na kuvaa vichupi tu hadharani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa muhstari huo wa maelezo binafsi wa Mheshimiwa Nyawazwa, sasa napenda kujibu maelezo yake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sheria ya makosa jinai sura ya 16 *Penal Code cap* 16 ya kifungu 175 (1) inakataza kwa mtu yeyote kutengeneza, kuchapisha, kuhifadhi au kumiliki maandishi, michoro, picha, picha za senema, mabango, nembo ama machapisho yoyote ya ngono au kuonyesha uchafu wa kuathiri utu wa binadamu kwa lengo la kufanya biashara, kusafirisha nje ya nchi kusambaza au kuonyesha kwa umma. Kifungu hiki pia kinakataza kwa mtu yeyote kushiriki au kutangaza hadharani masuala ya aina hii. Adhabu inaweza kutolewa kwa mtu atakayepatikana na hatia mahakamani kwa kosa hili ni kifungo cha miaka miwili au faini ya shilingi 200,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako tukufu na wananchi wote kwa ujumla kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, siku zote imekuwa mstari wa mbele katika kupiga vita mambo au vitu vinavyoathiri maadili na utu wa binadamu. Wizara yangu kwa ushirikiano mzuri wa Wizara ya Usalama wa Raia na vyombo vingine vya dola kwa nyakati tofauti vimekuwa vikiendesha operesheni maalum kwa kamati ya watu wanaochapisha na kuuza vijarida vya mambo ya ngono nchi nzima. Operesheni hiyo ambayo ni ya kudumu imeonyesha mafanikio ya kuridhisha kwani wahusika waliokamatwa wamefikishwa mahakamani. Kwa mfano, hivi karibuni watu 8 walikamatwa jijini Dar es Salaam kwa makosa hayo ya vijarida vya ngono na kufikishwa mahakamani na kesi zao zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika hoja ya Mheshimiwa Mbunge, alisema kwamba picha zilizopo kwenye karata hizo pia zimekuwa kichecheo na kishawishi kikubwa kwa vijana wengi waliozinunua na kuzicheza na hatimaye kufanya vitendo vya ngono ambavyo siyo salama ambavyo matokeo yake ni kupata UKIMWI. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba Serikali, haioni uhusiano wa moja kwa moja kwa karata hizo kusababisha vijana kufanya ngono zembe na kupata ukimwi. Hata hivyo Serikali kama ambavyo imebainisha katika sera yetu ya Afya vijana hawana budi kujikinga na balaa hilo la ugonjwa wa UKIMWI na kuachana kabisa na ngono zembe.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusisitiza kwamba mbele ya Bunge lako tukufu kwamba Serikali inaendelea kutekeleza wajibu wake wa kulinda na kuwajenga maadili mema vijana wetu ambao ndiyo nguzo ya taifa letu la baadaye. Pia Serikali na vyombo vyake hairuhusu na wala haitaruhusu vitu kama karata zilizotajwa ambazo haziwadhalilishi wanawake peke yao bali hata sisi wanaume pia kwa sababu wanawake wetu wote ni mama zetu, wake zetu, dada zetu, bibi zetu, shangazi zetu na hata binti zetu. Kwa hiyo, jamii nzima lazima iheshimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii, kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wote, kwa ujumla kwamba operesheni hii inayoendelea hivi sasa ya kupiga vita machapisho ya picha za ngono yanayoathiri maadili ya Taifa ni yetu sote.

Kwa hiyo, mwananchi yeyote mwenye taarifa zozote kuhusu uchafu huo achukue jukumu la kupeleka taarifa hizo kwenye kituo chochote cha polisi, Viongozi wa Serikali za Mitaa, au kwa vyombo vingine vya dola, ili hatua madhubuti zichukuliwe. Vita dhidi ya udhalilishaji wa wa binadamu ni vyote sote, siyo la Wizara yangu peke yake. Tushikiriane kukemea kwa nguvu zete zote maovu haya katika jamii yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha kwamba maadili ya utamaduni wa Kitanzania hayamomonyoki Serikali imeunda vyombo kadhaa vikiwemo vifuatavyo:-

1. Bodi ya Filamu Tanzania, ambayo kazi yake kubwa ni kukagua na kuhakiki filamu zinazotengenezwa hapa nchini na zinazoingizwa kutoka nje.

2. Kamati ya Maudhui *(Content Committee)* ambayo kazi yake kubwa ni kuhakiki maudhui ya vipindi vya Radio na Television vya Tanzania.

3. Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA) ambalo kazi yake kubwa ni kusimamia shughuli zote za sanaa na utamaduni kwa lengo la kuwaenzi, kuendeleza na kuimarisha shughuli hizo.

4. Idara ya Habari Maelezo, ambayo moja ya majukumu yake ni kufuatilia utekelezaji wa Sheria ya Magazeti na machapisho ya mwaka 1976 kwa lengo la kudhibiti matumizi mabaya ya machapisho hayo kama kuchapisha picha za ngono, lugha chafu na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, maelezo hayo naamini yatatosheleza kujibu hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Mbunge Esther Nyawazwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Tunashukuru kwa taarifa tunaendelea.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

**Muswada wa Sheria ya Kufanya Marekebisho katika Sheria Mbalimbali za Serikali za Mitaa kwa Mwaka 2006 (*The Local Government laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2006.***

*(Kusomwa mara ya Pili)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mabadiliko yaliyotokea na yanayoendelea kutokea hapa nchini, Serikali inawasilisha katika Bunge lako tukufu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Serikali za Mitaa, ili kuzifanyia marekebisho Sheria za Serikali za Mitaa, kukidhi haja ya mabadiliko ambayo yameathiri Mfumo wa Serikali za Mitaa. Muswada huu umezingatia Maoni ya Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, Wabia wa Maendeleo *(Development Partners)* na wadau mbalimbali.

Kutokana na maoni yao tumelazimika kuandaa Jedwali la marekebisho *(Schedule of Amendments)* ili kuufanyia marekebisho Muswada wa awali uliosomwa kwa mara ya kwanza katika Bunge hili mwezi Agosti 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na maoni ya wadau mbalimbali waliotajwa hapo juu tumelazimika kuaandaa jedwali la marekebisho *(Schedule of Amendments)* ambalo limegawanywa kwa Waheshimiwa Wabunge, ili lisomwe pamoja na Muswada wa awali. Jedwali hili linafanya marekebisho yafuatayo:-

(a) Kufuta vifungu vya namba 4, 5, 7, 19, 31, 32, na 36 na maeneo yafuatayo yanahusika:-

(i) Kwanza ni uanzishaji wa Ofisi ya Afisa Tarafa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na kazi zake.

(ii) Ni uanzishaji wa Kamati za Maendeleo za Tarafa na kazi zake.

(iii) Uanzishaji wa Kamati za Ulinzi na Usalama za Tarafa na kazi zake.

(iv) Ni Uanzishaji wa Mkutano wa Mashauriano wa Mkoa *(Regional Consultative Assembly*) na kazi zake na mwisho.

(v) Ni uanzishaji kisheria wa *clusters* katika Sekretarieti za Mikoa.

Maeneo hayo yote niliyoyataja yameondolewa katika Muswada huu kwa kuzingatia maelekezo ya Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, pamoja na maoni ya wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Jumuiya ya Serikali za Mitaa (*ALART)*.

(b) Kuweka upya (*renumbering*) kama ifuatavyo, baada ya marekebisho yale basi tumelazimika vile vile kufanya *renumbering* kwa hiyo, kifungu cha 6 kitasomeka kama 4, 8 itakuwa 5, na kuongeza kifungu kipya cha 6.

Pili, ni kuvitaja upya vifungu namba 9,10,11,12,13,14,15,16, 17 na 18 kuwa namba 7,8,9,10,11,12,13,14,15 na 16 kwa mpangilio huo.

Tatu, ni kifungu cha 20 sasa kitakuwa Namba 17.

Nne, ni kuweka kifungu kipya cha 18; na

Tano, kuvitaja upya vifungu vya namba 21, mpaka 29 na 30. Sasa hivyo vifungu vitakuwa ni 18,19,20,21,22,23, 24,25,26,27 na 28. Mwisho ni kuvitaja upya vifungu 33,34,35 na 36 ambavyo sasa vitakuwa ni 29,30,31 na 32.

(c)Kufanya marekebisho katika vifungu vilivyorekebishwa *as numbered* ambavyo ni namba 5 sasa 9, 13, 14,16, 17,18,19,21,27,30 na 31 hivyo sasa ndiyo vifungu ambavo tutavizingatia katika kufanya marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutumia fursa hii kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati yako ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa George Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa na wadau mbalimbali kwa michango yao mikubwa na mizuri sana iliyosaidia sana kuboresha Muswada ambao sasa tunauwasilisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya jedwali la marekebisho ambalo niliona ni vizuri nikaliweka wazi ili kuwarahisishieni kuweza kufuatilia mjadala naomba sasa kueleza madhumuni ya Muswada huu ambao umegawanyika katika sehemu tano zenye jumla ya vifungu 31. Muswada huu unakusudia kufanya marekebisho katika sheria mbalimbali za Serikali za Mitaa na umegawanya katika sehemu tano.

Sehemu ya kwanza, ya Muswada inahusu masharti ya utangulizi ambayo mtayaona yako dhahiri.

Sehemu ya pili, ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika sheria ya Serikali za Mitaa yaani Mamlaka za Wilaya ambayo ni sura 287 na wengi wenu mmeizoea tu kwa sheria namba 7 ya mwaka 82. Marekebisho hayo yanakusudia kuwezesha Halmashauri iliyopo kuendelea kuwa na mamlaka katika eneo iliyobakishiwa baada ya kuundwa Halmashauri mpya. Marekebisho haya pia yanakusudia kuwafanya Wabunge wa Kuteuliwa na Rais chini ya Ibara ya 66 (1) (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wajumbe, wasiozidi watatu wanaoteuliwa na Waziri kuwa Wajumbe wa Halmashauri za Wilaya wanazoishi.

Utaratibu wa kuwapata Madiwani hao utaanzia katika vyama vya siasa vyenye Madiwani katika Halmashauri husika. Vile vile marekebisho haya yanapendekeza kuweka muda ambao Mwenyekiti wa Halmashauri wa Wilaya na Makamu, watakaa madarakani pale kutakapokuwa na uwiano unaolingana wa Madiwani, kama ilivyo hivi sasa kwa Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji. Sheria hii pia inafanyiwa marekebisho kueleza bayana kazi na majukumu ya Afisa Mtendaji wa Kata, ambayo hapo awali hayakuwa bayana. Vile vile sheria inatamka wazi kazi na majukumu ya Wizara za Kisekta kuhusiana na Serikali za Mitaa.

Sehemu ya Tatu ya Muswada, inapendekeza kufanya marekebisho katika sheria ya Serikali za Mitaa mamlaka za Miji sura 288 ambayo wengi mnaijua vile vile kwa

sheria namba 8 ya mwaka 1982. Marekebisho haya yanakusudia kuongeza tafsiri ya baadhi ya maneno yaliyotumika katika kifungu cha tatu. Pia marekebisho hayo yanakusudia kuwafanya Wabunge walioteuliwa na Rais, chini ya ibara ya 66 (1) (e) Wabunge wa Viti Maalum vya wanawake na Madiwani wasiozidi 3 watakaoteuliwa na Waziri kuwa wajumbe sasa wa Halmashauri za Miji, Manispaa, Majiji isipokuwa Jiji la Dar es Salaam.

Sheria hii pia inafanyiwa marekebisho ili kuzitaka Halmashauri kutoa taarifa kwa Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya, kuhusu utekelezaji wa shughuli za maendeleo za Serikali za Mitaa ndani ya Mikoa au Wilaya zao. Sheria pia inaanzisha rasmi Ofisi za Mtendaji wa Mtaa na kueleza kazi na majukumu ya Afisa Mtendaji wa Kata. Hayo hayakuwepo hapo awali.Sehemu ya nne, ya Muswada huu inakusudia kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 12 cha sheria hii. Marekebisho haya yanakusudia kuweka utaratibu wa kufanyika kwa uchaguzi wa Madiwani pale Halmashauri inapogawanywa baada ya uchaguzi. Aidha, marekebisho haya yanaondoa kuwepo kwa uchaguzi endapo mgawanyo huo wa Halmashauri haujaathiri mipaka ya Majimbo ya Uchaguzi wa Wabunge.

Sehemu ya tano, ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Tawala za Mikoa, sura ya 97. Mapendekezo haya yanampa Mkuu wa Mkoa, wajibu wa kisheria wa kuzisaidia na kuziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa, kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Vile vile marekebisho haya yanawajumuisha Wabunge wa Viti Maalum na wa kuteuliwa na Rais kuwa Wajumbe wa Kamati ya Mashauriano ya Mkoa *(Regional Consultative Council)* kwa hivi sasa si Wajumbe.

Muswada huu pia unaanzisha Kamati ya Mashauriano ya Wilaya, ambayo itakuwa chini ya Uenyekiti wa Mkuu wa Wilaya na Katibu wake atakuwa ni Mkurugenzi wa Halmashauri. Kazi za Kamati hii ni za ushauri na mashauriano zaidi kama ilivyoonyeshwa katika kifungu cha 30 cha jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niwasilishe maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa mujibu wa Kanuni ya 70(2), Kanuni za Bunge, Toleo la 2004 baada ya kukamilisha kazi ya kuchambua Muswada wa marekebisho ya Sheria mbalimbali za Serikali za Mitaa yaani *The Local Government Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2006.*

Kamati yangu ilipokea maelezo ya Serikali iliyowasilishwa mbele ya Kamati na Mheshimiwa Mizengo Pinda, Mbunge, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala

za Mikoa na Serikali za Mitaa kabla ya kuanza kwa mkutano huu wa Bunge. Kwa mujibu wa maelezo ya Serikali na kama alivyoeleza mtoa hoja kwa muhtasari Muswada huu unalenga kutoa ufumbuzi wa masuala kadhaa ambayo yamejitokeza katika mamlaka ya Halmashauri zetu kama vile kukosekana kwa changamoto katika Mabaraza ya Kata, Muungano wa kisheria unaojitokeza pale Halmashauri mpya inapoanzishwa. Nafasi ya Wabunge wa Viti Maalum na wale wa kuteuliwa katika Mabaraza ya Kata pamoja na nafasi ya uwajibikaji wa Makatibu Tarafa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuuchambua Muswada huu, Kamati ilipata nafasi ya kuwasikiliza wadau mbalimbali waliofika mbele ya Kamati. Wadau hao walitoka Kituo cha Sheria ya Haki za Binadamu, *Legal and Human Rights Centre, National Organization for Legal Assistance, (NOLA)* na *Policy Forum.* Wadau hawa waliotoa mchango mkubwa sana kwa Kamati. Napenda niipongeze Ofisi yako kwa kuruhusu kuwa na utaratibu wa namna hii. Kwani una manufaa sana katika kuchangia uboreshwaji wa Miswada ya Serikali na masuala mengine muhimu ya kuwashirikisha wananchi kwa karibu zaidi katika mchakato nzima wa kutunga Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unafanyiwa marekebisho sheria nne. Sheria ya kwanza, ni Sheria ya Serikali za Mitaa, Mamlaka ya Wilaya ya 1982 yaani *The District Authorities Act, 1982,* Sheria ya pili ni Sheria ya Serikali za Mitaa, Mamlaka ya Miji, 1982, *Local Government Urban Authorities Act, 1982* Sheria ya tatu, ni Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, 1979 yaani *Local Authorities Elections Act, 1979* na Sheria ya nne ni Sheria ya Tawala za Mikoa, 1977 *Regional Administration Act, 1977.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi Kamati yangu inakubaliana na mapendekezo ya Serikali katika Sheria zinazofanyiwa marekebisho. Hata hivyo Kamati ina mapendekezo katika baadhi ya maeneo ili kuuboresha Muswada huu. Mapendekezo hayo yamegawanyika katika maeneo mawili. Mapendekezo ya jumla na ya kifungu kwa kifungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ibara ya tano ya Muswada inahalalisha kuwepo kwa nafasi ya Katibu Tarafa. Kama inavyofahamika Makatibu hao wapo na wanafanya kazi lakini nafasi na majukumu yao bado hayajatambulika kisheria. Aidha Kamati katika eneo hili Muswada huu unapendekeza kuwa Makatibu Tarafa wawajibike kwa mamlaka ya uteuzi kwa upande wa kazi zile zinazohusu Serikali Kuu na pia wawajibike kwa Halmashauri kwa majukumu kwa majukumu yanayohusishwa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaona kuwa kutenganisha mamlaka ya uteuzi na uwajibikaji au kuweka utaratibu wa uwajibikaji kwa mamlaka mbili tofauti ni kusababisha matatizo ya kiutendaji na hivyo kuathiri ufanisi. Hivyo Kamati inashauri kuwa ama Katibu Tarafa aendelee kuwa Serikali Kuu au ahamishiwe Serikali za Mitaa na aitwe Afisa Mtendaji wa Tarafa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ibara ya 5 pia inaanzisha Kamati ya Maendeleo ya Tarafa, kwa mujibu wa marekebisho haya Kamati hizi zinagharamiwa na Halmashari na zitaendesha vikao vyake kila baada ya miezi mitatu. Kamati ilijadili kwa kina kipengele

hiki. Mathlani iwapo ni busara kuanzisha Kamati hizi na kama zikianzishwa haitakuwa kurudia kuanzisha kitu ambacho kipo yaani *duplication.* Aidha, Kamati inaona kuwa Kamati hizi zitakuwa mzigo kwa Serikali na kwa walipa kodi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo lililojitokeza na ambalo Kamati inaona halijakaa vizuri ni mamlaka ya Kamati hizi mpya na zile za zamani, Kamati ya Maendeleo ya Kirafa, Kamati ya Maendeleo ya Kata. Muda wa vikao pia hauonyeshi mwelekeo wa kuboresha utaratibu uliokuwepo. Kwani Kamati za Maendeleo Kata zinakutana mara nne kwa mwaka na hizi zinaainishwa pia zitakutana mara moja kila baada ya miezi mitatu. Kamati inaona kuwa Kamati hizi zitakuwa ni mwendelezo na ucheleweshaji wa utekelezaji ya maamuzi ya wananchi na kuna uwezekano wa watendaji kubadilisha maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati za Maendeleo ya Kata, huongozwa na Madiwani wa Kata, Kata husika kama ambavyo inapendekezwa kwa Kamati hizi mpya. Kamati inatambua pia kuwa zipo Halmashauri nyingi nchini ambazo zinapata tabu za kuendesha Kamati hizi na jambo linalokwamisha hata kufanyika kwa vikao kwa muda muafaka. Sasa tunaongeza tena Kamati nyingine badala ya kuboresha zile zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada pia unaorodhesha Wajumbe wa Kamati za Maendeleo ya Tarafa katika sehemu ya 29(e) kifungu cha kwanza. Kamati imebaini kuwa idadi kubwa ya Wajumbe ni kutoka katika upande wa Serikali badala ya uwakilishi wa wananchi. Muswada hauonyeshi iwapo wajumbe hawa ni wajumbe kwa wadhifa wao, yaani *Ex-Official* au hapana. Hii ni kwa kuwa Tarafa zina wastani wa Madiwani watano na wataalam kati ya 30 hadi 40. Ikumbukwe kuwa Madiwani wako kuwakilisha maoni na mawazo ya wananchi. Kwa kuwa maamuzi hufanywa kwa makubaliano ya walio wengi kuna uwezekano mkubwa wa sauti za Madiwani kuzidiwa nguvu jambo linaloweza kuondoa maana halisi ya uwakilishi wa madaraka kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa baada ya majadiliano na Kamati, Serikali imeamua kufuta ibara hiyo ya tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ibara ya sita ya Muswada inahalalisha kuwepo kwa Ofisi ya Mtendaji wa Kata. Hawa pia walikuwepo ila sasa wanapewa nguvu ya kisheria. Kamati haina tatizo na jambo hili. Kifungu hiki pia kinaonyesha kuwa Afisa Mtendaji wa Kata atawajibika kwa Katibu Tarafa na atashughulikia pamoja na mambo mengine ya utekelezaji ya mipango ya maendeleo katika Kata na kuandaa mipango ya utekelezaji yaani *action plans* kwa majukumu yake yote na kuwasilisha kwa Katibu Tarafa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu inaona kuwa maendeleo ya Kata kwa kiasi kikubwa yanachangiwa na utendaji wa hawa watendaji wa Kata. Hivi ni vema wawezeshwe hasa kitaalam ili kuharakisha maendeleo. Aidha wawajibike zaidi iwapo watapewa mamlaka kamili ya kuwajibika kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ibara ya 8 ya Muswada inawaingiza rasmi Wabunge wa Kuteuliwa kuwa Wajumbe wa Halmashauri za Wilaya kwa maeneo wanayoishi. Aidha, Waziri mwenye dhamana ya Serikali ya Mitaa anapewa mamlaka ya kuteuwa Madiwani wasiyozidi watatu wawe wajumbe wa Halmashauri.

Kuhusu utaratibu utakaotumika kuwapata madiwani hao, Kamati yangu imeelezwa kuwa Waziri atafanya mawasiliano na vyama vya siasa vyenye uwakilishi katika Halmashauri husika. Vyama hivyo ndivyo vitapeleka majina waliyopendekezwa. Kisha Waziri atafanya uteuzi wake kutoka miongoni mwa majina hayo aliyopelekewa. Kamati yangu imefafanuliwa kuwa lengo la kifungu hiki ni kupanua wigo wa majadiliano katika vikao vya Halmashauri na kwamba haitatumika pale ambapo idadi ya wajumbe wa Halmashauri kwa chama tawala na upinzani itakuwa sawasawa.

Kamati inashauri kwamba Serikali iweke wazi vigezo vya uteuzi huu ili kuondoa malalamiko na uwezekano wa sheria kutumika vibaya. Mapendekezo hayo yalikubaliwa ambapo Serikali ilileta mabadiliko na mapendekezo ya awali yalikuwa madiwani hao watateuliwa kutokana miongoni mwa makundi ya walemavu, waathirika wa virusi vya UKIMWI, wafugaji na watu wenye taaluma mbalimbali. Kamati hairidhii na mapendekezo ya Waziri kutumia makundi yaliyoorodheshwa hapo juu kuwa ndiyo kigezo cha kuteua madiwani. Kamati inashauri Sheria ianishe vigezo ambavyo Waziri atatumia kuteua Madiwani badala ya kutumia makundi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ibara ya 9 inaanzisha utaratibu mpya wa kufuatwa pale inapotokea kuwa idadi ya Halmashauri kwa kila chama inalingana na kusababisha ugumu wa kutoa maamuzi wakati wa kupiga kura, kwamba hali hii inapotokea Halmashauri yaweza kupitisha azimio au kufupisha muda wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti kukaa madarakani tofauti na muda ule unaojulikana kisheria. Yaani Mwenyekiti miaka mitano na Makamu Mwenyekiti, mwaka mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi Kamati inaafiki wazo hili. Kwani itasaidia kuepusha mivutano inayoweza kuchelewesha maendeleo. Hata hivyo, Kamati inaona kuwa jambo hili linaweza kufanikiwa pale ambapo Halmashauri inaundwa na Wajumbe kutoka vyama viwili. Kwani hapa ni rahisi kwa Wajumbe hao kukubaliana muda wa kila chama kutoa Mwenyekiti na Makamu wake.Tatizo ni pale ambapo Halmashauri inahusisha vyama vinne au zaidi kwani uwezekano wa kufikia makubaliano kuongoza Halmashauri unaweza kuwa mgumu. Hivyo badala ya kutatua tatizo sheria itakuwa imezua tatizo lingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Kamati inaona kuwa matumizi ya maneno *may by the resolution determine* yanaleta utata badala ya Halmashauri kuachiwa kufanya maamuzi haya mazito. Ni vema Sheria itamke wazi kuwa inapotokea idadi ya Wajumbe kuwiana basi kila chama kitaongoza Halmashauri kwa kipindi cha miaka miwili na nusu. Kwa hiyo, katika kushughulikia tatizo linaloweza kujitokeza pia Halmashauri inapokuwa zaidi ya vyama viwili bila kuwepo chama kinachopata kura za kutosha kuongoza Halmashauri, Kamati inapendekeza kuwa Sheria iruhusu muungano wa vyama ambavyo utawekewa masharti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu hiki pia kinatambulisha suala jipya linalohusiana na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Halmashauri. Kuwepo na madaraka yanayolingana na ya Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri. Kamati haina pingamizi na pendekezo hili hasa kwa utaratibu huu unafuatwa pale tu ambapo idadi ya Wajumbe wa Halmashauri kichama inalingana. Vinginevyo, utaratibu wa kawaida wa Wenyeviti hawa wa Kamati kuchaguliwa kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ibara ya 11 utaratibu unawekwa kwa Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya kuwasilisha kwa Mkuu wa Mkoa husika taarifa za utekelezaji wa shughuli za maendeleo kila baada ya miezi minne. Hii ni pamoja na taarifa nyingine zozote ambazo Mkuu wa Mkoa atazihitaji. Kamati yangu inaona kuwa hili ni jambo jema. Hata hivyo nashauri kuwepo na utaratibu wa wazi utakaounganisha mamlaka ya Mkuu wa Mkoa kwa Halmashauri husika. Kwani kuwasilisha taarifa za utekelezaji pekee haitoshi. Kwa maana nyingine nafasi ya Mkuu wa Mkoa na Wilaya katika Halmashauri zao ziwekwe wazi kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inafahamu kwamba katika Sheria ya Tawala za Mikoa ya mwaka 1977 yaani *The Administration Act, 1977,* Mkuu wa Mkoa anatajwa kuwa ana wajibu wa kuwezesha Halmashauri kutekeleza majukumu yao. Lakini kwa Sheria hii jambo hili haliko wazi. Hivyo kwa kuwa Muswada huu unahusisha rasmi Mkuu wa Mkoa na Halmashauri ni vema basi nafasi yake ikawekwa zaidi ya majukumu yote ya msingi. Zaidi ya kupokea taarifa yabainishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ibara ya 12 ya Muswada unapendekeza kuwepo kwa nyongeza, ufafanuzi wa wajibu wa Sekta mbalimbali za Kiserikali Kuu, katika kufanikisha majukumu ya Serikali za Mitaa. Baada ya kupitia ufafanuzi huo Kamati imeona kuwa hakuna jambo jipya lililoongezwa ambalo halimo katika Sheria iliyorekebishwa. Mathalan ufafanuzi uliotolewa katika kifungu cha 174(a) hadi (f) cha Sheria imejitosheleza na unaeleweka vema zaidi ya hii nyongeza mpya. Kwa mfano Kamati inaona maneno kama *provide and secure anabling environment* kuwa yanaweza kuleta utata katika tafsiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unalenga kuweka utaratibu ambao utawezesha Wizara za Kisekta kushiriki katika kuziwezesha Serikali za Mitaa kusimamia maeneo yanayohusiana na Sekta husika kwa ukaribu na ufanisi zaidi.

Kamati inakubali kwamba kwa sasa Wizara nyingi zina uhusiano hafifu sana na Serikali za Mitaa. Baadhi ya Wizara vimekwenda mbali zaidi hadi kujaribu kubuni njia ya kutekeleza majukumu yake Mkoani na Wilayani bila kupitia mfumo uliopo wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Utaratibu huu ukiruhusiwa uendelee una hatari ya kudhoofisha mfumo mzima wa Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mantiki hiyo, Kamati inapendekeza Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ijiimarishe ili iwe na uwezo

mkubwa wa kuratibu na kushauriana na Wizara zinazohusika juu ya njia bora za kushirikiana na Serikali za Mitaa na kutekeleza majukumu ya Wizara hizo Mikoani. Nafurahi tena kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Kamati imehakikishiwa kuwa suala hili linafanyiwa kazi ili kuboresha mfumo mzima uliopo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili hili Kamati inapendekeza kuwa Wizara zinatakiwa ziweke utaratibu utakaowezesha kuzipatia Serikali za Mitaa watumishi wenye sifa zitakiwazo. Kuweka utaratibu wa kuwaendeleza na kuwapanga pamoja na kuzitafutia Serikali za Mitaa fedha na rasilimali nyingine zinazohitaji kutekeleza programu zilizopendekezwa au zilizobuniwa na Wizara. Masuala ya kitaalam yasimamiwe na Wizara, lakini masuala ya utawala na nidhamu ya watumishi yasimamiwe kwa utaratibu uliopo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuimarisha mawasiliano kati ya Wizara na Mikoa na ili kuwa kiungo kati ya Wizara hizo na Serikali za Mitaa na kuwezesha Serikali za Mitaa kupata maelezo ya kitaalam na ya Kisera kutoka Mikoani.

Kamati inapendekeza kwamba viongozi wa Kisekta katika Mikoa ambao sasa wanaitwa Washauri warudie kutambulika kama Wakuu wa Idara za Sekta zao. Kwa maana hiyo mfumo wa *clusters* kwa kuwa unadhoofisha huduma za kitaalam. Kwani unawaondoa wataalam kutoka kwenye shughuli zinazohusiana na taaluma zao na kuwatumia katika shughuli za utawala. Umerefusha mlolongo wa mawasiliano na unawafanya viongozi wa kisekta wasiweze kujitokeza kama Wakuu wa Sekta zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ibara ya 13 ya Muswada inapendekeza kutokamatwa kwa mali za Halmashauri kwa ajili ya kulipia fidia kutokana na kesi ambazo Halmashauri inashindwa badala yake Mkurugenzi ahakikishe kuwa fidia hiyo inalipwa kutoka katika mapato ya Halmashauri husika. Kamati inatambua kuwa raia ana haki ya msingi ya kupata huduma kutoka katika Halmashauri kama vile maji, elimu, magari ya kuzoa taka, zimamoto, afya na kadhalika.

Lakini pia raia ana haki ya kuishitaki Halmashauri iwapo imemkosea au kuvunja mkataba naye. Halmashauri nayo ina wajibu wa kutimiza masharti ya kisheria pamoja na kutekeleza hukumu zilizotolewa dhidi yake. Hivyo Mahakama yaweza kutoa amri ya kukamatwa kwa mali za Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa Mahakama yaweza kutoa amri ya kukamatwa kwa mali za Halmashauri kama vile majengo, magari ya zimamoto, kuzoa taka, kukamata akaunti za Halmashauri, kama vile Elimu mishahara na kadhalika kwa ajili ya kumlipa raia anayeidai Halmashauri.

Kamati inashauri kuwa ibara hii inahitaji marekebisho. Kwa kuwa kukamatwa mali ni hatua ya mwisho, baada ya mdaiwa kushindwa kulipa deni, basi sheria itoe utaratibu wa kuwabana Wakurugenzi kutekeleza amri za Mahakama katika kipindi kilichotajwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria nyingine inayofanyiwa marekebisho ni sheria ya Serikali za Mitaa, Mamlaka ya Miji, 1982, ibara ya 34 inaanzisha Kamati ya Ushauri wa Wilaya yaani *DCC.*, ambayo itaongozwa na Mkuu wa Wilaya.

Kulingana na marekebisho yaliyofanywa katika ibara hii ya Muswada miongoni mwa majukumu ya Kamati hizi ni kushughulikia suala zima la hali ya kisiasa na vyama vya siasa katika eneo husika. Ufafanuzi ulitolewa na Waziri kuwa nia ya mapendekezo haya ni kuwezesha vyama hivyo kuwa na sehemu ya kusemea na kujadili kwa pamoja na masuala yaliyojitokeza pamoja na kutatua migongano baina yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kamati haina tatizo na pendekezo hili isipokuwa sheria iweke wazi kuwa Wakuu hao wa Wilaya hawatakuwa na mamlaka ya kufuta vyama vya kisiasa.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tano ya sheria hii kama ilivyorekebishwa mwaka 1999 inafafanua majukumu ya Halmashauri za Miji, *Urban Authorities* ikiwemo miji, manuspaa na majiji. Aidha kifungu cha 69(a) cha Sheria hiyo kinazungumzia majukumu ya majiji bila kuyahusisha na yale ya Mamlaka ya Miji kama yalivyofafanuliwa chini ya sehemu ya 5.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatambua kwamba kuna matatizo ya kuhusiana na ushirikiano kati ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na Manispaa ya Kinondoni, Ilala na Temeke. Matatizo haya yanatokana na ukweli kwamba eneo lote limegawiwa Manispaa hizo tatu. Na haiko wazi Mamlaka iliyobaki kwa Halmashauri ya Jiji ni yapi.

Hivyo, kusababisha kuwepo hoja ya kuwekwa kwa utaratibu wa kisheria unaofafanua uhusiano wa Halmashauri ya Jiji na Manispaa na miongoni mwa Manispaa zenyewe na jinsi majukumu ya uhusiano huo utakavyotekelezwa. Kukosekana kwa mambo haya husabisha uwepo uhusiano wa hisani na kuathiri utekelezaji wa majukumu yanayohitaji uratibu na ushirikiano wa eneo lote la jiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapendekeza kwamba uwekwe uhusiano rasmi wa kisheria ambao utawataka watendaji wakuu wa mamlaka hizo kukutana mara kwa mara na kuandaa masuala yatakayowasilishwa kwenye Baraza la Madiwani la Jiji na ambayo yatazingatia maslahi ya wakazi wa jiji kwa sasa Watendaji hao sio wajumbe wa Baraza la Jiji na wala hawahudhurii vikao vya Baraza labda kwa mwaliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafsi hii. Aidha nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Mizengo Pinda, (Mbunge). Mheshimiwa Celina Kombani, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Luka Siyame, kwa ushirikiano waliotoa kwa Kamati yangu na kufanikisha kukamilisha kwa kazi hii.

Napenda pia niwashukuru na kuwapongeza kwa dhati kabisa Wajumbe wa Kamati, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa michango yao ya kina iliyowezesha kuuboresha Muswada huu na naomba niwatambue kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa George M. Lubeleje – Mwenyekiti. Mheshimiwa Tatu M. Ntimizi, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mheshimiwa Athumani S. Janguo, Mheshimiwa Rajab A. Juma, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Fatma M. Maghimbi, Mheshimiwa Ramadhan A. Maneno, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Nimrod E. Mkono, Mheshimiwa Salim Yussuf Mohamed, Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu na Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa. *(Makofi)*

Pia napenda kuwapongeza Makatibu wa Kamati hii Ndugu Emmanuel Mpanda, Nenelwa Mwihambi, Ernest Zulu na Charles Mloka, kwa kuihudumia vema Kamati na kutayarisha maoni katika hatua iliyofikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO – (k.n.y. MSEMAJI MKUU WA UPINZANI – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema ya kuniwezesha kusimama hapa hivi leo, aidha ninakushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii, kwa mujibu wa Kanuni ya Bunge Toleo la 2004, kifungu cha 43(5)(c) na kusomwa kwa pamoja na kifungu cha 70(2) kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya sheria mbali mbali za Serikali za mitaa *(LOCAL GOVERNMENT LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) ACT,2006).*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza Waheshimiwa Mizengo Pinda Waziri, Celina Kombani Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na wataalam wao wote wenye dhamana ya kuendesha Wizara hii ambayo ndilo chimbuko la demokrasia na kutoa uongozi bora katika nchi hii. Japokuwa kuna marekebisho ambayo yamefanyika lakini bado maudhui ya Muswada huu baada ya marekebisho hayatofautiani na kabla ya kufanyiwa marekebisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 34 (15)(b) baada ya kufanyiwa marekebisho na kuongezwa kwa kifungu kipya cha (g). Kimsingi kifungu hiki Kambi ya Upinzani hatukubaliani nacho kwa dhana kuwa ni Halmashauri tu ndiyo yenye madaraka ya kushughulikia masuala yote yanayohusiana na madaraka ya umma ambapo na vyama vya siasa vinahusika.

Lakini kama dhana ni kuwa na *forum* kama Mheshimiwa Waziri alivyotanabahisha kwenye Kamati ya Sheria na katiba. Kama Mkurugenzi atafanya kazi za kuandaa *Forum* ya vyama vya siasa kwenye ngazi za Wilaya ili kutekeleza kile ambacho Mheshimiwa Rais alichokishauri hadi kuundwa kwa Wizara inayoshughulikia na mambo ya siasa. Na katika mchakato huo marekebisho kwenye Sheria ya vyama vya

siasa *(POLITICAL PARTIES ACT)* yakafanyika kwa kuongeza kifungu cha *code of conduct* zitakazotengenezwa na Waziri kwa kushirikiana na Vyama vya siasa. Kongamano libaki kwenye *code of conduct* zitakazokuwa zimependekezwa katika ngazi ya wilaya na si vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya Muswada kufanyiwa mabadiliko tulipingana na kipengele cha ofisi ya Katibu Tarafa pamoja na majukumu yake kuwajibika katika mamlaka mbili tofauti, aidha kulingana na majukumu aliyokuwa nayo ni dhahiri kuwa aliingilia moja kwa moja majukumu ya wale waliochanguliwa ki-demokrasia kwa ajili ya kuwa viongozi wa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ambayo yamefanywa katika kifungu cha 35 kwa kuongeza kifungu cha 17A kama jedwali la marekebisho linavyoonyesha (*schedule of amendment)* kwenye sheria ya *Regional Administration Act* inaonyesha kuwa ofisi ya katibu tarafa na majukumu ambayo kimsingi tulikuwa hatukubaliani nayo itakuwa chini ya ofisi ya Mkuu wa Mkoa na kuwa kama kiunganishi baina ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, na sio kama alivyokuwa anawajibika moja kwa moja kwa Mkurugenzi na Serikali Kuu. Na hivi sasa uhamisho huo unaleta utata na mkanganyiko baina ya mamlaka za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, dhana nzima ambayo inafanya uwepo wa Katibu tarafa na majukumu anayopewa na muswada huu, sio tu yanaongeza ukiritimba bali pia yanaongeza udhibiti wa demokrasia katika ngazi za Serikali za Mitaa. Kwani ukiangalia kazi zake zilizoainishwa katika kifungu kipya cha 17A, kinaonyesha kuwa majukumu ya maafisa watendaji wa Kata, Vijiji na Mitaa, anayachukua yeye.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi hayo madaraka anayopewa Katibu Tarafa akiwa chini ya serikali kuu inapingana na sura ya nane (madaraka ya umma) ibara ya 146(1) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kinachotamka madhumuni ya kuwepo Serikali za mitaa na kupeleka madaraka kwa wananchi. Madaraka ya Umma/madaraka kwa wananchi ni uhuru wa kupanga na kuamua kulingana na mahitaji yao. Serikali kuu inatakiwa ihusishwe kulingana na matakwa ya wahusika ambao ni wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na kifungu cha 8 cha Muswada ambacho kinafanyiwa marekebisho Kifungu cha 35 kifungu kidogo cha (i) cha sheria. Licha ya marekebisho ya kifungu (f) cha Muswada na baadaye marekebisho mengine kama Jedwali la marekebisho *(Schedule of Amendement)* inavyosomeka. Kuwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa atawateua kuwa madiwani watu kutoka katika makundi yaliyotajwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla Kambi ya Upinzani inapingana na dhana hiyo, kwa misingi kuwa dhana hiyo inaua msingi mkuu wa demokrasia kwa wananchi kuchagua viongozi/wawakilishi watakao kuwa wanawaongoza. *(Makofi)*

Kifungu hiki hakitoi nafasi kwa Mheshimiwa Waziri kufanya uteuzi huo kwa kuzingatia matakwa ya wananchi wa maeneo husika au kwa kushauriana na vyama vya siasa katika maeneo husika, bali kinatoa nafasi kwa Waziri kutunga kanuni na mwongozo utakaotumika katika uteuzi huo. Na kifungu hicho hakitoi mwanya wowote kuwa ni lazima Waziri ashauriane na vyama vya siasa au kundi lolote lile.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli kwamba katika ngazi ya Kata ukishaanza kugawa uwakilishi kama jedwali la marekebisho linavyoeleza ni kuleta matabaka/ ubaguzi katika jamii, kwani sifa zinategemea matakwa ya Waziri na siyo kama yameainishwa katika Muswada huu wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwonekano huu ni dhahiri kuwa nia na lengo la kifungu hiki kuweka wateule wa Waziri katika chombo muhimu cha maamuzi katika ngazi hii ya uimarishaji wa demokrasia ni kuinyanganya jamii uwezo wa kuweza kutumia demokrasia kupitisha maamuzi bila kuwepo kwa shinikizo lolote toka ngazi yeyote ya kiutawala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inafikiri kama kweli kifungu hicho kina nia njema ya kuweka uwakilishi wa makundi yaliyotajwa katika jedwali la marekebisho. Inashuri makundi tajwa yafanye uteuzi kulingana na sheria zinazoyawezesha makundi hayo kutambulika, na watakaochaguliwa kidemokrasia wapate baraka za Waziri. Hapo dhana nzima ya uwakilishi wa makundi tajwa itakuwa na maana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 17 cha Muswada kinafanyia marekebisho kifungu cha 14A sheria kwa kuongeza kifungu kidogo cha (3) kinachoanzisha ofisi ya mtendaji wa mtaa (mtaa *Executive Office)* na Afisa Mtendaji wa Mtaa *(Mtaa Executive Officer)* ambaye atachaguliwa na mamlaka ya Mji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria hii haionyeshi majukumu ya afisa mtendaji wa mtaa pia haisemi nafasi ya wenyeviti wa serikali ya mtaa ni ipi kwani katika kila mtaa wananchi wameshiriki kuweka uongozi wao kwa ajili ya kusimamia shughuli zao na maendeleo ya wananchi katika mitaa. Majukumu ya mwenyekiti wa Serikali ya mtaa yamefafanuliwa katika waraka wa Waziri wa TAMISEMI, majukumu yale yale yanaonekana kukabidhiwa afisa mtendaji wa mtaa.

Je, Serikali inatangaza ukomo wa wenyeviti wa serikali za mitaa? Maofisa watendaji wa mitaa wameanza kazi toka Julai 2006, muswada wa kuwatambua umeletwa Bungeni Oktoba 2006 wamekuwa wakifanya kazi chini ya mamlaka gani ikiwa Bunge halijapitisha sheria ya kuwepo kwao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inakuwa na wasiwasi kuwa huu unaweza kuwa ndio mwanzo wa kifo cha demokrasia pale kifungu cha 17 (4) kinachosema kuwa afisa mtendaji wa mtaa atafanya kazi zake kulingana kama barua yake ya kuajiriwa inavyosema au pale atakapopata maelekezo kutoka Serikalini.

Kwa nini kama kweli kina nia njema majukumu yale yasiainishwe wazi katika sheria na pale atakapokiuka majukumu hayo wananchi waweze kuhoji? Tunasisitiza na kupinga tena kwa kuanzishwa kwa ofisi hii kwani kunawanyima haki na madaraka viongozi (wenyeviti wa Serikali za mitaa) ambao wamechaguliwa na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 9 cha Muswada kinachofanyiwa marekebisho kifungu cha 39 cha sheria. Kifungu cha 9(5) kinachoendana kwa pamoja na vifungu cha (3) na (4). Chini ya mfumo wa vyama vingi vya siasa.

Kwa vyama vingi vya Siasa, hali kama hii ndiyo inatokea katika Halmashauri ya Kigoma Ujijiji, kati ya CHADEMA na CCM. Kambi ya Upinzani inaona itakuwa ni jambo la Msingi pindi hali kama hiyo inapojitokeza basi, kuwepo na muungano wa vyama katika kuendesha Halmashauri au Manispaa. Utaratibu wa kuongoza utafikiwa kwa kuzingatia vigezo ambavyo vitakubaliwa na pande zote husika. Tunashauri hili kutokana na ukweli kuwa mvutano wa madaraka baina ya pande husika, ni kuendelea kuwanyima wnanchi haki yao ya msingi ya kupata maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inashauri, ili kuimarisha Demokrasia katika ngazi ya Halmashauri, muundo wa Demokrasia ya Kibunge utumike, ili muungano wa vyama utumike katika shughuli za kiutendaji, kama kweli Serikali ina dhamira ya kweli ya kutoa mamlaka ya demokrasia katika ngazi za Halmashauri na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia uwajibikaji, na matumizi mazuri ya fedha za wananchi. Kambi ya upinzani inashauri kuwa Kamati ya Fedha za Halmashauri, Uenyekiti wa Kamati hiyo uwe chini ya Diwani toka kambi tofauti na ile inayoendesha Halmashauri au Manispaa. Hii italeta nidhamu kwa matumizi ya fedha za walipa kodi. Kwani hutokea matukio ambayo fedha za wananchi zimeingizwa katika shughuli ambazo hazihusiani kabisa na matakwa ya malengo ya Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 20 cha Muswada kinachofanyiwa marekebisho, Kifungu cha 19 cha sheria ya *Local Governmemnt (Urban Authorities) Act, 1982* kwa kuongeza kifungu kidogo cha (e) kinachohusu Wabunge wa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Madiwani katika vikao vya Halmashauri. Kambi ya Upinzani inapingana na kifungu hiki, kwani hakuna kifungu kinacho weka angalizo kuwa kabla Waziri mwenye dhamana hajatoa mwongozo kwa Mbunge mteule kuingia katika Halmashauri ni bora kwanza ashauriane na viongozi wa vyama vya siasa, ambao wanachangia katika kuendesha halmashauri husika. Vinginevyo kifungu hiki kinatoa mwanya wa maamuzi kuelekea upande mmoja pale panapokuwa na ulinganifu. Aidha kwa kuweka wabunge wateule, maana yake ni kuwanyang'anya wananchi haki yao ya kidemokrasia kupitia kwa wawakilishi wao katika kutoa maamuzi. Kambi ya Upinzani inaliona hili kuwa njia nyingine ya kukandamiza demokasia katika vyombo vya maamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema haya, nawasilisha na pia, napenda kusema kuwa. Sisi Kambi ya Upinzani, hatuungi mkono Muswada huu. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru asubuhi hii ya leo kunipa nafasi ya kwanza na mimi niweze kuwa mchangiaji katika Muswada huu uliopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kumpongeza sana Waziri, Naibu Waziri katika Ofisi yake na Wataalam, kwa kupendekeza kuleta Muswada huu wa kurekebisha Sheria mbali mbali za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mimi napenda nitamke tangu mwanzo kwamba ninaunga mkono mapendekezo ambayo yanaletwa hapa, pamoja na mabadiliko makubwa ambayo Waziri ameyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niombe radhi ya kwamba hotuba yangu niliyoiandaa ilikuwa inalenga ule Muswada wa awali ambao umefanyiwa marekebisho makubwa sana. Kwa hiyo, mtiririko wa maelezo yangu, ama hotuba yangu itakuwa imeathirika kwa kiasi fulani. Lakini hata hivyo, nitatumia tu vile vifungu ambavyo vimependekezwa na marekebisho ya Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Muswada huu, Serikali imependekeza kurekebisha Sheria Nne muhimu. Ya kwanza ni Sheria ya Serikali za Mitaa, Mamlaka ya Wilaya Sura ya 287. Ya pili, ni Sheria ya Serikali za Mitaa, Mamlaka ya Miji Sura ya 288. Sheria ya Tatu ambayo inapendekezwa kurekebishwa ni Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Sura ya 292 na Sheria ya Nne, ambayo inapendekezwa kurekebishwa ni Sheria ya Tawala za Mikoa Sura 97.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nianze kuchangia Muswada huu. Kwanza kwa kutoa pongezi. Ninaanza na pongezi, katika Kifungu cha 11 kama ilivyorekebishwa na 22 kama ilivyorekebishwa. Serikali inapendekeza kuongeza Vifungu 2 katika Sheria mbili tofauti. Serikali inapendekeza kuongeza Kifungu kipya cha 194(A) katika Sheria ya Serikali za Mitaa, Mamlaka ya Wilaya na katika Kifungu cha 22 inapendekeza kuongeza Kifungu kipya cha 109(B) katika Sheria ya Serikali za Mitaa, Mamlaka ya Miji.

Napenda niipongeze Serikali kwa kuleta maependekezo haya. Mapendekezo haya yanalenga katika kuzuia mali za Halmashauri kuporwa na wajanja wachache. Katika hali ya sasa hivi, kuna watu binafsi huwa wanajitokeza kwenda Mahakamani na kudai kulipwa fidia kwa shughuli ambayo wamefanya ama kwa kazi ambayo wamefanya na matokeo yake mara nyingi Mahakama zinatoa amri ya kukamata mali za Halmashauri. Kwa mapendekezo hayo, naamini kabisa Serikali inataka kulinda mali za wananchi.

Ninapenda nikubaliane na mapendekezo ya Serikali kwamba, badala ya mdai na kukamata mali za Halmashauri kama magari, nyumba, kufunga akaunti na kadhalika, kama ilivyopendekezwa katika sheria hii. Mimi ninafikiri ndiyo mwafaka kwamba

Mkurugenzi Mtendaji wa kila Halmashauri awajibike kulipa madai ama amri ya Mahakama kama itakavyotolewa badala ya Halmashauri kukamatiwa mali zake.

Kwa hiyo, ninapenda niipongeze Serikali na Waziri kwa kuleta pendekezo hili. Hii itadhibiti uporaji wa mali za Halmashauri bila utaratibu. *(Makofi)*

Pamoja na maependekezo haya mazuri, lakini ninaushauri kidogo tu kwamba, Halmashauri za Wilaya, Miji na kadhalika ni Taasisi zenye kumiliki mali nyingi sana. Lakini katika utendaji wake kuna mapungufu kidogo. Halmashauri nyingi hazina Wanasheria.

Sasa mimi napendekeza kwamba ili Halmashauri hizo ziweze kusimamiwa vizuri kisheria, Wizara ama Serikali kwa ujumla ingelielekeza kila Halmashauri iweze kuajiri Wanasheria wenye taaluma ya kuweza kusimamia mali za Halmashauri. Pamoja na kipengele hiki, naamini kabisa kwamba Wanasheria wakiajiriwa katika kila Halmashauri watasimamia ili Halmashauri zetu ziweze kuendeshwa kwa misingi ya kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niipongeze Serikali kwa kuleta mabadiliko katika Kifungu cha 30, kama kilivyorekebishwa na Waziri. Katika Kifungu cha 30 inapendekezwa Serikali kuongeza Kifungu cha 15(A) katika Sheria ya Tawala za Mikoa ya mwaka 1977 na hapa inapendekezwa kuundwa kwa Kamati ya Mashauriano katika ngazi ya Wilaya. Mimi naamini kwamba, Kamati hii, kama inaweza kuitishwa mara kwa mara, kama ilivyopendekezwa kwenye Muswada huu, itasaidia sana kusukuma maendeleo katika ngazi ya Wilaya.

Hivi sasa katika ngazi ya Wilaya, zaidi ya Baraza la Madiwnai hakuna chombo ama Kamati ambako inaweza kujumuisha wadau mbali mbali waweze kuchangia mawazo yao katika uendeshaji wa Wilaya. Lakini ninaona kuna dosari kidogo, ama kuna mapungufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukipendekeza, Kamati ikae kikao mara mbili, bila kupendekeza Bajeti kwa ajili ya vikao hivyo, bila shaka hicho kikao ama Kamati hiyo haitawahi kukaa hata siku moja. Kwa hiyo, mimi napendekeza katika mapendekezo haya ambayo ni mazuri sana ya kuunda Kamati ya Mashauriano ya Wilaya, pia Sheria itamke wazi kwamba bajeti, kwa ajili ya vikao hivi vya mashauriano inatoka ofisi ipi. Natambua kwamba Mwenyekiti atakuwa ni Mkuu wa Wilaya, lakini Sheria haijatamka kwamba huyu Mkuu wa Wilaya atawezeshwa namna gani kuweza kuitisha vikao hivi. Kwa hiyo, ninaomba, kama si katika sheria hii, basi katika Kanuni naomba itamke wazi kwamba bajeti kwa ajili ya kuendesha vikao hivi itatoka katika kifungu gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye kifungu cha 5(e) na Kifungu cha 17(e) kama ilivyorekebishwa ambayo inahusu Wabunge wa kuteuliwa na Rais. Mimi ninakubalina kabisa na mapendekezo ya Muswada kwamba hawa Wabunge wanaoteuliwa na Rais, waingie katika vikao vya Halmashauri husika, kwa zile Halmashauri ambako wanatoka. Lakini kinachonikwaza ni kipengele kimoja tu. Chini kunaelezwa kwamba, endapo hawa Wabunge wa Kuteuliwa na Rais, watazidi zaidi ya

waatatu, wakiwa zaidi ya watatu, wale watakaozidi, Waziri, sijui kama amefanya marekebisho katika eneo hili. Waziri atakuwa na mamlaka ya kutangaza kwenye gazeti za Serikali kwamba hawa waliozidi wahamishiwe katika Halmashauri ya jirani, hivyo ndivyo sheria ama Muswada unavyopendekeza.

Mimi sikuona sababu, ama tunalenga kutatua nini. Sioni sababu kama mimi nimeteuliwa na Rais kuwa Mbunge na niko katika Wilaya ya Kondoa, kama tuko wawili ama zaidi ya watu tumeteuliwa katika wilaya hiyo wanne sioni sababu niweze kwenda Babati ili niwe mjumbe wa Halmashauri hiyo, sioni mantiki, kwamba tunataka kutatua nini pale. Kwangu mimi inaonekana kama vile tunawapeleka hawa Wabunge kama Maluki katika hizo Wilaya ambako wanakwenda. Kwani hawataeleweka wanamuwakilisha nani. Kwanza hawatakuwa na *interest* hata ya kuweza kuzungumzia masuala ya maendeleo kwa sababu siko wanako ishi. Kwa hiyo mimi ninapendekeza kwamba kama nimesoma kwa haraka haraka Jedwali la Mabadiliko yaliyotolewa lakini sikuwe kuli-*note* hili kama limefutwa sintakubaliana nalo. Lakini kama halijafutwa mimi ninapendekeza hilo eneo liangaliwe upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye Kifungu cha 17(f), kama kilivyorekebishwa. Uteuzi wa Madiwani watatu (3) na Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa. Ukweli wenyewe ni kwamba hata mimi sikuelewa kwa nini pendekezo hili limeletwa, sielewi kabisa. Tunategemea, ama mategemeo yetu ni kwamba tunategemea Madiwani wa kuchaguliwa na wananchi waweze kuwawalikilisha wananchi hao hao, sasa hawa wanaoteuliwa na Waziri mimi sielewi malengo yake ni nini. Sikuelewa kabisa. *(Makofi)*

Kwa nini nimeshindwa kuelewa. Mimi katika Jimbo langu tumeshaurina sana na Wapiga kura, walichoniambia ni kwamba wao wangelipendelea Kata ambazo ni kubwa sana katika Jimbo la Kondoa Kusini, zigawanywe ili uwakilishi uongezeke badala ya kuwa na Madiwani wateule wa Waziri. Kwa hiyo, walipendekeza kwamba Kata zifuatazo, zingeliweza kupewa nafasi hiyo. Kata ya Mrijo ambayo ni kubwa sana. Goima, Chandama, Jangalo, Ovada na Lalta, zingeweza kutoa uwakilishi mzuri zaidi kuliko hawa Madiwani wanaoteuliwa na Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kugusia machache katika vifungu ambavyo vimependekezwa na Serikali katika mabadiliko ya Sheria nilizotaja, basi nimalizie kwa kusema tu kwamba Sheria ama Muswada huu kama utapita kuwa Sheria utakuwa umeunda Ofisi tatu muhimu. Ngazi ya Kijiji, Ofisi ya Kijiji ama Mtaa. Ngazi ya Kata, Ofisi ya Kata na ngazi ya Tarafa Ofisi ya Katibu Tarafa. Itakuwa imetambuliwa kisheria kwamba hizi ofisi ni za Serikali kwa hiyo zitafanya kazi kama ofisi za Serikali. Lakini ofisi hizi ukiziangalia zinahitaji kuimarishwa.

Kwanza ngazi ya kijijii, Kata, Tarafa, hawa Watendaji hawana ofisi kabisa. Wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Kwa kuwa ofisi zao zimetambuliwa kisheria, basi tuanze kujenga na kuimairisha ofisi zao kwa maana ya majengo. Eneo la pili watumishi. Ukichukua ngazi ya kijiji mtumishi yuko mmoja tu ambaye Mtendaji wa Kijiji, lakini majukumu ni mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninapendekeza Serikali ingeliangalia namna ya kumsaidia huyu Mtendaji wa Kijiji, awe na angalau wasaidizi wachache, hasa Askari Mgambo wa kuweza kusimamia utulivu na amani katika eneo lake. Ngazi ya Kata, Mtendaji ni mmoja tu, pamoja na kwamba hana ofisi lakini pia ni kwamba hana watumishi wa kumsaidia, mimi ninapendekeza tungeliangalia namna ya kuongeza wasaidizi katika ngazi ya Kata. Msaidizi angalau mmoja na hasa hasa Askari ama Mgambo hata wawili watatu wanne kwa ajili ya kumsaidia kusimamia utulivu na amani katika eneo hilo.

Eneo la tatu na la mwisho Ofisi ya Katibu Tarafa. Hii ni Ofisi kubwa inahitaji vitendea kazi. Kwa hiyo, ninaomba asaidiwe wasaidizi wa kusimamia ofisi yake. Pia kuwe na Miundombinu, kama kituo cha afya katika kila Tarafa, Kituo cha Polisi katika kila Tarafa na pia kuwe na Mahakama angalau ya kuweza kusimamia Sheria katika ngazi ya Tarafa.

Eneo la nne ambalo ninapendekeza liimarishwe katika ofisi hizi ni bajeti. Ofisi za Serikali ni lazima ziwe na Bajeti ya kuendesha ofisi hizo. Lakini ofisi ya ngazi ya kijiji, Kata, Tarafa, Serikali imezipuuza kabisa kuhusu Bajeti. Serikali inafikiri kwamba hawa watumishi wanaweza kufanya kazi bila kuwa na Bajeti yoyote, Kuna gharama nyingi sana za kuendesha ofisi. Kwa mfano katika ngazi ya Kata, mlinzi wa amani anahitaji kuwa na Mahabusu. Mahabusu wanalazwa pale, wanahitaji kusafirishwa kwenda Wilayani, hana namna ya kuwasafirisha zaidi ya kuwachangisha walalamikaji. Kwa hiyo, ninaomba ofisi hizi ziimarishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya machache ninaunga mkono Muswada huu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati ninataja majina nilikuwa nimesema baada ya mzungumzaji huyu atafuatia Mheshimiwa Michael L. Laize na baadaye Mheshimiwa Mgana I. Msindai. Ninaomba nifanye mabadiliko kidogo, ili Mheshimiwa Mgana Msindai, atangulie na Mheshimiwa Michael L. Laizer, baadaye, kwani kuna dharura imetokea.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kunipa nafasi na mimi nichangie kwenye mabadiliko mbalimbali ya Muswaa huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza mimi nilidhani haya mabadiliko yangelianzia ngazi ya Mkoa. Pale Mkoani tunaye *Regional Local Government Officer,* ambaye ndiye anashughulika na Halmashauri zetu. Huyu mtu yuko pale kama pambo, hajapewa mdaraka na madaraka yote yanafanywa na Afisa Tawala wa Mkoa. Kwa hiyo, mimi ningeliomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hilo. Kwa sababu madaraka tunapeleka kwa umma, basi ianzie pale Mkoani kuwe na mtu ambaye anashughulika na Halmashauri zetu moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, mimi ningelikwenda kwenye mabadiliko Na.17(f) , linalohusu Waziri kuteua Madiwani. Kwa kweli kufanya hivi ni kupora mamlaka za Halmashauri zetu. Kwa sababu tunataka madaraka yaende kwa umma. Sasa hapa Waziri anapoingilia ana maana gani. Sisi tunashauri kabisa hiki kifungu kifutwe. Mamlaka yaendelee chini ya Halmashauri zetu na kama basi Serikali itang'ang'ania.

Serikali itoe mapendekezo ya watu inaowataka kama kawaida waende wapigiwe kura na Madiwani wetu kama tunavyofanya kwa Bunge la Afrika ya Mashriki. Kwa sababu hii, hawa watu kwanza watawajibika kwa nani wakiteuliwa na Waziri, watakuwa wanadharau viongozi wa Halmashauri, Wenyeviti wetu na Mameya watashindwa kuwasimamia hawa. Kwa hiyo mimi ninashauri kabisa aidha ifutwe au kama ndiyo hivyo, yatolewe mapendekezo yaende kwenye Baraza na Madiwani ndiyo wawapigie kura. Hata kama ni vilema, wasomi na watu wa aina hiyo lakini Waziri asiingize vidole kwenye Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningelipenda kuongea juu ya Katibu Tarafa. Katibu Tarafa kama wenzangu ambavyo wamesema ni mwajiriwa wa Serikali Kuu. Sasa hapa anapoingia tena kwenye Halmashauri maana yake inaonyesha kwamba Halmashauri zetu hazina uwezo, ni lazima zipate wakimbizi wa kuwasaidia, kitu ambacho kwa kweli hakipendezi.Kama tunaona umuhimu wa kuwa na Katibu Tarafa. Katibu Tarafa wa Halmashauri ateuliwe na awe moja kwa moja yuko chini ya Halmashauri zetu. Kwanza atasaidia sana kwa sababu ukienda kwenye Kata kuna vikao vya *Ward C*. Kwa hiyo Kata kwenye Tarafa moja zinaweza kuanzisha kama mlivyopendekeza kuwe na Kamati ya Tarafa ya kushughulikia maendeleo. Kwa hiyo, kwa kumweka awe upande wa Serikali na upande wa Halmashauri mimi kwa kweli ninaona ni kwenda kinyume na kupeleka madaraka kwa wananchi.

Tukija kwa watendaji wa Mitaa. Kwenye Majiji, Manispaa na Watendaji wa Vijiji, sasa umefika wakati ni lazima wapewe nyenzo za kufanyia kazi. Kwanza hawa watendaji ukienda sehemu kama Dar es Salaam, sasa hivi wanaoteuliwa ni watu wenye *Degree* zao, lakini unakuta kwanza hawana mahali pa kufanyia kazi. Halafu pili wanawajibika kwa wenyeviti wa mitaa ambao hawana ofisi, hawana vitendea kazi na maisha yao yanategemea kufanya kazi kwa kujitolea. Kwa hiyo, mimi ningelishauri, kuanzia kwenye Manispaa, Jiji na kwenda hata kwenye Kata zetu na vijiji vyetu hawa watu wakumbukwe na watengenezewe ofisi nzuri na waanze kupata Bajeti ya kufanyia kazi zao. La sivyo kwa kweli mambo hayatakwenda kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mabadiliko mimi sijaona wakirekebisha utendaj kazi wa Madiwani. Sasa hivi bado kuna mgongano mkubwa sana katika ya Madiwani na Watendaji. Bado Madiwani wetu hawajapewa elimu ya kutosha, bado wanaingilia kazi za watendaji. Bado hawaelewi wafanye nini wanapokuwa kule kwenye Wilaya zetu. Mimi ningelishauri kabisa, elimu iendelee kutolewa kwa Madiwani wetu, na watendaji ili wasiingiliane. Na sasa hivi kuna Halmashauri nyingine kazi haziendi kwa matatizo hayo.

Mhehimiwa Naibu Spika, mimi niseme kabisa. Tumeishakubali Ma-*VEO,* waanze kupata mishahara, lakini Halmashauri nyingi bado hawa watu wanateseka. Bado hawapati mshahara, na hata kuna Ma-*WEO* ambao mpaka sasa bado wanafanya kazi kama vibarua. Mimi ninaweza kutoa mfano, ukienda Halmashauri ya Mji wa Mpwapwa, kuna Ma-*WEO* 11, kuanzia mwaka 1997 wako kazini lakini mpaka leo hii hawana mshahara. Kwa hiyo mimi ningeliomba kwenye haya marekebisho ningeliomba Serikali iingilie ihakikishe hawa watu wanaingia kazini na wanapata haki zao. Kwa sababu bila kupata haki zao hawatafanya kazi kama inavyostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kwenye mabadiliko haya, mimi ningelishauri. Mabadiliko haya yanapotokea basi hii elimu ipelekwe kule kwa wahusika na hizi sheria zinazobadilishwa zipelekwe mpaka kwenye ngazi za chini. Tatizo tulilonalo tunafanya mabadiliko hapa, Sheria zinabadilishwa lakini wahusika hawazipati hizi sheria. Kwa hiyo, mimi ningelishauri kabisa, Mheshimiwa Waziri ahakikishe hizi sheria zinafika Wilayani, zinafika kwa watendaji wetu kule chini na vile vile zinakwenda Mahakamani, maana kuna zingine zinaingiliana na tafsiri za sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile hata tukifanya mabadiliko ya Sheria hizi, kama hatutaimarisha ofisi zetu za Wilaya kwa kweli tutakuwa hatujafanya kazi ya maana. Sasa hivi kila wilaya watendaji wengi Wanakaimu, na hao wanaokaimu wanakuwa hawana sifa. Sasa mimi ningelimwomba Waziri, ili mabadiliko haya yaende vizuri, apitie wilaya zote aangalie watendaji ambao wanakaimu. Kuna wengine wanakaimu wana sifa. Kuna wengine wanakaimu hawana sifa. Mimi ningeliomba kabisa Mheshimiwa Waziri, hili alifanye liwe kitu cha haraka ili shughuli zetu ziende vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa na haya tu ya kusema juu ya Muswada huu. Kwa hiyo, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na ninaunga mkono Muswada huu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Muswada huu. Kwanza ninapongeza sana Waziri kwa kuleta Muswada huu leo hapa Bungeni. Nitangulie tu kusema kwamba nitauunga mkono Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda tu kumpongeza kwa sababu Muswada wenyewe ulikuwa ni mzito, ni mkubwa. Lakini baada ya kuleta marekebisho leo asubuhi kwa kweli imekuwa ni vizuri sana. Tumefuta baadhi ya maeneo ambayo tulikuwa tuchangie, lakini tungelipenda tu kuchangia machache yaliyopo.

Kwanza marekebisho haya ni muhimu sana kuletwa. Kwa sababu kuna wakati mwingine Serikali inaona ni vema kugawa Halmashauri au kugawa Wilaya. Lakini baada ya kugawa unakuta kwamba kuna sheria vinazonyima Halmashauri kugawanywa. Kuna Halmashauri zilizogawanywa mwaka 2002, lakini kwa ajili ya sheria hii, wameshindwa kuunda Halmashauri mpaka baada ya miaka mitano. Mimi ninasema

kwamba haendani kabisa pa *philosophy* tunasema siku hizi ya Ari Mpya, Kasi Mpya na Nguvu Mpya. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kuletwa Muswada huu sasa tunaweza tukaenda na kasi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Wilaya zetu zimegawanywa mwaka jana, lakini mpaka sasa bado tuko kwenye ile Halmashauri moja ambayo umuhimu wa kugawa Wilaya ni pamoja kugawa hii Halmashauri. Sasa nafurahi kabisa kwamba Muswada huu umekuja na naomba baada ya kupitishwa hizo Halmashauri zianze kazi mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningependa kuzungumzia kwa kuanza na kazi ya Katibu Tarafa. Katibu Tarafa wote tunaelewa kwamba yuko upande wa Serikali Kuu ndiyo msaidizi wa *DC*. Katibu Tarafa kufanya kazi za Halmashauri siyo kwamba kuna sheria iliyoletwa akapewa tena majukumu ya Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kazi yake inabidi kabisa afanye kazi za maendeleo, ukiangalia kazi zilizopo kwenye Halmashauri zetu kazi kubwa ziko kwenye Halmashauri na kazi zilizoko kwenye Kata ni hizo hizo za Halmashauri mpaka kwenye vijiji. Hivi huyo Katibu Tarafa akipewa majukumu ya *DC* itakuwa ni Ulinzi na Usalama basi, je, shughuli zingine kuendesha maendeleo? Kwa hiyo, mimi naona kwamba huyu Katibu Tarafa ukiangalia na ukipima uzito wa kazi uko wapi utaona kwamba uzito wa kazi uko kwenye Halmashauri.

Mheshimwia Naibu Spika, kwa hiyo, labda *DC* akitafutiwa msaidizi kwa kweli mimi nasema kwamba huyo Katibu Tarafa anafaa awe mmoja wa mwajiriwa wa Halmashauri ili aweze akazunguka na akafanya kazi kwenye Kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni kikao kilichowekwa kwa ajili ya ushauri wa *DC*. Hiki ni kikao ambacho hakikuwepo lakini bado naona ni muhimu kiwepo kwa sababu ni kikao cha ushauri, ni kikao cha kuangalia utekelezaji wa kazi, ni kikao cha kukumbushana na kupeana majukumu. Kwa hiyo, mimi bado nasema kikao hicho kiwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu nyingine ambayo ningependa kuzungumzia ni suala la hao Wabunge wanaoteuliwa na Mheshimiwa Rais kuingia kwenye vikao vya *RCC* hapo mimi sioni tatizo kabisa. Naona ni vyema kwa sababu ni viongozi waliochaguliwa na ni lazima wajue ni nini kinachoendelea na ni lazima nao wachangie katika vikao hivyo. Kwa hiyo, sina matatizo hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo yangu yanakuja kwenye wajumbe walioteuliwa na Waziri. Kwanza, mimi sifahamu ni nini kilichowasukuma wakaona kwamba hawa wana kazi kubwa watakayokwenda kufanya katika vikao hivyo. Kuhusu hao tunaomba tu Waziri atusikie na apokee ushauri wetu kwamba hii ni malumbano tu yanazidishwa katika Halmashauri zetu. Kwa sababu kwanza, tuna Madiwani wa Viti Maalum, hao ni watu ambao hawana Kata, unaongeza tena wengine ambao wako tu hewani hawana Kata wala siyo Viti Maalum. Hivi ukiwaongeza hawa pamoja na wale

wa Viti Maalum utakuta kwamba wao ndiyo watakuwa wengi au watakuwa robo tatu ya Madiwani ambao wana Kata.

Kwa hiyo, mimi sioni sababu ya kuwateua Madiwani wengine kuingia kwenye hiyo Halmashauri wala sijui watachaguliwa kwa njia gani, sijui ni mapendekezo tu kwamba kuna watu wanaotafutiwa kazi, sijui ni nini. Kwa hiyo, mimi naungana na wenzangu waliotangulia kusema kwamba hao waachwe tu kabisa kwa sababu haipunguzi chochote kwenye huu Muswada ulioletwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo ambalo nilitegemea sana lingewekwa kwenye Muswada huu kama tunataka kuimarisha Halmashauri zetu. Kuna hili suala la *tender* za Halmashauri, mimi sioni sababu kabisa kwa nini Madiwani wameondolewa kwenye Bodi ya *Tender*. Kwa sababu kuna fedha nyingi sana zinazokwenda kwenye Halmashauri kwa ajili ya miradi ya barabara, kwa ajili ya miradi ya aina yoyote inatakiwa wapewe *tender* ndiyo wafanye. Hakuna Diwani yeyote, hakuna mwakilishi wa wananchi, watendaji wanakwenda kukaa na kuunda kampuni zao, hii kampuni ni ya fulani, hii kampuni ni ya fulani wanapeana hizo *tender* ndio wanazo halafu unasema kwamba Madiwani waje kudhibiti, wanadhibiti nini kitu kilichoundwa na wale wale watu ambao unakwenda kuwadhibiti ndiyo hao hao wamepeana kampuni. Hizi zabuni zilizotolewa ni wao ndiyo wamepangiana halafu unamwambia Diwani aende kuangalia nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata siku moja huwezi ukagundua kwamba fedha zimeliwa kwa sababu wale wale watu ndiyo wanalindana na wale ambao hawakupata hizo *tender* na hawana kampuni nao wanakula fedha za Halmashauri kwa njia nyingine na wale hawathubutu kuwadhibiti kwa sababu wakiwadhibiti na wao watawasema wengine na fedha za Halmashauri zibaki kuliwa tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, badala ya kuleta hata haya mambo ya Madiwani kuwaongeza kule, mngelileta hata hili suala la *tender* tulijadili kwa sababu ndilo linamaliza Halmashauri zetu kila Mbunge hapa anajua kwamba fedha za barabara mlizotuma hazikwenda sahihi zimeliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa vile hili halikuwa kwenye Muswada huu lakini ningependa kusema kwamba na hilo liangaliwe na ni suala la kuleta katika kikao kingine tulijadili ili tuangalie namna ya kuliweka vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu kusema kwamba baada ya Muswada huu kupita, namwomba Mheshimiwa Waziri, sasa zile Halmashauri zote ambazo zimetangazwa kama Halmashauri ya Longido, Halmashauri ya Arumeru na Siha sasa zianze kwa sababu zina matatizo makubwa sana, imekuwa ni afadhali wakati ule kabla hazijatangazwa kwamba zimekuwa Halmashauri kuliko sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ndiyo tunapata shida zaidi kwa sababu kila Halmashauri inajulikana kwamba mradi wake ni huu na huu tupewe sasa na tuanze mara moja. Madiwani wa Halmashauri mpya wakae na hatuna matatizo kabisa kwa sababu kuna Mwenyekiti, kuna Makamu Mwenyekiti. Mwenyekiti kama yupo upande mwingine

ataongoza tu vikao na kama Makamu Mwenyekiti, yupo upande mwingine ataongoza vikao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie Muswada huu. Kwanza, nieleze wazi kwamba naunga mkono Muswada huu na ni moja ya sababu ya kuomba nafasi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nieleze pia kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na tulipata nafasi nzuri sana ya kuupitia Muswada huu na tunamshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa jinsi alivyokuwa muwazi na alivyokuwa tayari kujadili yale yaliyokuwepo na kufikia makubaliano na Kamati katika masuala mbalimbali pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme pia jambo hili ninalielewa vizuri kwamba nimekuwa katika mfumo huu wa Tawala wa Mikoa na Serikali za Mitaaa kwa sehemu kubwa sana ya maisha yangu. Nafikiri nimepata nafasi ya kuelewa mfumo wake kwa kiasi. Ningeomba nitumie uelewa huo huo vilevile kuchangia katika Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza kabisa Muswada huu ni mwanzo wa kujaribu kurekebisha mfumo wa utawala katika Mikoa na Serikali za Mitaa. Ni mwanzo ninasema kwa sababu kutakuwepo na haja ya kuangalia maeneo mengine ambayo hayakushughulikiwa katika Muswada huu na ambayo yasipoimarishwa tutaendelea kuudhoofisha utawala katika Mikoa jambo ambalo litaathiri maendeleo katika Halmashauri katika Mikoa yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utawala ni muhimu sana, pale ambapo utawala uko imara, umepangika vizuri, unafanya kazi vizuri maendeleo yanapatikana. Pale ambapo utawala ni legelege basi tunapata maendeleo legelege pia. Hatupati maendeleo yale ambayo tulikusudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Muswada huu ni muhimu sana kwa kweli kwa Serikali zetu za Mitaa na kwa Tawala zetu za Mikoa na ni vizuri tukatambua hilo na tukalishughulikia. Lakini tumekubaliana kwamba shughuli nyingi zitafanywa katika Serikali za Mitaa, katika Halmashauri za Wilaya, katika Halmashauri za Miji tumekubaliana, kwa hiyo, Serikali itakasimu madaraka yake kwa Serikali za Mitaa ili yatekelezwe katika Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhana ya *eyes on and hands off,* kwa hiyo, kazi kubwa Serikali itakayofanya ni kusimamia kwa kuona kwamba Halmashauri zinatekeleza yale mambo ambayo zinatakiwa zitekeleze na siyo kwenda kuziingilia kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, maamuzi yanayofanywa katika Halmashauri yatafanywa na Halmashauri zenyewe na zitasimamia utekelezaji wa maamuzi hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lazima Serikali ihakikishe kwamba sera zake zinatekelezwa, kwamba programu zake kama MMEM, MMES na Afya na nini zinatekelezwa na vilevile kuhakikisha ya kwamba yale maamuzi ambayo yanafanywa na Halmashauri yanatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya mambo ambayo Muswada huu unajaribu kufanya ni hilo la kuhakikisha kwamba inakuwa *eyes on* lakini *on* kweli kweli. Mheshimiwa Michael Laizer, amesema kwamba watendaji wanaweza wakala zile fedha zinazopelekwa kwenye Halmashauri kwa ajili ya maendeleo. Lakini Madiwani kama hawakuona inatakiwa Serikali Kuu ione na iwaambie Madiwani kwamba kuna ulaji wa fedha hapo ushughulikieni. Nafikiri hiyo ndiyo kazi moja ambayo Mkuu wa Mkoa na *RCC* wanapaswa kufanya ili kuhakikisha kwamba mambo ya Halmashauri yanatekelezwa yanavyotakiwa yaende. Kwa hiyo, siyo *eyes on* na kuachia mambo yaharibike bali ni *eyes on* ya kutaka marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri nyingi sana zinapitisha mambo mazuri kabisa, mpango wa kutengeneza barabara kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine. Mwisho wa mwaka ukifika ile barabara haikujengwa Serikali inapaswa kuuliza wewe ulipanga kujenga barabara mbona hiyo barabara haikujengwa. Nafikiri hiyo ndiyo kazi kubwa ambayo Serikali inapaswa kufanya kuhakikisha kwamba Serikali za Mitaa zinatekeleza majukumu ambayo zimejiwekea. Lakini ili kufanya hivyo tunatakiwa tuwe na mfumo mzuri wa utawala na kama mfumo mzuri wa utawala haupo *then* tuna matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sitazungumzia suala la Katibu Tarafa kwa sababu hili limerekebishwa vizuri kabisa kama wanavyopendekeza Waheshimiwa Wabunge kwamba Katibu Tarafa kwa sasa atabaki katika Serikali kwa muda, Waziri amesema suala hilo litaangaliwa ili baadaye yaletwe mapendekezo pengine ya kutekeleza mapendekezo hayo ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyatoa hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo mengine pia ambayo tumeomba yatazamwe ambayo yako nje ya mapendekezo haya. Ningeomba niyagusie kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Mkoani tumepafanyia majaribio ambayo yamepaharibu. Mwanzoni tulikuwa na Wakuu wa Idara katika Mkoa ambao walikuwa ni kiungo kati ya Wizara, Mkoa na Serikali za Mitaa. Tukaanzisha kitu kinachoitwa Sekretarieti wakaitwa washauri, sasa washauri wa nani sina hakika kwa sababu hatukuelezwa vizuri ni washauri wa nani, nafikiri wanamshauri *RAS*. Kwa hiyo, hakuna tena Afisa ambaye ni kiungo kati ya Wizara, Mkoa na Serikali za Mitaa. Tukaendelea na hatua nyingine tukaweka *cluster*. *(Makofi)*

Kwa hiyo, huyo mtu sasa amepotelea kwenye *cluster* na ni mshauri, sasa sijui ni mshauri wa *cluster,* ama ni mshauri wa *RAS* ama ni mshauri wa kitu gani. Kwa sababu

amepotelea kwenye *cluster* wala hatumwoni. Lakini ukienda ukimkuta anakwambia ni mshauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa kweli hakuna tena kiungo kati ya Wizara, Mkoa na Serikali za Mitaa. Hakuna kiungo kati ya Mkoa sasa na Serikali za Mitaa, maana huyo mtu akienda kwenye Serikali ya Mitaa anakwenda kama mshauri wa kitu fulani. Sasa aliyemwita kwenda kushauri kule kwenye Halmashauri ni nani? Lakini tulitegemea kwamba pale Mkoani pangekuwepo na kitengo chenye wataalam, chenye zana kwa mfano zana za kutengeneza barabara ambazo kila Halmashauri haiwezi kuwa nazo tungeweza tukawa nazo Mkoani zikasaidia Halmashauri. Utaalamu ambao kila Halmashauri haiwezi kuwa nao tungeweza kuwa nao pale Mkoani ili utakapohitaji na katika Halmashauri ukapelekwa katika Halmashauri kwenda kusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunafikiri pale pamevurugika kiasi kwamba hapafanyi tena jukumu lolote la maana na tunapendekeza pale parekebishwe parudie kama palivyokuwa. Sheria inajaribu kurudisha uhusiano kati ya Wizara na Serikali za Mitaa. Lakini itapata tatizo kuvuka hilo korongo pale Mkoani.

Kwa hiyo, pasiporekebishwa sasa hivi Wizara iweze kutumia Afisa wake katika Mkoa kuwasiliana na Serikali za Mitaa. Haya mambo tunayopendekeza hapa kwamba Wizara zitekeleze majukumu yafuatavyo kuhusiana na Serikali za Mitaa yatakuwa magumu sana kutekelezwa. Ni muhimu Wizara zikahusiana na Serikali za Mitaa kwa sababu wao ndio wenye vyuo vya kufundisha, ndio wenye uwezo wa kutafuta fedha, ndio wenye uwezo wa kutafuta wataalam, ndio wenye uwezo wa kutafuta vifaa na kila kitu. Kama hakuna uhusiano imara kati ya Wizara na Serikali Mitaa, Serikali za Mitaa zitaathirika katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tumependekeza na Waziri amelitazama na akaona kweli kuna haja ya kulifanyia kazi ili baadaye lirudishwe tena katika Bunge tuangalie ni jinsi gani tutakavyoparekebisha pale Mkoani pakae sawasawa. Lakini moja ya kazi ambayo inatakiwa ifanyike pale Mkoani ni ile ya *eyes on* kwa maana ya kutazama Halmashauri zitekeleze majukumu yake na kuzionyesha udhaifu uliopo ili urekebishwe kwa manufaa ya maendeleo ya wananchi wetu katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo tunapaona bado pamelegalega na tunapendekeza parekebishwe. Mkuu wa Idara atambuliwe kama Mkuu wa Idara na awe na mawasiliano moja kwa moja na *RAS* na katika masuala ya kitaalam atakuwa ndiyo *focal point* ya Wizara ili Wizara iweze kuwasiliana naye na kupitia kwake kuwasiliana na Serikali za Mitaa. Hatusemi awe ni mtekelezaji katika Serikali za Mitaaa, tuna miradi mingi sana inayotekelezwa nchini sasa hivi ambayo inatekelezwa na Wizara kupitia katika Halmashauri za Serikali Mitaa, kuna *DADPs* katika Kilimo kuna *ASDP* yote itatekelezwa kwa utaratibu huo, *focus* iko katika *District,* lakini tunahitaji *support* kutoka Mkoani na mfumo uliopo sasa hivi hautupi *support* hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Katiba, Sheria na Utawala amezungumzia suala la Dar es Salaam. Pale Dar es Salaam kuna Halmashauri nne, tatu za Manispaa na moja ya Jiji. Hakuna uhusiano uliojengeka unaooanisha hizi

Halmashauri nne. Kwa hiyo, kila mmoja ni Halmashauri kamili inayojitegemea na inayoendesha shughuli zake. Sasa lengo kuwa na Halmashauri ya Jiji ilikuwa ni kuziunganisha hizi Manispaa tatu ziweze kufanya kazi kama kitu kimoja kwa sababu zinafanya kazi katika eneo moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningeomba nipendekeze kabisa kwamba utaratibu ule wa Dar es Salaam usitumike katika Halmashauri nyingine mpaka umerekebishwa, mpaka uwekwe mfumo wa kuwezesha ile Halmashauri ya Jiji kuratibu hizo Halmashauri zingine. Kwa hiyo, watendaji waweze kukutana wakae na wapange mambo yao ndiyo wayapeleke kwenye Baraza. Kwa hiyo, Halmashauri ya Jiji ni lazima iwe na gharama ndogo sana za uendeshaji. Kwa sababu kazi zake si za utendaji, kazi za utendaji ziko katika Manispaa. Manispaa ndizo zinatakiwa zitengeneze barabara, zijenge vibanda vya wafanyabiashara, zihakikishie usafi, ziweke elimu na afya na kila kitu. Halmashauri ya Jiji kazi yake ni kuziratibu ili tupate maendeleo yanayofanana katika Jiji lote. Kwa hiyo, gharama zake lazima ziwe ndogo, lakini lazima wawepo wataalam wenye uwezo watakaohakikisha kwamba huo uratibu kweli unafanyika, wachache, siyo wataalam wengi kama walivyo katika Manispaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunamwomba Mheshimiwa Waziri, alitazame hili suala la Dar es Salaam tujifunze kutokana na matatizo ya Dar es Salaam kabla hatujaenda Mwanza, Arusha na kwingineko kuweka mfumo kama ule. Kama ule mfumo ukiwekwa vizuri una manufaa makubwa sana, usipowekwa vizuri kwa kweli kwa sasa hivi hakuna hata mmoja anayeufurahia, ukienda kwenye Halmashauri ya Jiji yenyewe haifurahishwi na muundo uliopo, ukienda kwenye Manispaa hawa wanafanya shughuli zao kama wanavyoona kwa sababu hawaoni manufaa yanayopatikana katika kuwepo kwa Halmashauri ya Jiji. Kwa hiyo, kuna haja ya kujenga huo uhusiano na kuuwekea utaratibu utakaowezesha utekelezwe ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimwia Naibu Spika, vinginevyo tutapata matatizo ya kila Manispaa kuandaa mipango yake bila kuoanisha na mipango ya Manispaa nyingine na unaweza kukuta mipango ya Manispaa moja inaathiri mipango ya Manispaa nyingine kwa sababu hakuna mahali ambapo wanakaa kuratibu shughuli zao ambazo wanazifanya kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tungeomba sana utaratibu huu utazamwe na urekebishwe na uwekwe vizuri ndipo twende tena tuangalie jinsi ya kulirekebisha na kuweka utawala mzuri katika Jiji la Mwanza pengine na Arusha na kwingineko kama itakavyoonekana inafaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa na hayo machache tu ya kuzungumzia. Lakini naomba nisisitize kwamba umuhimu wa Wizara kuwa na mauhusiano ya karibu sana na Serikali za Mitaa kupitia kwenye Ofisi za Wakuu wa Mikoa na vile vikao vinavyofanyika katika Ofisi za Wakuu wa Mikoa ni jambo ambalo halikusisitizwa vya kutosha. Hawa ndio wenye uwezo wa kwenda kusaidia Halmashauri kutekeleza majukumu yake na kuwa na watumishi wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila atakayezungumza hapa atazungumzia juu ya upungufu wa watumishi wa aina moja ama aina nyingine, lakini vyuo viko kwenye Wizara za Sekta, kama Wizara za Sekta hazifundishi wataalam tutaendelea kuwa na upungufu wa wataalam wa Kilimo, wa Maendeleo ya Jamii, wa Afya na wa kila namna. Kwa hiyo, ni lazima huu uhusiano ujengwe na uimarishwe na tunaomba sana Wizara ya TAMISEMI ijiimarishe ili iweze kufanya jukumu hilo kwa ufanisi mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, naomba kurudia kwamba naunga mkono Muswada huu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia Muswada huu muhimu sana wa Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nitoe shukrani zangu za dhati kwa Waziri na Naibu wake kwa jinsi walivyokuwa wasikivu. Kwa sababu ukiusoma Muswada huu kama tulivyogaiwa Waheshimiwa Wabunge mwezi Julai, 2006 na ukiangalia sasa hivi zile *amendments* ambazo wamezileta kwa kweli wamekuwa wasikivu sana.

Mheshimiwa Naobi Spika, nakumbuka baada ya kuwa nimepata Muswada huu nilimwandikia Mheshimiwa Waziri kama *point* nane hivi za kuonyesha jinsi gani ambavyo Muswada huu una matatizo na katika mabadiliko yote pamoja na ushauri wa Kamati karibuni *point* sita zimekuwa *taken into consideration* na zimefanyiwa marekebisho. Kwa hiyo, huu usikivu wa Waziri na Naibu Waziri wake kwa kweli ni lazima niwapongeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uteuzi wa Madiwani watatu, limezungumzwa na takriban na wazungumzaji wote isipokuwa mzungumzaji aliyemaliza kuzungumza sasa hivi. Nadhani hoja imeweza kuelezwa vizuri. Ninachoshauri ni kwamba tuwe *open minded* tusikilize hoja mahsusi ya Serikali na Serikali isikilize pia hoja mahsusi za Waheshimiwa Wabunge na vilevile kuweza kuangalia kwamba tusianze kuua demokrasia kwa kuhakikisha kwamba uwiano wa kura na Madiwani ndani ya Halmashauri unazingatiwa katika hatua yoyote ambayo Serikali inachukua. Kwa hiyo, nisingependa nilizungumze kwa undani zaidi suala hili kwa sababu limezungumzwa na wenzangu vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ambalo nataka kulizungumzia ni suala *Township Councils*. Muswada ulivyoletwa kwa mara ya kwanza, Ibara ya 16(4)(a) ilikuwa inaanzisha *level* mpya ya Serikali za Mitaa inayoitwa *Township Councils.* Sasa hivi kutokana na mabadiliko ambayo yameletwa ya mwanzo na ya leo asubuhi, *level* hii imefutwa. Kama ilivyo kawaida *amendments* haziji na maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwa maoni yangu, *level* ya *Township Council* ilikuwa inaondoa mgogoro ambao upo sasa hivi kwa kuwa na *level* ya zile *Townships* kwamba kijiji kinaweza kikapanda kikawa ni Mji Mdogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utakumbuka kwamba mara ya mwisho Serikali imetangaza vijiji kuwa Miji Midogo ilikuwa mwaka 2002 mpaka leo hii hiyo Miji Midogo haifanyi kazi,mpaka leo hii hiyo Miji Midogo haijafanya chaguzi za kuchagua mamlaka ya Miji Midogo.

Kwa hiyo, lilipokuja pendekezo hilo la *Townships Council* ambapo ni zaidi ya kijiji kimoja, ni zaidi ya Kata moja, zinaunda *Township Council*, mimi nilikuwa naona ni *very progressive idea*. Sijui ni kwa nini Serikali imeamua kuitoa na bahati mbaya sipo kwenye Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, lakini hii ilikuwa inatatua tatizo la mamlaka ya Miji Midogo ambalo lipo hadi hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo langu mimi lina Miji Midogo mitano, Kagunga, Bitale, Kalinzi, Mahembe na Mwandiga mpaka leo hii uchaguzi uliopita wale watu wamechagua Wenyeviti wa Vijiji, hawajachagua Wenyeviti wa Miji Midogo na ni kwa sababu gani, ni kwa sababu sheria ya zamani ya Miji Midogo, *Local Government Authority Act,* Sheria namba 7 haijaweka mazingira mazuri kama jinsi ambavyo *proposal* hii ya sasa hivi ilivyokuwa imewekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nilikuwa nashauri na nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri aiangalie. Nafahamu kwamba labda hapakuwa na maandalizi ya kutosha ya kuleta Muswada huu, lakini suala la *Township Council* lilikuwa ni *very progressive idea* kwa sababu tunatarajia *District Councils* zikue na zingine zije kuwa Halmashauri za Miji. Lakini haiwezi ikawa *District Council* kwa umoja wake, kwa pamoja ni lazima baadhi ya vijiji vitakua haraka kuliko vijiji vingine. Kwa hiyo, vile vijiji ambavyo vinakua haraka na kama *geographical proximity* iko pamoja vinaendana vile vijiji vipandishwe hadhi viandaliwe kuja kuwa Halmashauri za Miji kwa sababu Mji unakua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika *point* hii nilikuwa naomba sana tufikirie kuhusu Dar es Salaam. Mzungumzaji aliyepita Mheshimiwa Charles Keenja, amelizungumzia na bahati nzuri yeye alikuwa *authority* kwa Dar es Salaam, amekuwa Mwenyekiti wa Tume ya Jiji kwa muda wa kutosha, lakini Dar es Salaam inavyokua ni tofauti kabisa na Miji mingine ya nchi inavyokua. Kwa mujibu wa kitabu cha *Economic World Fact Book* cha mwaka 2000 sasa kinaingia mwaka 2007, Dar es Salaam ni Mji wa nne kwa kukua kuliko Miji mingine yoyote duniani, ni Mji wa nne kwa kukua. Mwakani au miaka mitatu ijayo kuna watu ambao watakuwa wanakaa Mwenge hawaendi Mjini kufanya kazi, watakuwa wanafanyakazi Mwenge au Kijitonyama kwa sababu sasa hivi ofisi zinaanza ku-*move* kutoka *City Centre* kwenda kwenye maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *Township Councils* zinaweza zikasaidia ndani ya Dar es Salaam kwa mfano, ndani ya Manispaa ya Kinondoni kukawa na *Township Council* ya Ubungo, Ubungo ika-*develop* yenyewe, kukawa na *Township Council* labda Mwenge, hiyo ni mifano michache tu ambayo naweza nikaitoa. Kwa hiyo, nilikuwa naomba suala hili tulifikirie, inawezekana lisiweze kutekelezwa sasa hivi, lakini liwepo kwenye sheria na Waziri awe na mamlaka ya kutoa *regulations* kwa ajili ya upandishaji wa maeneo kama hayo. *(Makofi)*

Nilikuwa naomba tufikirie Dar es Salaam kwa upana sana. Dar es Salaam inabadilika sana na uendeshaji wa Jiji la Dar es Salaam unakuwa *more complex* kila siku zinavyoongezeka. Kwa hiyo, hili nilikuwa napenda nilisititize katika suala zima la *Township Council* kwamba irudi kama jinsi ambavyo ilivyokuwa imependekezwa mwanzo. Nitaleta *Schedule of Amendments* kuomba *amendment* ya hiki kitu kiweze kurudi katika Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, tulipoenda kwenye uchaguzi mwaka jana, vyama vilienda na Ilani kwa ajili ya kuomba vipewe ridhaa ya kuongoza. Chama cha

Mpinduzi kikapewa ridhaa ya kuongoza Serikali Kuu na baadhi ya Serikali mbalimbali za Mitaa isipokuwa Karatu, Bariadi na Kigoma Mjini. Kigoma Mjini wananchi walitoa ridhaa kwa vyama viwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi, katika suala zima la maboresho ya Serikali za Mitaa, Ilani inasema sasa hivi Serikali itaenda kujenga *Parliamentary Democracy* katika ngazi za chini. *Parliamentary Democracy* maana yake nini, leo tukifanya uchaguzi, Waziri Mkuu anapoteuliwa, chama chenye Wabunge wengi ndio kinachotoa Waziri Mkuu. Kwa mfano leo Rais hawezi akaamka akamteua Zitto Kabwe kuwa Waziri Mkuu kwa sababu chama chake hakina *majority* ndani ya Bunge. *Parliamentary Democracy* maana yake ni kwamba kwenye Halmashauri za Wilaya, chama chenye Madiwani wengi, ndio kitoe Mwenyekiti wa Halmashauri na ikitokea kwamba hakuna chama kimoja chenye Madiwani wengi zaidi, basi vyama kwa mujibu wa sheria viruhusiwe kuunda *coalition*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mizengo Pinda, anakumbuka mgogoro wa Kigoma, nilikuwa naye Kigoma, amekaa Kigoma wiki nzima, tukazungumza. Tukajikuta kwamba sheria inasema tu Mwenyekiti atateuliwa miaka mitano. Hakuna *provision,* anapatikanaje, anafanyika namna gani! Matokeo yake ni nini, ni kwamba kuna kuwa na *friction* ambazo zinakuwa hazina maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa napendekeza, Ibara ya 21(b) iwe *re-written* na iseme wazi kabisa kwamba Mwenyekiti au Meya wa Halmashauri atokane na chama chenye Madiwani wengi na kama hakuna chama chenye Madiwani wengi, basi vyama viweze kuunda *coalition*. Sasa kwa Tanzania, historia imewekwa kwa Kigoma ambapo leo kufuatia muafaka kati ya CHADEMA na CCM, Halmashauri ya Manispaa ya Mji wa Kigoma inaongozwa na CHADEMA na CCM, kwa makubaliano ambayo siyo ya kisheria, ni muafaka tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mwaka 2000, Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma, Halmashauri ambayo mimi Jimbo langu lipo, hapakuwa na chama ambacho kilikuwa na *majority,* siyo CCM, siyo CHADEMA. Chama cha *NCCR-Mageuzi* kikawa na Madiwani wawili, *difference* ikawa ni Diwani mmoja. *What happened,* sheria hairuhusu *coalition,* kilichofanyika ikawa ni *horse trading* na hii ina-*provide for* rushwa, hii inaweza ikapelekea mtu anayetaka kupata Umeya au Uenyekiti, akahonga hao Madiwani wengine wa chama kingine kidogo, wakaunda Halmashauri, na *that's what happened* Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama Sheria ingekuwa inaruhusu *coalition* kuundwa kule chini, ingeweza kuweka hali muafaka kabisa na wala nchi isingekuwa na *tension* ya kumfanya Waziri atoke Dar es Salaam aende Kigoma, aite Wabunge, afanye nini, tukae wiki nzima tunajadiliana kitu ambacho kwa mujibu wa sheria kilikuwa ni kitu cha saa moja tu, ni vyama kukubaliana, wanakubaliana *a pact* wanaunda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri na nilimwomba toka Muswada huu ulipotangazwa, nilipomwandikia ki-*note* hakunijibu

mpaka leo. Abadilishe hili ili liwe na *a some sort of Parliamentary Democracry* na *in addition to that,* Waziri Pinda wakati amechukua Uwaziri alisikika akizungumza, alirekodiwa na hajawahi kukanusha kwamba ili kuimarisha utendaji wa mamlaka za kifedha katika Halmashauri, kule ambapo Halmashauri inaundwa na chama zaidi ya kimoja, palipo na Diwani wa *Opposition,* basi yule Diwani wa *Opposition* ndiye awe Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha. Hali ya sasa ilivyo ni kwamba hata ujumbe kwenye hizo Kamati za Fedha, watu ambao ni wa *Opposition* wanaondolewa na hii ni *very clear* hata Karatu. Karatu CHADEMA inaongoza Karatu, hatujaweka Diwani hata mmoja wa CCM kwenye Kamati ya Fedha, tunaficha nini? Lakini hiyo ni nyingi zaidi kwa CCM kwa sababu inaongoza Halmashauri nyingi zaidi. Kwa hiyo, nilikuwa napendekeza kwamba iweke sheria kabisa kwamba Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha ya Halmashauri atokane na chama ambacho hakiongozi Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada, Ibara ya 20(c) unaongeza idadi ya Madiwani wa Viti Maalum kutoka asilimia 30 mpaka asilimia 40. Lakini Muswada umeshindwa kuendana na hali ya mabadiliko ya sasa na hasa mabadiliko ya Katiba. Mwaka jana mtakakumbuka Bunge hili Tukufu lilipitisha mabadiliko ya Katiba likasema, Wabunge wa Viti Maalum watapatikana kutokana na uwiano ambao chama kimepata katika uchaguzi wa Wabunge na *reform* mmeiona. Leo Waziri analeta Muswada anarudia kwamba Madiwani wa Viti Maalum, ameongeza idadi, *which is very good*, itaongeza idadi ya wanawake katika Halmashauri zetu. Lakini kutokana na idadi ya kila chama idadi ya Madiwani ndani ya Halmshauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa nashauri Mheshimiwa Waziri kwamba tufanye *amendment* katika hili na nitaenda katika *schedule of amendments* kwamba Madiwani wa Viti Maalum wa Halmashauri watokane na uwiano wa kura ambazo kila chama kimepata katika uchaguzi wa Madiwani. Hii itasaidia sana kuvifanya vyama vigombee kutokana na sera, badala ya *personalities* na itaimarisha demokrasia katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *forum* ya vyama vya siasa kama jinsi ambavyo limependekezwa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani, tunashauri, kwa kuwa tumebadilisha Sheria za Vyama vya Siasa na kwamba kutakuwa na Kanuni za ku-*regulate* Vyama vya Siasa zitakazotolewa na Waziri mwenye dhamana ya Vyama vya Siasa, basi uendeshaji wa *forum* hiyo utokane na Kanuni kama jinsi ambavyo vyama vimekubaliana katika *level* ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, yale mambo *substance* niliyokuwa nayataka kuyazungumza ni hayo na nataka tu moja la ufafanuzi. La ufafanuzi ni kwamba ninavyofahamu, Waziri Pinda ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, si Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa. Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa kwa hali ya sasa ni Waziri Mkuu. Sasa Miswada yote iliyoletwa hapa pamoja na *amendments* zimewekwa Jina la Waziri Pinda. Sasa nilikuwa nataka nipate ufafanuzi, ikoje? Nilitarajia kwa kuwa Serikali za Mitaa ni dhamana ya Waziri Mkuu, ningetarajia kwamba iwepo ni Waziri Mkuu hapa na Miswada ya huko kote nyuma nilivyo angalia

imekuwa hivyo lakini hapa naona ni tofauti kidogo. Kwa hiyo, naomba nipate ufafanuzi katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, ahsante! *(Makofi)*

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii nami leo niungane na wenzangu kwa kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu. Kwanza kabisa, naomba nami nimshukuru Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wake kwa kuuleta huu Muswada ambao kiundani kabisa unaelekeza mabadiliko katika vijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitazungumzia zaidi upande wa Tarafa kwa sababu Tarafa ndiko msingi wa Muswada huu umeibuka. Kwanza kabisa, nikubaliane na mabadiliko kwamba Katibu Tarafa ni muhimu akawepo kama ilivyopendekezwa na hii siyo kusema kwamba pengine inatokana na kitu gani, ni kutokana na mfumo wenyewe wa utawala. Tunae Rais, Rais amekwenda na mkondo huo mpaka huko chini, Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya. Sasa baada ya Mkuu wa Wilaya pale nani awepo? Kwa hiyo, ndiye huyu Katibu Tarafa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama tunataka kujua umuhimu wa huyu Katibu Tarafa, basi tuangalie umuhimu wa Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya, halafu tutakuja kutambua kwa nini Katibu Tarafa yupo. Mimi nasema kwamba Katibu Tarafa ni muhimu na nakubaliana kabisa na mapendekezo yaliyoletwa mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa labda nizungumzie tu katika upande wa watendaji na nashukuru kwamba marekebisho yamebainisha wazi uwajibikaji wa hawa watendaji wa kawaida kwamba hapo siku za nyuma, kulikuwa na tatizo kidogo hasa katika Tarafa na katika Kata. Ilifikia mahali watu wanaanza kuhoji, wewe unawajibika kwa nani, Mtendaji wa Kata anafika mahali anasema mimi nawajibika kwa *DED*. Sasa Muswada huu umefafanua wazi kabisa kwamba huyu Mtendaji wa Kata atawajibika kwa Katibu Tarafa na vile vile Katibu Tarafa atawajibika kwa Serikali Kuu na Halmashauri. Mimi nafikiri kwamba hii ni njia nzuri sana kwa sababu inalenga kuboresha hali ya utawala na hali utekelezaji zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa sababu lengo ni kujaribu kuleta mabadiliko ya kimaendeleo, hebu tuangalie watendaji ambao wako kwenye Tarafa. Ukimchukua Katibu Tarafa ana watendaji wake, Mtendaji *WEO, VEO,* Diwani na wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu ambacho nataka nizungumzie ni hali halisi ya hawa watendaji ambao tunao, inasikitisha sana. Inasikitisha kwa sababu Muswada umezungumza namna ya utaratibu wa utendaji lakini haijazungumzia maslahi ya hawa watendaji, imeacha kabisa kuzungumzia maslahi ya watendaji wakati ikijulikana kabisa kwamba hali ya watendaji ni mbovu. Sasa unawapa majukumu makubwa kama haya bila hata kujaribu kuwasaidia jinsi gani wanaweza wakafanikisha haya majukumu. Inasikitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuchukue mfano wa Jimbo langu, Diwani au Mtendaji ambaye yuko mwisho kabisa kutoka Makao Makuu ya Wilaya, kilometa 270. Huyu Diwani ana shilingi 30,000/= kwa mwezi ndiyo posho yake. Unamtaka aje kwenye vikao hivi ambavyo tayari vimepangwa kisheria na kiratiba. Sijui unategemea kwamba huyu Diwani atafanikisha namna gani hizi kazi zake. Vivyo hivyo hata kwa watendaji wana hali mbaya sana. Wenzangu wameshazungumzia masuala ya kiofisi, masuala ya vitendea kazi.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa nafikiri kwamba ili kusudi tuboreshe huu mfumo ambao umeletwa mbele yetu, ni vizuri tukawaangalia hawa watendaji kwa sababu ndio watendaji wakuu, ndio wanaosimamia maendeleo katika hizo sehemu zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano mdogo tu jinsi mtendaji anavyoweza kufarijika na akatenda kazi yake vizuri. Mimi katika moja ya Kata zangu, baada ya kuona hili ni tatizo kubwa, Mtendaji anakuwa na vijiji zaidi ya vitano, namna ya kuvizungukia inakuwa ni shida, niliamua nitoe motisha kwao kwa kuwapa baiskeli, walikuwa watano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali sasa hivi imeleta mabadiliko makubwa sana. Ni kitu kidogo tu, tumemwezesha huyu Mtendaji kwa kumpa baiskeli ambayo ndiyo imemwezesha kuzunguka katika kufuatilia na vile vile katika kutetea na vile vile kutangaza nini sera za Serikali upande wa maendeleo zinafanyika. Kwa hiyo, wameleta mabadiliko makubwa sana. Nilikuwa nafikiri kwamba Wizara ili kusudi tufanikishe hili, basi iwaangalie hawa watendaji na ni pamoja na wale wa Ugani *(Extension Officers)*. Sehemu zingine wameshafika mahali wamejiamulia kwamba sasa tufanye nini, wengine wamekuwa wakulima, wengine wamekuwa wavuvi. Sasa ni kutokana tu na ile hali halisi, wewe unakwenda kumweka mtu katika umbali wa kilometa 270 hana baiskeli, hana pikipiki na unamwambia kwamba azungukie maeneo, atafanya nini! Lazima aende kwenye sehemu zingine akapate maslahi yake binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lingine ambalo na lenyewe nigusie, linahusu ajira ya hawa watendaji, hasa watendaji wa vijiji. Mpaka hivi sasa inaonekana kwamba haijaeleweka wazi wazi. Mimi katika Jimbo langu nina watendaji ambao mpaka hivi sasa hawajielewi kama wameajiriwa na Serikali Kuu au wameajiriwa na Serikali za Mitaa. Sasa hii imepelekea mpaka kutoa athari kwa upande wao, hasa wanapokwenda kujaribu kuomba mikopo kwenye Benki. Wanapokwenda kwa Mkurugenzi ili kusudi awadhamini, Mkurugenzi anasema hapana, ninyi bado haieleweki sawa sawa mko wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili nafikiri lingeeleweka zaidi. Halafu mbali na hao, lakini kuna wengine hawajapewa ile posho yao. Nadhani ni vizuri, ikaeleweka kwamba hawa ni watumishi. Wakati ulipoamua kwamba uimarishe hii, ulikwenda kuwatafuta. Sasa leo kwa nini uendelee kuwatesa. Mimi nilikuwa nafikiri kwamba hilo nalo lingeangaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu kuna malalamiko ambayo mimi nimeyapata, hayakuwa rasmi, lakini ni kutoka kwa Wenyeviti. Unaposema Serikali ya Kijiji, ni lazima

kunakuwa na Mwenyekiti. Yule Mwenyekiti anachaguliwa, lakini tatizo linakuja, pamoja na majukumu yote ambayo wamepewa, huyu mtu hana kitu chochote pale. Hana posho, hana nini! Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri kwamba ili kusudi tuimarishe ule utendaji wa kijiji, basi tuwafikirie hao wenyeviti angalau wapate hata posho, hata *allowance* kidogo kwa mwezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kuna tatizo la baadhi ya kata zetu hazina Madiwani ambao ndio hao tunaowategemea kwamba wataungana pamoja kwenye zile Kamati mbalimbali kwa ajili ya maendeleo. Mfano, katika Kata yangu moja Diwani alifariki, lakini sasa hivi inakwenda kwenye mwaka hatujampata Diwani mwingine. Nilikuwa nafikiri kwamba kwa sababu Muswada huu umekuja, basi nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ajaribu kufikiria kuagiza ili kusudi maeneo hayo yapate Madiwani kwa njia ambayo ni sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi zaidi nilikuwa nimeamua nizungumzie hayo matatizo ya Tarafa. Lakini kuna hili suala ambalo limekuja la kuongeza uteuzi wa Madiwani watatu katika Halmashauri. Wanakwenda kufanya nini, hawa Madiwani wanakwenda kufanya nini? Tayari tuna Madiwani pale waliochaguliwa, tuna watendaji ambao wako pale, watendaji wa Halmashauri. Sasa hawa tunaowatafuata tena, wanakwenda kufanya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa nafikiri kwamba pengine Mheshimiwa Waziri angelifikiria hilo sidhani kama litasaidia sana, isipokuwa litakwenda kuvuruga tu huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa kunipa dakika tano. Mheshimiwa John Cheyo, aah! Kuna dakika kumi na tano za kwako ndio dakika zenyewe zinazotakiwa. Mchana nafunga, tena watazungumza watu wanne tu basi!

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, lakini umeni-*ambush*. Maana yake nilikuwa nimejitayarisha sasa kuteremsha vitu mchana. Sasa nitatumia uzoefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nataka kusema neno la utangulizi kwamba kazi kubwa ya Halmashauri au Serikali za Mitaa ni maendeleo ya wananchi na ndio maana katika mikutano mingi ya Madiwani, tunasema tusiweke itikadi ya chama. Sisi ambao tuna *Council* ambazo ziko karibu sana kwa ushindani kama sasa watu wa Bariadi walitupa *Council* kwa mara ya pili. Bariadi ndiyo sisi chama tawala pale. Lakini tunasema itikadi nyuma, tuweke maendeleo ya wananchi wetu mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili limefanya kazi na leo tunajivunia kwamba hatukuwa na *Secondary School* Bariadi, lakini sasa tuko mahali ambapo tunawaambia wananchi hebu muende pole pole kidogo kwa sababu wananchi sasa wamehamasika wanataka kujenga *Secondary School* kwa kila palipo na *Primary School*. Ndiyo ari

ambayo wananchi wameipata na hiyo ni kwa sababu tumefika hapo ambapo tumewafundisha kwamba maendeleo ndio jambo la kwanza, itikadi ya *UDP* huku, ya CCM huku! Tuendelee na maendeleo ya watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo kwa maendeleo ya shule, natoa wito kwa Serikali. Kwa kuwa Wanabariadi wamehamasika kiasi hicho, kwamba wanajenga maboma ya shule, wanajenga maboma ya nyumba za walimu, basi Serikali isibaki nyuma katika kusaidia kuhakikisha kwamba maboma hayo yamekamilika kwa kuweka mapaa. Tusipoweza kuwa-*support* wananchi ndio kusema watarudi nyuma katika *issue* yao ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetanguliza hili neno la maendeleo kwa makusudi kwa sababu nilipokuwa namsikiliza Waziri, anasema wanataka kuimarisha Halmashauri hizi kwa mabadiliko ambayo wanataka kuleta. Mimi napinga moja kwa moja, mabadiliko haya kusema kweli ni ubakaji wa demokrasia katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na kinachonisikitisha ni kwamba mtu ambaye anataka kuwanyang'anya wananchi madaraka yao…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa John Cheyo, unataka kutumia kweli neno ubakaji wa demokrasia au?

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Kama… lakini, Mheshimiwa…

**NAIBU SPIKA:** Halipo kwenye Kanuni zetu!

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama halimo kwenye Kanuni zenu na nataka kuliondoa kwamba siyo ubakaji. Lakini tumetunga Sheria ya Wabakaji, sijui kama tuna hili neno. Naomba Mwongozo. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Ninachosema Sheria ya ubakaji, ni Sheria ya Ubakaji. Lakini ubakaji wa demokrasia mimi sifahamu. *(Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naona ni *synonimous* kueleza *exactly* kwamba *you are rapping a democracy*. Ndio tafsiri ambayo nilikuwa nataka kuweka hapa, *to rape democracy*. Sikuweza kupata maneno mengine na nasema haya kwa sababu zifuatazo:-

Kwanza, tangu mwanzo hata tulipokuwa tunajadili mwaka 1997, Sheria ya Tawala za Mikoa, tulisema kwamba tuiondoe Serikali Kuu kwa watu, watu wajitawale wenyewe na sababu hata sisi tulipokuwa tunaomba Uhuru, tulikuwa tunaomba Uhuru, Mwingereza ondoka, utuachie tujitawale sisi wenyewe. Tukasema kwamba basi Serikali Kuu iishie kwa Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ukiusoma pamoja na Waziri kwamba amekubali kurekebisha, lakini mtu unajiuliza, hivi dhamira ya Serikali Kuu ni nini! Ni wazi kabisa *thinking* ya mawazo ya mwanzo ambayo ndiyo yamejitokeza kwenye

Muswada huu, ni Serikali Kuu kutawala mpaka kijiji. Hii ndiyo ni *clear* kabisa. Kwa sababu tukisoma, utasema tumekatazwa, watasema umekatazwa, lakini haijulikani watakujaje kwa njia gani baadae!

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiona Mtendaji wa Kijiji anawajibika kwa *Ward Executive* yaani Kata, wa Kata anawajibika kwa Tarafa, Tarafa anawajibika kwa *DC, DC* anawajibika kwa *Regional Commissioner, Regional Commissioner* anawajibika kwa *President*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ukiangalia kabisa *thinking* ya watu hawa ni kwamba wanataka kutawala mpaka kule chini. Sasa hii ndio nasema, sijui nitumie neno gani, maana yake nikitumia ubakaji mnasema nakosea. Lakini hii ndiyo nasema kwamba unawaondolea kabisa madaraka ya watu wa chini kujitawala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Katiba inasema tutoe madaraka kwa wananchi. *So the issue here, where is the cut off point*, ni wapi Serikali Kuu inaishia ili sisi tuweze kuendelea na mambo yetu. Haiko *clear* hapa na hii ndiyo kitu cha msingi. Waziri amesema maneno mengine, nataka kuimarisha, kuweka…*issue* ni kwamba ni lini Watanzania watajitawala kuendesha mambo yao ambayo ni ya Mitaa yao? *This is the issue* na Serikali inaondosha hii na hii ndicho ninachouliza Serikali kwa nini mnafanya hivyo? Sisi hatukupigana lakini tulipewa Uhuru na Waingereza, chukueni! Kwa nini ninyi hamtupi Uhuru wa kuendesha mipango yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu dhana nzima hii inapingana na kila kitu. Mambo ya *TASAF* mnatuambia ibueni mipango yenu. Leo unatuletea hapa *a District Consultive Council* inasema *to ensure*. Sasa unasema kwamba utatudhibiti tena sisi kwa miradi ambayo tumeibua sisi wenyewe! *Don't you see Honorable Minister, there's a contradiction* katika maeneo haya mawili? Upande mmoja *TASAF*, fanyeni mambo yenu. Halafu huku unatuwekea chombo cha kutudhibiti katika maamuzi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia mpango wa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika hapa ambaye leo amekaa vizuri kama Waziri Mkuu, lakini ni yeye pia anayetuambia ibueni miradi yenu ya kilimo. Leo unatuletea *a Parallel Organization* ambayo ni ya *District Commissioner* na hiyo *District Commissioner* anaendesha hiyo watu wanaingia mle ni *Chairman* tu mmoja na Mbunge, wengine wote ni wataalam! *Why are you doing that?*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiondoka pale unaenda tena kutuchagulia Madiwani watatu. Eti nitachagua vipofu, nitachagua vilema, nitachagua sijui watu ambao tunaona wana ujuzi zaidi. Tumeona juzi hapa tu tumempatia Rais kuchagua Wabunge kumi. Ametuletea vilema? Na siyo kwamba *President* hana watu wa kuweza kuchagua kama Waziri! *Because* kama kuna Chama ambacho kina *bank of well knowledgable Members of Parliament* ni Chama cha Mapinduzi, kimejaa, watu wamejaa humu wenye Ma-*Ph..D*, memgine ni ya *Internet*, lakini Ma-*Ph.D* yako humu. Lakini bado kachagua watu aliowataka wao. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunachojiuliza hawa watatu sio kwa sababu unataka kuchagua vilema. Mimi niwambie kama kweli nia ni hiyo, mbona sisi Bariadi tumechagua kilema na hakuna hata Waziri aliyetuandikia barua kusema kwamba *you have done a wonderful job!* Mimi najua jamani kama ni mambo ya uchaguzi wa Urais mwaka 2010 ili mtu awe na watu watatu, watatu kila *Council* angalau kumpigia debe, si mtuambie tu, siasa ni uwazi kwamba kuna mtu anajaribu kujitengenezea *Costituency* angalau ya watu watatu, watatu kila Wilaya, kila *Council* ya kuweza ku-*support* Urais. Kama ni hilo tuambieni kuliko kwenda kutumia maneno ambayo sitaki kuyatumia, kutuondoshea hata ile raha ya kuchagua. Ehee, unaleta wengine watatu, *for what! (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ubaya wa Bunge letu, wingi unatawala na leo tutasema maneno yote haya, lakini wingi utatawala na wala Waziri usiwe na matatizo kwamba itafutwa hii kitu, haitafutwa. Utakuja kueleza Mheshimiwa Naibu Spika, anayesema ndiyo, itakuwa ndiyo tu. Lakini mimi nasema na nataka niwe *registered,* haya ni matumizi mabaya ya wingi ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mantiki kabisa, Muswada huu ungerudi, kwa sababu hautuongezei mahali popote. Ukiangalia hata matumizi ya fedha, mimi ningefikiri ingekuwa vizuri zaidi kama angetuambia kwamba katika kuimarisha matumizi ya fedha, sasa tunaweka Kamati ndani ya Halmashauri zetu za kuangalia mahesabu ya Halmashauri, hapo ningesema sawa sawa, unaimarisha. Leo labda angetuambia kwamba sasa tunataka kuhakikisha kwamba *District Executive Director* au Mkurugenzi, anaajiriwa moja kwa moja na *Council*. Hapo ningesema ndiyo, unaimarisha.

Leo hii Mkurugenzi ni sawa sawa yeye ni kama anajiona yeye ndiyo *DC*. Mkurugenzi hata kwenda kwenye miradi wengine hata hawaendi, anagoje Madiwani wamalize waje waripoti kwake. Ni kwa sababu hatujaangalia maana ya Utawala, *Local* Utawala ni Madiwani hata wawe wabovu namna gani, sawa! Kwani Bunge hili, hakuna wabovu humu? Ndani ya Bunge hili wabovu wapo, wazuri wapo, wa kati kati wapo, wasomi wapo, wasiosoma wapo. Sasa mtu aje atu-*dismiss* kwamba hili Bunge halifai, ngoja nitengeneze *a Consultative Board* ya Bunge ya kulidhibiti hili Bunge linavyofanya mambo yake! *This is exactly where we are doing here!*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka kusema kwamba kama ni Bunge, ni Bunge la watu wa Tanzania ambapo kuna watu wazuri, kuna watu wabaya, kuna watu wenye akili, kuna ambao wako nusu nusu, ndio hali hiyo. Hata kama vile ni *District Council* hivyo hivyo, kuna wabovu, kuna wazuri. Lakini mimi nakuambia, wananchi wa Tanzania wanataka uhuru wa kuendesha maendeleo yao na Waziri hajawapa hiyo fursa, tunadai uhuru wetu. Hayo ndiyo maneno yetu ya mwisho na Waziri amechukua uhuru wetu wote. Jambo hili ni nje ya Katiba. Siungi mkono hoja hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kipindi cha asubuhi kimeishia hapa. Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge liliahirishwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mara ya mwisho Kamati ya Uongozi ilipokutana kuangalia ratiba za kikao hiki walikubaliana na kuagiza kwamba kesho tumalize Kikao cha Bunge, asubuhi baada ya maswali. *(Makofi)*

Kwa hiyo, napenda kusema hayo kwa sababu bahati nzuri Muswada huu walioomba kuchangia ni wengi kabisa. Kwa maana hiyo, itabidi saa 12.00 jioni tuwe tumemaliza kuchangia, tumuite mtoa hoja aanze kujibu maswali. Kwa hiyo, kuna wenzetu ambao wengine wameomba kuchangia hawatapata nafasi.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, samahani chombo hapa kilikuwa hakifanyikazi kwa hiyo, imebidi nisogee upande huu. Ahsante kwa kunipa fursa ya kutoa mchango wangu katika haya marekebisho yanatolewa katika Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mizengo Pinda, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, ambaye amefanya *presentation* toka asubuhi tumemsikiliza na ambaye kwa kweli mimi nafikiri ametusaidia sana. Nafikiri kwamba mabadiliko yale na marekebisho yale ambayo yamefanyika asubuhi yamepunguza *tension* humu ndani na *in fact* kama uliangalia vizuri ili-*pre empty* mambo mengi. *(Makofi)*

Mimi awali ya yote napenda kuipongeza sana Serikali hasa katika hili linalohusiana na Ofisi ya Katibu Tarafa na kwa kweli eneo lile ni eneo ambalo limezungumzwa hata kwenye *ALART* tumezungumza na hatimaye mimi naipongeza Serikali sana kuonyesha *flexibility* na kukubaliana kuna haja ya kuondoa ile. Nitajaribu kuonyesha na kuchangia kwa sababu nafasi ya Katibu Tarafa, ina maana yake na ina nafasi yake inajulikana.

Lakini nilitaka nianze kwa hilo la kusema kwamba Serikali ikubali kuondoa kipengele kile na ku-*delete* yale maeneo mengine imeleta *compromise* nzuri na napenda kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha, kuipongeza sana Serikali. Lakini nilitaka tuweke mambo katika *perspective* yenyewe inayotakiwa. Hizi *Local Authorities* tulikuwa nazo na baadaye ziliwahi kuondoka zikarudishwa tena. Tukawa na kitu kinachoitwa Madaraka Mikoani, kwa maana ya *decentralization*. Nia na shabaha ya mpango ule ni kuhakikisha kwamba unatoa nguvu zaidi na madaraka zaidi na mamlaka zaidi kwa hizi Serikali za Mitaa kwa maana ya kwamba unaziwezesha kufanya maamuzi bila kuhitaji kufanya maamuzi katika *center* zijiendeshe zenyewe, zijipeleke zenyewe. Kwa kweli, ukiangalia historia za nchi zile ambazo zimepiga hatua kubwa ya kimaendeleo kwa mfano Denmark, Sweden unakuta wao mpaka mapato yake wanayamiliki wao wenyewe na kuendesha shughuli zao wao wenyewe.

Kwa hiyo, mpango wowote unaokuja hapa unatakiwa ulenge kwenye hilo la kuona kwamba unazipa hizi *Local Authorities* mamlaka ya kutosha ya kufanya mambo yake na kuweza kujiendesha zenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini haikumaanisha *therefore* katika mazingira ya kwetu kwamba uachane kabisa na kitu kinachoitwa mtu anaitwa Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Nchi na Mkuu wa Wilaya. Lakini nataka nieleze vizuri, nimewahi kueleza siku nyingine hapa haikueleweka lakini naomba leo nirudie tena. Mkuu wa Wilaya, pale katika Wilaya inayohusika ni msimamizi mkuu wa shughuli zote za Serikali pale Wilayani, ikiwa ni pamoja na hiyo Serikali ya Mitaa iliyoko pale, yeye ni mwakilishi wa Rais katika eneo linalohusika. Huwezi kuondoa pale ndiyo kuna mifano unaambiwa watu wanazungumza habari ya Sweden, watu wanazungumza habari ya Uingereza na kadhalika, wanasema wanazo hizo. Hii mimi nataka nione kama *process* tu haya mabadiliko hapa yanayozungumzwa hapa yanakwenda wanazungumza hata na kuwa na *policy* ya Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, wako wenzetu wamefika hatua kubwa namna hiyo wanaozungumza habari ya Mkurugenzi atokane na wao wenyewe. Lakini mimi nataka kusema kuhusu hii Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, ili tuweze kuelewana vizuri hapa. Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ina majukumu yake, ina hizo suala la kusimamia shughuli zote za Serikali katika eneo linalohusika, ni mwakilishi wa Rais pale katika eneo linalohusika. Pale chini yake pana mtu anaitwa Katibu Tarafa, hii Ofisi ya Katibu Tarafa ni Ofisi ambayo inakuja *immediately* kutoka kwenye Ofisi ya Mkuu wa Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninayezungumza hapa niliwahi kuwa Mkuu wa Wilaya ya Arusha, kwa hiyo, najua hicho ninachokizungumza hapa. Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, unaipa dhamana kubwa mno kiasi kwamba ukiiacha tu inaogelea pale haijui kitu kinachoendelea kule kwenye Halmashauri unapata matatizo makubwa. Lakini majukumu aliyonayo Mkuu wa Wilaya, kama mambo yote yanakwenda vizuri Halmashauri inakwenda vizuri, watoto wanasoma vizuri, watu wanatibiwa vizuri, yeye kazi yake atasimamia mambo ya *law and order*. Mambo ya amani na utulivu ndiyo mambo anayosimamia. *(Makofi)*

Lakini chini ya Katibu Tarafa ukienda kule chini hakuna nafasi nyingine ya Mkuu wa Wilaya. Huyu Mkuu wa Wilaya, ni mtu ambaye anabeba dhamana kubwa katika eneo la Wilaya inayohusika. Huyu unamtafutia nafasi ile ya kwanza acha hii ambayo ilifanyiwa *amendment* halafu baadaye mkaiondoa tukasema hivi itakuwa ni vizuri Katibu tarafa ambaye ni Msaidizi wa Mkuu wa Wilaya akawa anaingia pale kwenye Halmashauri, walau ajue ni mambo gani yanayofanyika pale. Waheshimiwa Waziri Mkuu, Rais, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya, mlikwenda kule Ngurdoto mkafanya semina elekezi mnawaambia Wakuu wa Wilaya waeleze ni nini watakachokwenda kufanya kusimamia elimu, mambo ya MMEM, MMES mambo ya mifereji, mambo ya barabara. Hii ofisi hii unaiachia hapa kwa Katibu Tarafa paa, unasema ikae hapo hapo, isiingie kwenye Halmashauri pale, halafu baadaye una-*hold responsibilities,* Mkuu wa Wilaya unamuuliza hivi tumesema jenga madarasa yako wapi, hana mtu anayeingia pale kwenye Halmashauri. *(Makofi)*

Mimi nilikuwa nafikiri kwamba unachofanya, unafanya *extension* ya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, pale kwenye Halmashauri siyo katika maana ya kuingilia shughuli za utendaji lakini kwa maana ya kuifanya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, iwe *informed* kuhusu

mambo yanayoendelea. Vinginevyo kama ni mambo ya *law and order* huyu Katibu Tarafa atakwenda kulala tu. Mimi nasema ile *arrangement* ya kusema muweke na Kamati zake za Ulinzi na Usalama ahaa, lakini nasema kuhusu huyu Katibu Tarafa. Katibu Tarafa anamfanya Mkuu wa Wilaya ambaye ndiyo Msimamizi Mkuu wa Serikali ajue nini kinachoendelea pale kwenye Halmashauri. Mkuu wa Wilaya kazi yake ni kuingilia kati mahali popote mambo hayaendi, hawezi kukaa pale akasema unajua mimi kule, wamekula hela za MMES lakini sihusiki pale, *never,* hakuna mtu atakubali habari ya namna hii. *District Commissioner is the incharge of the all Government affairs* katika eneo linalohusika *he/she has tell us why* imetokea hivyo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, huyu unampindulia pale asogee ili wakizungumza habari ya maendeleo ajue ni nini kinachoendelea. Mimi naishukuru Serikali kipengele cha kuiweka Ofisi ya Katibu Tarafa, pale moja kwa moja ikae pale na kwamba sasa hawa watoke ilikuwa *problem*. Kwa sababu kwa kweli Katibu Tarafa, ni mtu ambaye anakuja moja kwa moja chini ya Mkuu wa Wilaya. Hii nyingine ya kimaendeleo Katibu Kata, kwa maana ya Mtendaji wa Kata yeye anawajibika kwa Mkurugenzi wa Halmashauri. Haya mambo yote ya Ulinzi na Usalama kwa maana ya Halmashauri ndiye anayefanya pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nasema bado nasema kama unafikiri Mkuu wa Wilaya anatakiwa atumike hivyo anavyotumika lazima asogeze mkono wake pale kwa maana ya kupata taarifa na kujua mambo yanavyoendelea katika Halmashauri. Ukimwamba akikaa pale pembeni wanakaa pale kama *DAS* wananyamaza pale, *you are in trouble. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kuzungumza habari ya maendeleo, hapo tunakuwa na Mkuu wa Wilaya hapa hana habari ya maendeleo ya shule, hajui habari ya mifereji, habari ya maendeleo ya shule, hajui habari ya barabara, hajui habari ya mifereji, hajui habari ya chochote kinachoendelea pale halafu ukasema hivi *it is okay* wewe mzee kazi yako kusimamia *laws and orders*. Nataka tuelewane hilo kwanza.*(Makofi)*

La pili, hapa imezungumzwa habari ya maendeleo pale katika Halmashauri, unasema hivi sisi tutapata matatizo pale kupeleka mtu yeyote anayepelekwa pale. Tumezungumza habari ya wale Wabunge wanaoteuliwa na Rais, wako Tanzania nzima unawapeleka pale, pale wanakwenda kufanya nini unasema hivi, hivi huyu bwana kaja hapa Bungeni miaka mitano akitoka hapa maana yake kule Ikulu haendi kule Mbunge atoke hapa aende Ikulu, Mbunge akishateuliwa na Rais anakwenda kwenye shughuli za maendeleo, mimi nataka niseme Mbunge akitoka hapa kama anatoka Newala tunataka aende pale Newala. Kwa hiyo, pale Halmashauri ikikutana pale hata kama ni wale wanatokana na UWT wataingia pale. Sasa kumbe huyu bwana atakuwa anafanya nini, sasa anakuwa wapi, anafanyaje itakuwa kuwaje? Lakini hili la Madiwani lilozungumzwa ndiyo nilitaka nilieleze.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia hili la Madiwani linalozungumzwa ukianza kuliangalia kwa sura ya kisiasa *it is a problem* ukiangalia kwa sura *political parties* kazi yake ni *capture political power* kwisha. Ukishapata madaraka mambo ya siasa pale yanakuwa yamekwisha mnaingia kwenye Chama kinachoitwa *development*. Halmashauri

inapokutana pale hakuna barabara ya CHADEMA wala CCM, wala ya *CUF* wala ya *NCCR-Mageuzi.* Maendeleo pale ndiyo yanaunganisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii nataka niisema mimi natoka katika Halmashauri ya Wilaya ya Hai, tulikuwa sisi pale, CHADEMA ndiyo walikuwa na watu wengi sisi CCM tulikuwa wachache pale. Lakini mle ndani tunazungumza habari ya *development* pale miaka mitano kumbe msipozungumza maendeleo pale mtafanya nini, mimi nimemuuliza Waziri, Waziri nataka uniambie hivi utamchagua kama Rais anavyomchagua Diwani? Anasema mtakwenda mtakaa katika Halmashauri ya Wilaya ya Hai, nitawaangalia kama kuna viziwi, kuna vipofu kama kuna maeneo ambayo yanaonekana yuko nyuma kimaendeleo mtapendekeza majina na mtayapitisha katika *Council* yenu ndiyo mpelekee majina pale. *(Makofi)*

Sasa kama ni Halmashauri ya Wilaya ya Karatu ambayo ipo chini ya *opposition* ndio mfano mzuri. Ninyi kama mnafikiri huyu hafai ninyi mtapelekaji jina lake sasa, ninyi mtapeleka jina lake pale kufuatana na matakwa yenu ninyi watu wa Karatu. Huyu Waziri hana *prerogative* ya kumtambua kutoka Makao Makuu, nimemchagua mimi Mheshimiwa Edward Lowassa awe Diwani, Aggrey Mwanri awe Diwani wenu niwie radhi Mheshimiwa Waziri Mkuu kama nimekutaja ni kwa vile wewe unafahamika. Hawezi mpaka Monduli wamtajie mtu halafu hao ndiyo hawa ndiyo ambao tunawateua. Mimi sikuona *problem* kabisa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda kuishukuru Serikali kwamba imetuletea utaratibu kwa ajili ya Halmashauri mpya. Utaratibu ule wa nyuma wa kusema tungoje mpaka wakati wa uchaguzi ule unatuletea matatizo makubwa sana. Tumeanzisha Wilaya mpya, Wakuu wa Wilaya wako kule, hawana Wakuu wa Idara, hawana Afisa Elimu, hawana Afisa Maji, hawana ma-*engineer* wako kule wanafanyakazi. Muswada ulioletwa leo hapa unaruhusu kuanzisha Halmashauri bila kungoja uchaguzi madhari mipaka ile ya wakati wa Jimbo la Uchaguzi inabakia hiyo hiyo. *(Makofi)*

Mimi ninayesimama hapa na wenzangu wa Chato na wale wengine wanaotoka kule Masasi tulipata fursa hapa na Serikali ikatukubalia kuwa Wilaya. Napenda kusimama hapa kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Siha, kuishukuru Serikali kwa kutupatia Wilaya ya Siha na sasa tunapozungumza hapa tunaye Mkuu wa Wilaya anaitwa Anna Rose Nyabumbi, ameletwa pale ndiyo Mkuu wetu wa Wilaya. Naiambia Serikali ahsante kwa sababu niliwahi kusimama katika nyumba hii nikaililia Serikali kuiomba itupatie Wilaya ya Siha na leo tunayo Wilaya ya Siha. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wenzangu, nawaomba mpitishe Miswada yote kwa sababu mimi nina maslahi mle ndani. Mimi Wilaya yangu ni mpya na hivi Serikali inasema kwamba kuanzia sasa kwa utaratibu huu uliokuja tutaruhusiwa sasa kuanza Halmashauri bila kusubiri Uchaguzi Mkuu mwaka 2010. Wale wenzangu mnaokwenda kwenye Wilaya mpya mjue hicho ndicho kinachopitishwa hapa, nawaomba tupitishe Muswada huu ili haya yaweze kutekelezwa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema maneno hayo nasema ahsante sana na naunga mkono hoja hii iliyoletwa hapa. *(Makofi)*

**MHE. ADAM K. A. MALIMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii ya kusema machache na mimi katika Muswada huu muhimu sana kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba niseme wazi kabisa kwamba nina kila imani na ninawapongeza sana Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali Mitaa, Mheshimiwa Mizengo Pinda na Naibu wake Mheshimiwa Celina Kombani na pia naomba niseme hapa kwamba mimi ni miongoni mwa watu walio na bahati ya kutembelewa na Mheshimiwa Celina Kombani, Wilayani kwetu na ujio wake ulikuwa na manufaa makubwa sana kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi ya kwangu yanahusiana kimsingi na nadharia nzima ya Serikali za Mitaa. Lazima kwanza kwamba hili ni suala gumu na uelewa wake ni mgumu kwa sababu hakuna *formular* moja ambayo inaweza ikawa *applicable* kwa *situation* zote. Kwa hiyo, kusema kweli watu wanaofanyakazi chini ya Serikali za Mitaa hasa utawala wa Kimataifa wanafanyakazi chini ya mazingira magumu na ninawatakia kila heri na nashukuru kwa kazi yao kubwa wanayofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Aggrey Mwanri, muda mchache uliopita, nadharia ya Serikali za Mitaa ni *decentralization* na kwenye *decentralization* kunakuja *responsibility* katika *level* ile ya chini kabisa ambayo mtaka ijifunze kufanyakazi, lakini kufanya maamuzi katika *level* ile waliyokuwa nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi naomba nisema machache kuhusiana na haya niliyoyaona hapa kwenye Muswada huu. Kwanza kabisa kwenye ukurasa wa 94 kuna nafasi ya *Sector Ministries* inasema *Sector Ministries shall in relation to local authorities perform the following functions,* halafu inatoa maelezo pale na ukiangalia kwa kiasi kikubwa *functions* zake zinahusiana na *human resource management*. Pale ndiyo tunapokwama kwenye Halmashauri kwenye upande wa *(Human Resource Management)* kwenye upande wa taaluma kwa sababu unakuwa na mhandisi ambaye ukiangalia unaona kazi yake iko *underrated* unamwona nani. Sasa *according to this* kwa hii *provision* hapa ni kwamba *Sector Ministry* ita-*ensure* kuwa-*alert assurance the performance monitoring and evaluation of the technical personnel performance*, *human resources development*. Lakini tunapofika kwenye utekelezaji na uwajibikaji wa *technical staff* ndani ya Halmashauri tuna tatizo kubwa na *management* ya hawa watalaam.

Sasa nilikuwa naomba niliseme hilo kwa sababu hapo hapo katika utendaji tena tunaingia na tatizo kwamba tunapokuwa haturidhiki na utekelezaji wao tunamwona nani? Je, tunaripoti kwenye *Sector Ministry* kwamba mtaalam wenu wa maji hana uwezo, tunaripoti kwenye *Sector Ministry* kwamba mtalaam wenu wa miundombinu, Mhandisi hana uwezo, tuna ripoti afya kwamba mganga hana uwezo, tunaripoti wapi, nasema hivyo kwa sababu sisi kwenye Halmashauri za wenzangu tumeona kwamba tunapotaka kuwa na mabadiliko katika watalaam hawa tunataka matatizo makubwa ya namna ya kuwabadilisha. Nasema kwa masikitiko kidogo *mourning* yao tunapokuwa na barabara

mbaya au tunapokuwa na barabara ambayo haikutengenezwa kwa viwango unatarajia labda uende kwa Mhandisi Mkuu wa Mkoa yeye akusaidie, lakini yeye anakuambia kwamba Mhandisi wa Halmashauri hayuko katika *mandate* yake. *(Makofi)*

Sasa mimi nilikuwa nataka nipate maelezo kidogo ya ufafanuzi kuhusu *role* ya *Sector Ministries* hasa katika *control* ya watalaam hii *gap* inaishia wapi na sisi tunavyotaka kwenda na matatizo ya watalaam hawa *mandate* yao inaishia wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nilitaka kulisemea liko kwenye ukurasa 107 ambalo linahusu nguvu ya *RC,* uwezo wa *RC* inasema *for the purposes of this section* halafu inatoa kazi za *RC* mwisho inasema hivi; *"doing all such acts and things as shall facilitate or secure the effective, efficient and lawful execution by the local authorities of their statutory or incidental functions."*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika yote haya nimejaribu kutafuta wapi pana *control* ya *authorities* ya kusema hili sasa mmekosea kwa hiyo, mimi ni kama *RC* nachukua uamuzi fulani. Hapa hamna sehemu ambayo inasemwa *specifically in the event of decision making* ambayo inakwenda kinyume na *excursion by the local authorities of the statutory or incidental functions, RC* ana uwezo gani katika kurekebisha hali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni *introduction* hii ya *Regional Consultative Assembly* ukurasa namba 108. Nilikuwa naomba labda Mheshimiwa Waziri, akisimama anisaidie hasa *economic argument* ya kuwa *Regional Consultative Assembly* ni nini. Kwa sababu tayari humu humu ndani wanaingia *all members of the Regional Consultative Committee*, matokeo yake hii *Regional Consultative Assembly* linakuwa ni *monster* kubwa sana ambao watu wote waliongea kwenye *Regional Consultative Committee* wanaingia tena humu humu ndani.

Sasa sijui kama *function* yao ni *advisory* au hakuna sehemu yoyote ambayo inasema kwamba *decision making* iliyofanywa kwenye *Regional Consultative Committee* inaweza ikawa *overturned* na *Regional Consultative Assembly*. Sijui kama nimeielewa vibaya lakini ninavyoiona hapa ni kwamba ni *The Regional Consultative Assembly* ni kama *advisory board*. Sasa kama ni *advisory board* nilikuwa naomba kwamba labda Mheshimiwa Waziri atakaposimama atuambie kwa nini tuna *Regional Consultative Committee* ambao ina wajumbe hao hao tena na wengine wengi zaidi kwenye *Regional Consultative Assembly. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba nizungumzie hii *District Consultative Committee (DCC)*. Mimi nimefurahishwa sana na hii *DCC* kwa sababu naona ujio wake umechelewa, nadhani kuwepo kwa *DCC* katika ngazi ya Wilaya ni kitu sana. Lakini hapa hapa tena ningependa pawe na *demarcation* ya *responsibility* ambayo ni *transparent* zaidi kwamba hii *District Consultative Committee* je ina uweze *overturn* maamuzi ya *District Council* au pia nalo linakuwa kama ni baraza la ushauri. Mimi ningependa kwa sababu naona hii *encompassing* zaidi inachukua uwezo mkubwa zaidi basi hilo tuambiwe *demarcation* yake iko wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa baada ya kuyasema hayo naomba nirudie sasa kwenye suala zima la *decentralization*. Diwani kimsingi *function* yake ndiyo mwakilisha wa wananchi katika *level* ile ya *Ward*. Tunataka tuwape Madiwani kazi kubwa sana na ndiyo lengo letu kwa sababu wao ndiyo wawakilisha wa wananchi katika sehemu ile kama sisi tulivyokuwa wawakilisha wa wananchi kwa Wilaya nzima. Lakini katika utekelezaji wake pamoja na kwamba sheria zinaoanisha wazi *role* ya Diwani na uwezo wake, utekelezaji wa kazi haulingani na yale ambayo nchi inategemea kutoka kwao.

Sasa mimi nilikuwa naomba Waziri anisaidie tatizo liko wapi? Kwa nini tuna tatizo la utekelezaji wa maamuzi wa Madiwani? Labda *motivation* yao ya kufanya kazi imekuwa ni ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningependa kuishauri Wizara kwamba kwa kuwa kila Diwani anafanyakazi katika eneo ambalo lina *targets* basi labda tuangalie kama tunaweza tukawapatia motisha ya kwamba *remuneration* yao maslahi yao yakategemea na *economic targets* ambazo zinafikiwa na maamuzi yao.

Kwa hiyo, wanapokuwa kwenye *District Council* uwezo wao wa kusimamia maamuzi ya kiuchumi yawe ni sababu ya kuwapa motisha zaidi kwa sababu kusema kweli kwa sasa hivi madiwani na hata viongozi wa Serikali za Mitaa za Kijiji *motivation* yao ya kufanyakazi ni ndogo na ni imani yangu kwamba tutaweza kutengeneza sheria nzuri, lakini kama wao wasimamizi wa sheria hizi katika ngazi za chini hawapati motisha ya kufanyakazi kwa kuweka malengo ya kiuchumi mbele basi siamini kwamba tutapata matunda ya yale ambayo tunayakusudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hayo nilikuwa pia naomba Wizara, katika sehemu mojawapo hapa itupe nafasi ya *Public Participatory Approach (PPA)* ili tujue nguvu hasa ya *public participation* kupitia Madiwani katika *decision making* isiwe ni kitu ambacho ni *theoretical* iwe ni kitu ambacho ni *practical* na kinachoweza kupata utekelezaji wa uhakika zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo, machache naomba niseme kwamba naunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia machache katika hoja iliyo mbele yetu. Napenda nimpongeze kwanza mtoa hoja Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, wasaidizi wake, Kamati kwa mawazo ambayo wamechangia katika uboreshaji wa Muswada ambao upo mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimesimama kwa lengo kuunga mkono hoja hii moja kwa moja. Nitakuwa nayo machache ambayo nakusudia kuyasema kwa lengo la kuboresha Muswada huu. Kwanza naipongeza Serikali kwa kuamua kuweka majukumu yamuhusuyo Katibu Tarafa. Kwa sababu Katibu Tarafa ni mtendaji mwenye majukumu mengi. Lakini ambaye mara nyingi amekuwa akiyumba yumba katika utendaji wake wa kazi na hasa akiyumbishwa kwa sababu alikuwa akienda kwa Mkuu wa Wilaya, akienda

kwa Mkurugenzi anaonekana mahali, haeleweki hasa yuko mahali gani vizuri. Lakini kwa kuwa sasa linakuja kisheria naamini hili litakwenda kutendeka vizuri, utumishi wake utaendelea wake utaendelea kuwa chini ya Serikali Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini utendaji wake wa kazi hakuna namna yoyote ambayo unaweza ukamkwepa Katibu Tarafa asifanye kazi zinazotolewa na Halmashauri. Kwa hiyo, hili naliunga mkono na mimi siamini kwamba litaleta matatizo yoyote. Kwa sababu Makatibu Tarafa walio hodari walikuwa wanafanya hivyo wakifahamu kwamba wanaajiriwa na Serikali Kuu lakini majukumu yao wanayatekeleza chini ya Serikali za Mitaa. Mimi katika uzoefu wa jimbo langu na Wilaya yangu ya Muleba sijawahi kuliona tatizo, Makatibu Tarafa wanafanya kazi vizuri. Kwa hiyo, likiletwa kisheria mimi nadhani watafarijika zaidi na watafanya kazi vizuri zaidi.

Pia nashukuru sana kwanza kwa kuwaongezea nguvu Makatibu Tarafa. Kwa sababu Watendaji wa Kata na Vijiji wao walikuwa wanajiona kwamba wanawajibika moja kwa moja kwa Mkurugenzi. Kwa hiyo, pamoja na kwamba Katibu Tarafa yuko karibu yao sana lakini walikuwa wanaona afadhali waende kwa Mkurugenzi kisha huyu Katibu Tarafa anawatumia Watendaji wake wa Kata na wa Vijiji kama namna vile wamsaidie. Si kwamba ilikuwa ni wajibu wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa kitendo cha kwamba sasa huyu Mtendaji wa Kata na wa Kijiji atakuwa yuko moja kwa chini ya Katibu Tarafa mimi naamini kwamba majukumu haya yatakuwa sasa yamedhibitiwa na utendaji wa kazi utakwenda kuwa ni mzuri zaidi na mimi naamini kabisa katika mtazamo huu wa ari mpya, kasi mpya na nguvu mpya haya mambo yatakwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niseme tu hii ngazi ya Ukatibu Tarafa *I mean* u-Katibu Kata ambaye sasa anapewa majukumu mapya. Naiunga mkono moja kwa moja, nikiwa tu napenda kwamba pengine nipendekeze kuhusu upatikanaji wa Mtendaji wa Kata. Tulizoea kwamba Watendaji wa Kata wanafanya *interview* kwenye maeneo yetu ukiondoa Dar es Salaam hapo sijui wanapatikane kwa sababu Dar es Salaam Watendaji wa Kata nafikiri wote kama sio wote ni wachache waliobaki. Lakini karibu wote wana digrii za Vyuo Vikuu. Sisi tuliobaki bado tunao wale wa darasa la saba wenye vyeti vya kughushi ambao wanajua wenyewe walivyovipata, walioletwa kwa sababu ya fulani.

Sasa hali hii kwa namna fulani mimi naona inadhoofisha majukumu makubwa ambayo anatakiwa ayatekeleze Katibu huyu wa Kata pamoja chini ya Katibu Tarafa. Kwa hiyo, pendekezo langu mimi nililokuwa nalo nilikuwa napendekeza kwamba Serikali ingebadilisha utaratibu wa kuwapata hawa Watendaji wa Kata na wa Vijiji kwa sababu zamani kulikuwa na tatizo kubwa sana la kuwapatia mishahara. Mishahara yao ilikuwa inapatikana kutokana na makusanyo ya kodi na mapato mbalimbali ya Halmashauri za Wilaya ya Halmashauri zinazohusika. Kwa sasa hivi mishahara ya Watendaji wa Vijiji na Watendaji wa Kata inatolewa moja kwa moja na Serikali Kuu. Kwa hali hiyo baada ya kuondoa tatizo hilo mimi nilikuwa napendekeza sasa Serikali ingebadilisha upatikanaji wa hawa Watendaji wa Vijiji na wa Kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapomaliza kidato cha nne na cha sita iwe kama *post* wanavyopata *post* wanaotaka kwenda kwenye ualimu, wana-*opt* kwamba mimi nikimaliza nitapenda kwenda kwenye ualimu na kama *marks* zake zinamruhusu basi anapangiwe ualimu moja kwa moja. Anabaki kupokea fomu kutoka Chuoni kwenda kujiunga.

Mimi ningeshauri pia kuanzishwa hii *direct employment* ya Mtendaji wa Kata inayotoka moja kwa moja kwenye Serikali anapomaliza Kidato cha Nne kwa sasa itaonekana na kwamba huyu amemaliza kidato cha nne na itabakia tu kumweka kwenye *refresher course* ili aweze kufanya kazi vizuri za Serikali. Nilikuwa napendekeza hilo likirekebishwa tunaweza kuwa na Makatibu Kata, Watendaji wa Kata ambao wataweza kushiriki vizuri katika utekelezaji wa mikakati ya kutekeleza majukumu ya kimaendeleo katika maeneo yao.

MNnachopenda kushauri ni kwamba Watendaji hawa wajitahidi sana kutojihusisha masuala ya kisiasa. Watendaji wengi wa Kata sasa hivi na wa Vijiji wamegeuka kuwa ni wanasiasa, wanashabikia vyama vya siasa na kushabikia wagombea wa vyama vya siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokuwa katika kikao cha Baraza la Madiwani la Muleba la tarehe 21 Oktoba, 2006 ambao ni mwezi uliopita, ni wiki tatu, kufika siku ya leo, Madiwani wanalalamika sana, Waheshimiwa Madiwani wa Muleba wa Baraza la Muleba wanalamikia sana utendaji mbovu wa Watendaji wa Kata, kauli mbovu inaonyesha kwamba sasa Watendaji wameamua sasa na wenyewe kujifanya ni chama kingine cha siasa. *(Makofi)*

Hali hii haiwezi kuleta amani na kama hakuna amani kati ya viongozi wa kuchaguliwa na hawa watumishi wa Serikali maana yake hata majukumu yanayotakiwa kutekelezwa hayatatekelezwa ipasavyo. Hili wajiepushe sana Watendaji wafanye kazi za utendaji. Wajiepushe na tabia za chuki, wajiepushe kutumia mamlaka wanazopewa kuzitumia kwa namna ya kulipiza visasi au kukomoa watu wengine. Hii itaweza kusaidia kuharakisha hali ya maendeleo na kuleta upendo na amani kwa watu ambao wanakusudia kwenda mbele kwa lengo moja.

Lakini pamoja na ombi langu hilo, mimi naishauri Serikali upya masuala ya kuwapa vitendea kazi. Utendaji kazi wa Watendaji wetu hawa wa Kata na Vijiji wakati mwingine unarudishwa nyuma na kupungukiwa na nyenzo za kazi. Zamani walipewa pikipiki saa hizi hawana pikipiki. Hawana Ofisi kama ambavyo imeelezwa na inavyokusudiwa kurekebishwa. Lakini Ofisi peke yake bila kuwa na vitendea kazi bado watashindwa kufanya kazi zao vizuri. Nilikuwa nashauri hili lifanyike ili kuweza kuona kwamba tunaweza kupiga hatua mbele kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo naomba Serikali ilitazame inapokusudia kuboresha hizi ngazi Katibu Tarafa na Mtendaji wa Kata na hata Vijiji, isiache kuangalia hawa Madiwani wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi kirefu sana tangu mwaka 2000 nilipoingia Bungeni mpaka leo mwaka 2006 napenda kushukuru kwamba aliyekuwa Naibu Waziri wa Wizara ya TAMISEMI sasa hivi ndiyo Waziri kamili. Kila akijibu maswali yetu yaliyokuwa yakihusu kero za Madiwani alieleza kwamba Serikali haina uwezo na mimi nakubali. Lakini naomba siku ya jana siyo ya leo mambo yaende yakiangaliwa siku hadi siku ili Madiwani waangaliwe vizuri zaidi. Uonekane uwezekano wa kuwapa posho hawa Madiwani zinazolingana katika *Council* zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha kuona hata posho za Madiwani zinatofautiana kutoka *Council* hadi *Council* kutegemeana eti na kipato chao. Lakini kama Serikali Kuu imekubali sasa hivi kugharamia au kubeba mzigo wa uendeshaji wa Halmashauri zetu, mimi naomba hata hivyo iangalie, iangalie posho za Madiwani iziweke vizuri. Lakini ikubali pia kwamba pale mahali ambapo Madiwani hawafanyi kazi vizuri hata kazi za utekelezaji wa Ilani hazitakwenda vizuri. Kwa hiyo, pia uangaliwe uwezekano wa kuweza kupewa vitendea kazi ili waweze kuwa na hali iliyo bora zaidi, hali ambayo itaweza kusaidia utekelezaji wa Ilani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi jambo ambalo siungani nalo moja kwa moja katika Muswada huu, siungani na suala la Waziri mwenye dhamana kuteua Madiwani watatu. Mimi hilo siliungi mkono. Kwa sababu mimi katika muda wangu wote ambao nimekuwa Mbunge, mimi nina kawaida kila Bunge linapokwisha lazima niende Jimboni. Nikutane na wenzangu katika ngazi mbalimbali kwenye vijiji, kwenye kata, kwenye Wilaya na kwenye Mkoa hata tunapokuwa tunazungumza na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, mimi sijasikia hili dai la kwamba wanahitaji kuwa na Madiwani wa ziada. *(Makofi)*

Tatizo lililotokea Kigoma litazamwe kwa namna ya pekee. Lakini lisiwe ni chanzo cha kuongeza Madiwani wa kuteuliwa. Hawa Madiwani wa kuteuliwa wanaweza wakatuletea matatizo makubwa zaidi. Kwa sababu mimi sijui kama ni ombi la nani, wala sijui ni shinikizo la chama gani au la vyama gani, sijui ni *NGO* gani, wala sijajua ni maombi ya wananchi wa Jimbo gani au wa Mkoa upi, mimi sijaelewa. Na wadau kama walikaa wakalijadili hili kama litasaidia kuendesha *Council* mimi nadhani wanatafuta sasa kuvuruga sasa *Council.*

Mimi nadhani wanatafuta sasa kuvuruga *Council,* kwa sababu hakuna namna yoyote ambayo utaweza kuweka watu watatu ambao hawapingani. Sasa unataka kuleta upinzani ambao kwenye kugombea hatukukutana nao tukutanenao katika kuendesha *Council*. Mimi sioni sababu. Vyama viendelee kusimama kidete kuhakikisha kwamba vinapata Madiwani katika Kata na wa Viti Maalum na utaratibu mwingine wowote mzuri utakaokuwa umekubalika. Lakini ambao zaidi utakuwa unaweka namna bora ya kuziendesha Halmashauri. Mimi nadhani hili halitasaidia.

Sisi shinikizo tulilokuwanalo ambalo kama leo Mheshimiwa Waziri atalitolea tamko atakuwa ametusaidia sana. Atuambie lini tuanze kumletea orodha ya Kata za kugawanywa. Tuna Kata nyingi ambazo zinasubiri zipewe kibali cha kugawanywa. Ni kubwa sana, nyingine bado zina miundombinu mibovu. Lakini kwa sababu ni kubwa

mno na hazifikiki hata Diwani mmoja ambaye hana vitendea kazi anazishindwa. Hii ingeweza ikatusaidia sisi kuliko kuongeza hawa Madiwani wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba pia Serikali iongeze mkakati wa namna ya kutatua kero za wananchi katika masuala ya jamii ikiwemo elimu ambayo inaendelea vizuri, ulinzi na usalama, kwetu Kagera unasikia tunavyolalamika matatizo ya wakimbizi na mambo mengine ya ajabu ajabu. Hayo ndiyo yanayotusumbua ambayo nafikiri hata wananchi wakisikia Serikali yetu imetoa tamko itakuwa imesaidia. Tuongeze vijiji ili mamlaka za wananchi zizidi kuwa karibu zaidi, wananchi watoe mawazo yao zaidi, tuwe na mikutano na Madiwani na wananchi watoe mawazo yao zaidi. Tuwe na mikutano ya Madiwani na wananchi ambao wanawaeleza nini *Council* zao zinafanya. Haya mimi naamini yatasaidia kwa sababu wananchi watapata habari zaidi, watatoa mchango zaidi, na yataweza kusaidia kuendesha *Council* zetu. *(Makofi)*

Vilevile Serikali iangalie namna ya kudhibiti utendaji kazi wa vyombo vyake, Mahakama, maeneo wanayoshughulikia masuala ya ardhi sasa hivi kumeanzishwa na Mabaraza. Haya Mabaraza ya Ardhi muyaangalie sana Waheshimiwa Wakuu wa nchi, haya hayana matatizo makubwa sana, yalitegemea kutenda kazi nzuri lakini sio kila mahali inapotenda kazi nzuri. Iangaliwe polisi iboreshwe, ipewe vitendea kazi ili wafanye kazi zao kwa haraka na kwa uaminifu zaidi. Vile vile maeneo ambayo wananchi wanadai haki zao, haya ndiyo mambo ambayo yanasumbua. Kuna mambo mengi ambayo wenzangu wamekwishayazungumza ambayo sasa hivi yanakabili jamii na jamii imekasirika, kuna mambo ya ubakaji ya watoto wadogo. Kuna mimba za utoto, kuna walimu hawatoshi, kuna madarasa hayatoshi, haya ndiyo yanayotukabili na Serikali iweke nguvu zake hapo kuona kwamba haya yakishakuwa yamepata majibu mimi naamini kabisa kwamba tunaweza tukaenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi langu la kumalizia naipongeza Serikali, ilichelewa lakini imeamua kuhakikisha kwamba wale Wabunge sasa wanaanza kuhudhura vikao, Wabunge wa Viti Maalum kunyimwa haki ya kuhudhuria vikao kwa kweli ilikuwa ni kosa kubwa sana. Kwa sababu hili lilikuwa linawalenga hasa wanawake wameteuliwa, tayari viti vyao maalum vimekubalika kisheria. Lakini katika vyombo wanapotakiwa kutoa maamuzi hawapati nafasi. Hili lilikuwa jambo baya sana. *(Makofi)*

Naipongeza Serikali kwa kuona kwamba sasa limerekebishwa na mimi naliunga mkono kwa wale wanaoteuliwa na Rais vile vile naunga mkono lakini vile vile naomba sheria nyingine ziangaliwe. Mimi sijui ni sheria ama ni maamuzi, Diwani wa Viti Maalum haruhusiwi kuwa Mwenyekiti wa *Council,* haruhusiwi kuwa Mwenyekiti wa Kamati, mimi sijui ni sheria ama ni tabia za *Council* sijajua. Ni taratibu za maeneo gani? Kama ni sheria naomba hii irekebishwe, kwa nini Diwani wa Viti Maalum asiweze kuwa Mwenyekiti wa *Council* kwa nini asiweze kuwa Naibu Mwenyekiti, kwa nini asiweze kuwa Mwenyekiti wa Kamati? Huku ni kuwapa viongozi nafasi halafu mnawanyima haki zao kitu ambacho naona siyo sawasawa. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Sema mwanangu.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, naomba kwa heshima na unyenyekevu kabisa nirudie kusema naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Huyu alikuwa Naibu Meya wa Mwanza wakati mmoja. *(Makofi)*

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Naibu Spika. *(Kicheko/Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Naibu Meya?

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabla ya yote nipende tu kuchukua nafasi hii kabla sijasahau nipende kutamka rasmi kwamba naunga mkono Muswada huu utakaopitishwa leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi linapozungumzwa suala la Halmashauri hizi ninaguswa kwa sababu moja ya kitu ni kwamba nimeshawahi kuwa kiongozi katika haya yanayoongelewa, ukimwongelea Katibu Tarafa, nilishawahi kuwa Katibu Tarafa, ukiongelea masuala ya Halmashauri nimeshakuwa Naibu Meya wa mfululizo wa miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nianze la kwanza kabisa kukushukuru Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii ambayo nilikuwa nina wasi wasi nayo kwamba inawezekana nisingeweza kuipata, lakini basi nashukuru kwa hili kwamba kumbe na mimi nilikuwa katika orodha. Ninapenda nianze kuzungumzia suala la huyu Katibu Tarafa. Katibu Tarafa anawajibika *fully* yaani moja kwa moja kwa Serikali Kuu, hivi sasa chini ya Mkuu wa Wilaya, bosi wao ni Mkuu wa Mkoa. Wakati Katibu Tarafa huyu akifanya kazi chini ya Serikali Kuu niwaambieni ukweli ni kwamba huwa hakuna kiungo kati ya Katibu Tarafa huyu na Halmashauri ambazo hivi sasa tunaongelea leo chini ya Waziri mwenye dhamana. Hakuna kabisa, pana *vacume* hapa katikati yaani iko hewa ambayo huwezi ukaivuta hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi ukamwambia Mkurugenzi akatoa amri kwa Katibu Tarafa, atasema siyo Serikali yangu. Serikali kama Serikali Kuu nayo inapotoa amri, huyu atamtolea kauli nani huyu Katibu Tarafa huyu, amwambie Afisa Mtendaji atasema nitapokea amri ngapi. Niwaambieni iliyo kweli, mimi nilishafanya kazi hii. Sasa katika hili labda tukubaliane tu kwamba kama tunampokea huyu Katibu Tarafa kweli aingie moja kwa moja kwenye Halmashauri, ili ajue anapokea amri ya nani maana ukimchukua Mkuu wa Wilaya *okay* ndiye yuko kule kwenye Serikali Kuu, unamchukua Mkurugenzi yuko kwenye Serikali za Mitaa, wakutane kwa chombo gani? Wanakutana kwenye chombo gani ili kusudi wamkutanishe, wakutanishe maamuzi yao ya kuweza kuunganisha Afisa Mtendaji na Katibu Tarafa. Hakuna kiungo hapo katikati, mnielewe hivyo mimi nilishafanya kazi hiyo. *(Makofi)*

Lakini ninachotaka kusema nimeona mimi limeletwa kwenye maagizo kule tunakopokelea maagizo kule. Mnasema kwamba eti naye Katibu Tarafa awe na kikao. Katibu Tarafa awe na kikao gani? Cha maamuzi gani? Mnavyosema Katibu Tarafa

anasimamia ulinzi na usalama, mnamnyang'anya madaraka huyu Afisa Mtendaji? Maana kwa hivi sasa Afisa Mtendaji ndiye anayesimamia ulinzi na usalama katika maeneo anayotawala yale. Sasa huyu Katibu Tarafa atakuwa na kikao gani na Wajumbe gani? Atakuwa na wajumbe gani? Hebu jamani sisi wote tunatoka huko nadhani ninyi, chekecheni ubongo ana wajumbe gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu Afisa Mtendaji ana Wenyeviti, wote anawabeba. Sasa na yeye ndiye Katibu, Diwani ndiye Mwenyekiti, yeye atakuwa na nani? Hata na wewe Mbunge si unaalikwa? Sasa yeye atakuwa na chombo gani ambacho kitamwezesha awe na maamuzi ya kwenda hapo mbele ya safari kwamba eti na yeye kakaa ili aweze kutoa maamuzi ya kuweza kusikilizwa na Serikali, hakuna, hana chombo Katibu Tarafa.

Sasa tukubaliane kwamba Kamati ya Maendeleo ya Kata maana yeye ndiye anabeba wote kutoka huku chini anakwenda, anapofika yeye katika ngazi ya Kata, Katibu Tarafa hana chochote tena kingine na bado yeye ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, huyu Afisa Mtendaji yeye Katibu Tarafa ataning'inia hapa katikati ataishi katika hiyo *vacume* ninayoisema, atakuwa hana chombo chochote ambacho kitaweza kumwezesha aweze kuwa na maamuzi ya kusikilizwa katika ngazi yoyote ile. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi niombe katika hili kama Katibu Tarafa basi, kama tunamhitaji huyu Katibu Tarafa basi aingie moja kwa moja kwenye Halmashauri ili *chain of command* iende moja kwa moja ifike mahali sasa kama kuna kitu cha ku-*amend* kutoka kwa Mkurugenzi na *DC* sijui kiundwe kitu gani hapo katikati kuizima ile *vacume* ili kusudi basi *I mean* maazimio ambayo yatatoka kwenye Ofisi ya Halmashauri yaweze kuingia kwenye Serikali Kuu kwa *DC* moja kwa moja.

La pili, mimi nipende kuongelea juu ya Waziri mwenye dhamana ya kuteua. Kwa kweli hebu acheni tu, hivi tunaongeza ongeza tunaongeza nini jamani? *Too much, it is harmful* jamani, kwanza sisi tu hebu niseme tu iliyo kweli, mtanisema huko nje, lakini niseme tu iliyo kweli. Sisi tu Wabunge wa Viti Maalum kwenda kuingia kwenye majimbo kule wenye majimbo nao wanajiuliza wanasema, hivi amekuja anatafuta jimbo? Anafanya, anafanya! Sasa leo tena wanakuja wa kuteuliwa, lakini hata sisi wenyewe, tunajua sisi siyo wa kuteuliwa. Sisi ni wa kuchaguliwa Viti Maalum. Shangilieni, sisi ni wa kuteuliwa bwana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wa kuchaguliwa siyo wa kuteuliwa. Tuna vikao vyetu, lakini hata hivyo bado wanasema sisi ni wa kuteuliwa. Sisi si wa kuteuliwa, sisi ni wa kuchaguliwa, tuna vyombo vyetu ndani ya vyombo vyetu ambavyo huwa tunavitumia. *(Makofi)*

Sasa katika hili hebu tupunguze tu mgogoro, tufike mahali sasa tena wanatafuta wa kuteuliwa. Waende wapi? Waende wapi? Mara ya tatu waende wapi? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapana, kwa hili naomba tuone kwamba hawa hebu kwanza, hebu acha kwanza sisi tuambae ambae wale tulio na vyombo vya kuchaguliwa.

Kuna Mbunge mmoja alizungumza suala la Madiwani na *tender*. Hebu niombe jamani suala la *tender,* hebu Madiwani walau mmoja tu kutoka kwenye Kamati ya Fedha mmoja tu ili itakapofika wakati wanakaa *finance* Madiwani hawa wapate mwakilishi. Hivi kwa nini Diwani anabanwa kiasi hicho cha kutokuingia kwenye Kamati ya *tender?* Kwenye ajira anawekwa, kwenye maboresho anawekwa, ikiguswa fedha hafai. Ninyi vipi? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu tufike mahali jamani, hawa Madiwani nao wafikiriwe basi kwamba wanayo akili ya kufikiria kwamba fedha inayoingia kwenye Halmashauri yao wanapaswa kuwa na mwakilishi wao mbele ya safari wapate kumwuliza. Hivi nini, si ni mmoja tu aingie humo aweze kuona nini fedha inavyoambaa ambaa MMES, MMEM na nini jamani na mambo mengine mengi tu ya *tender* hizi? Hivi mmoja tu inawauma nini ili aweze kueneza ambacho na yeye hata akikataa peke yake si atasema? Tunawaonea mno hawa Madiwani jamani. Tufike mahali na wenyewe wawe na kitu mahali ambapo hapana pesa tunawajaza, ambapo pana pesa tunawanyofoa, kwa nini? Na nikitaka kusema tu ni kweli kwamba kweli huko ndiko wanakofanya kazi hawa Madiwani, *we are the top,* sisi tunapokwenda kule tunakwenda kuwaunga mkono lakini tunawaunga mkono kwa msingi upi? Hebu tufike mahali basi na miradi yote wawe wanaielewa na thamani zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa kwa maana ya *RCC* huyo kwa kweli anayekwa kwenye Mkoa eti kuwakilisha Halmashauri ni sifuri. Kwa sababu sisi Wabunge tumo humo humo kwenye *RCC,* hivi yeye anakaa pale anajadili nini anapokuwa kwa *RC* anajadili nini? Yeye atoke sisi tuwemo tu mle ili mradi tu Wajumbe kwenye *RCC* na kila kitu nadhani mambo yote yatajipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini narudia nasema jamani tumuenzi Diwani, na Diwani na kweli mahala popote anapolalamika basi tufike mahala Wabunge wote tumwone anatufaa kama Shina na sisi tuwe Matawi ambayo yanaweza yakaunga mti ukawa hai katika kulijenga Taifa hili. Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba basi kwa ridhaa yako niweze kutumia nafasi hii uliyonipa kutoa maelezo au ufafanuzi kutokana na hoja mbalimbali zilizojitokeza leo asubuhi na jioni hii. Lakini kabla sijasema hivyo naomba kwanza basi niwashukuru sana wale wote ambao wamechangia Muswada huu kwa kutoa maelezo moja kwa moja hapa Bungeni, lakini vile vile kwa maandishi. Kwa hiyo, mtaniwia radhi inawezekana baadhi ya maandishi bado yanapita kuja kwangu lakini naomba angalau hawa nilionao kwanza niwatambue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni Mheshimiwa George Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala. Lakini pili, ni Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mbunge Viti Maalum, Naibu Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, TAMISEMI. *(Makofi)*

Pia waliochangia ni Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Michael Laizer, Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimwia Adam Malima, Mheshimiwa Ruth Msafiri na mwisho ni Mheshimiwa Maria Hewa. *(Makofi)*

Waliochangia kwa njia ya maandishi ni pamoja na Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa Savelina Mwijage na Mheshimiwa Ania Said Chaurembo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana kama nilivyosema pengine baadhi sikuwa-*include* hapa, lakini nitaomba wataalam wangu kama kuna michango iliyoingia wakati niko hapa basi wanikumbushe ili niweze kunisaidia kuwakumbuka katika orodha yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema naomba niwashukuru sana Wabunge wote kwa sababu, mabadiliko haya tuliyowasilisha hapa kwa kupitia Muswada huu, yamezaa mjadala mzuri, mjadala kidogo ambao ulinifanya nikawa msikilizaji kweli kweli kwa sababu ilibidi nijue kabisa ni nini kinatafutwa na kwa nia hiyo nzuri tuone na sisi tutatoa maelezo gani. Lakini nataka niseme kwanza mambo ya jumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni mdau mkubwa sana katika suala zima la kupeleka madaraka kwa wananchi kupitia Serikali za Mitaa. Ni Serikali hii hii ambayo kila kukicha inajaribu kubuni mipango, inajaribu kubuni programu zinazowezesha kusaidia Halmashauri zetu ziweze kufanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa zaidi. Ninyi Waheshimiwa Wabunge mnajua Serikali hii haina dhamira hata kidogo ya kuvunja Serikali hizi za Mitaa na ama kwa namna yoyote ile kujaribu kusitisha zoezi la kupeleka madaraka kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni Sera ya Chama cha Mapinduzi, iko ndani ya Ilani ya Chama chetu, lakini kubwa zaidi ni jambo la Kikatiba na hakuna namna ambavyo leo tungeweza tukafanya jambo linalotaka kuvunja Katiba ya nchi yetu. Kwa hiyo, nilitaka niliseme hili kwa nia njema tu kwamba mambo yote mnayojaribu kuyaona Serikali inayafanya ni katika jitihada za kujaribu kuziweka Halmashauri hizi katika nafasi ya kuwatumikia wananchi vizuri zaidi. Sasa katika kufanya hili inawezekana kabisa tukaonekana tumekuwa *exessesive* katika maeneo fulani fulani au pengine tukaonekana kama tunatoa hisia zinazoelekea pengine kutaka kutoa picha kama hiyo. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge nia hiyo haipo, wala hata fikra za kufanya jambo hilo halipo. Rais kasema, Waziri Mkuu alikwisha sema lakini na ninyi wote mnajua ndiyo maana Serikali yetu inafanya kila juhudi kuhakikisha Halmashauri hizi zinakwenda vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka nitoe angalizo vile vile. Mimi kama msaidizi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye eneo hili, lakini ninajua hata ninyi Waheshimiwa Wabunge mnajua kwa sababu kila tunapokutana Bungeni mnayo malalamiko mengi sana kuhusiana na utendaji wa Halmashauri zetu katika maeneo yetu

makubwa sana na mara zote mnaitaka Serikali ijaribu kufanya kila linalowezekana kuondoa haya ili tuweze kupiga hatua mbele na wananchi waweze kunufaika vizuri zaidi. Hili nalo msije mkaona kama ni jambo dogo, ni jambo kubwa na ni wajibu wa Serikali muda wote kuhakikisha kwamba tunajaribu kufanya kila litakalowezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu na la mwisho la jumla, ninataka niseme tu kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni moja tu. Hiki chombo kinachoitwa Serikali za Mitaa, tusije tukafika mahali tukafikiri ni Serikali nyingine tofauti kabisa na Serikali iliyopo sasa hivi. Maana tukifanya kosa hilo tutafika mahali hapa kila linalojaribu kufanywa na Serikali, linaonekana kama vile ni jambo linafanywa na mnyama mmoja amekaa kulia anataka kuingilia Serikali zetu wakati kusema kweli sisi ni Serikali moja. Hawa ni Mawakala wa Serikali Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vyombo hivi ndiyo vimepewa kazi ya kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Haiwezikani Serikali Kuu, imewapa jukumu hilo, inawapa fedha, inawapa watumishi, inawajengea mazingira mazuri ya kufanya kazi halafu mseme mkishafanya hivyo basi kaeni pembeni msiulize, msitake kujua kitu gani kinachofanyika, tutakuwa tunafanya makosa makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimeona nisema haya kwa sababu katika michango iliyojitokeza unapata mawazo kama kwamba pengine tuna Serikali mbili, moja imesimama upande mmoja na nyingine upande wa pili na kwamba jitihada za upande mmoja kusaidia upande wa pili inaonekana kama vile inakuwa nongwa. Wakati kwa kweli lengo ni zuri na kazi yetu ni kurekebisha kasoro hizi ili tuweze kwenda vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba basi niende katika maeneo moja moja, nijaribu na mimi kutoa maelezo. Eneo la kwanza, ni la Makatibu Tarafa. Naomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla wenu, wako wanaoona jambo hili kana kwamba pengine halistahili kuwepo, lakini nafarijika tu kwamba wako wengi wanaona bado ni nafasi inayoweza ikasaidia sana katika kusukuma maendele katika nchi yetu.

Hoja niliyoiona kubwa ni ile kwamba maadam tumedhamiria kupeleka madaraka kwa wananchi, ingependeza kama chombo hiki kingewekwa moja kwa moja chini ya mfumo wa Serikali za Mitaa. Naomba niwahakikishie kwamba rai hiyo mimi binafsi, lakini hata viongozi wangu Wakuu, hasa Mheshimiwa Waziri Mkuu, tumesema wazi wazi tuichukue rai hii, kwa sababu haikinzani na azma nzima ya kujaribu kusimamia shughuli za maendeleo. Lakini haiwezekani tukaseka kwamba Katibu Tarafa asiwepo. Ninyi wenyewe mnajua kutoka kwa Mkurugenzi anayefuatia ni Mtendaji wa Kata, ipo *gap* kubwa sana na ndiyo maana wakati mwingine Mtendaji wa Kata naye anakuwa ni Mungu Mtu pale, anafanya anavyoona anahitaji mtu wa kumsaidia. Kwa hiyo, hili nadhani ni jambo la msingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunazidi kuliomba Bunge hili, mkubaliane na rai, hasa baada kuwa tumeondoa maeneo mengi ambayo Serikali ilikuwa imeyaweka

kwa dhamira ya kutaka kuimarisha usimamizi wa shughuli za maendeleo katika ngazi ya Tarafa. Sasa tumeridhia tumesema vema nadhani mawazo ya Wabunge ni mazuri. Tumuache Katibu Tarafa, lakini tumpe majukumu ya ujumla ya kusimamia shughuli za maendeleo katika Tarafa nzima. Maana hilo nalo hatuwezi kulikataa Waheshimiwa Wabunge. Huyu anamwakilisha Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Wilaya anamwakilisha Mkuu wa Mkoa, viongozi hawa wote kwa ujumla wanamwakilisha Rais, lazima awepo mtu anayeitwa angalau Katibu Tarafa, ambaye kwa ujumla ataona kama mambo ambayo yameambiwa Serikali za Mitaa zitekekeleze kweli yanatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakubali kabisa kwamba Ofisi hii ya Afisa Katibu Tarafa huyu haijaimarishwa sana. Hilo tunalikubali na juhudi Serikali inafanya kuimarisha Ofisi kwa kiasi cha kuridhisha. Tutakachofanya na hili tumeshauri sana na hata Kamati yetu ya Katiba, Sheria na Utawala, kwamba ili pasiwe na uwazi katika eneo hili, ni vizuri basi katika ngazi ya Wilaya Mkuu wa Wilaya akajengewa uwezo zaidi kidogo kama ilivyokuwa zamani, anakuwa na labda *DAS* wasaidizi kadhaa hivi, wanapewa jukumu la kusimamia shughuli za maendeleo katika Tarafa kadhaa, kila mmoja katika eneo lake, ili huyu Katibu Tarafa, sasa atazamwe chini ya Mkurugenzi na huyu mwingine abaki ana-*over see interest* na masuala yote kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili mimi nafikiri kimsingi kama Serikali sidhani kama lina ugomvi mkubwa isipokuwa hatuwezi kuliamua leo kupitia Muswada huu, linataka maandalizi, linataka maamuzi ya Baraza la Mawaziri, ili kwa baadaye tuweze kuliweka sasa vizuri zaidi kwa kadri itakavyowezekana. Narudia kuwashukuru, tena sana.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni bahati mbaya tu kwamba kwa sababu tumekuwa na marekebisho mengi, kwa hiyo, baadhi ya Wabunge wamekuwa wakizungumza wanaingiza na yale ambayo tayari tumekwishayaondoa. Lakini hilo tunalikubali, linatokana na marekebisho. Lakini alichobakia nacho kwa kweli Katibu Tarafa ni usimamizi wa jumla. Uratibu wa jumla, kwa sababu lazima am-*feed DC* wake kuhusiana na kazi zinazoendelea pale katika Wilaya. Hili ni eneo la kwanza. *(Makofi)*

Eneo la pili, ambalo nalo limechangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi, sitaweza kuwataja mmoja mmoja, nimeshawakiri tangu mwanzo, ni eneo la Kamati ya Ushauri ya Maendeleo ya Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa mara nyingine niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, wameelewa nia nzuri ya Serikali na kwa kweli wengi wameona na wanadhani tumechelewa. Tulitakiwa kwamba tumefikiria wazo hili mapema zaidi kidogo, kwa kuwa Mkuu wa Wilaya pale ni kiungo muhimu sana katika kumsaidia Rais kujua kinachoendelea ni nini katika Wilaya yake. Tumeliweka bayana, majukumu yake kama mtakavyoona kwenye mabadiliko tumeachia ni majukumu ya jumla kabisa, ambayo yanamsaidi tu, kupata picha ya mambo yalivyo katika Wilaya. Lakini ni chombo vile vile ambacho watakapokusanyika kunaweza kuwa na masuala ambayo, yana-*cut accros* Wilaya nzima na mahali peke yake pa kuyazungumza ni kupitia Kamati ya mashauriano kama hiyo. Yametokea majanga kwa mfano. Umetokea ujambazi usioelezeka umetokana na nini. Hata ukichukulia tu ujenzi wa Shule za Sekondari kwa

maana elimu ya ujumla, bado ni muhimu wakawa na *forum* mpaka ambapo mambo ya namna hii yazungumzwe kwa pamoja, ili yaweze kupenya kwa kila mdau, akitoka pale tuseme tumeelewana. Sasa nimeulizwa na kwamba tungependa tupate ufafanuzi. Kamati hii haitakuwa na madaraka ya kutengua mamuzi ya Baraza la Madiwani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili tumelieleza wazi wazi kabisa. Kamati hii ni ya mashauriano. Tumesema kamwe haitakuwa na mamlaka ya kutengua maamuzi halali ya Baraza la Madiwani. Maamuzi yale yamefikiwa kwa utaratibu mahsusi wa kisheria kwa hiyo, yataheshimika. Lakini kama katika kuangalia Wilaya inavyokwenda hata yale mliyoamua ninyi wenyewe kwenye Mabaraza yenu mnashindwa kuyatekeleza, chombo hiki tulidhani kinaweza kikawa ndiyo nafasi nzuri ya kuhimiza, kusisitiza haja na umuhimu wa kutimiza yale waliyokuwa wamekubaliana. Ni mahali pa kushtuana tu, ni mahali pa kukumbushana ili mambo katika Wilaya yaweze kwenda vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nigusie hili la siasa kwa sababu lilizungumzwa. Hatukuwa na dhamira mbovu hata kidogo na ndiyo maana utaona katika lugha tuliyoiweka tumetambua kwamba chini ya Sheria ya Mfumo wa Vyama vya Siasa, liko hili jukumu la kuwa na kitu kinachoitwa *a code of conduct* ya kusaidia tu nchi iweze kuendesha shughuli zake vizuri zaidi bila mikwaruzano na kwa kuheshimiana. Sasa ninyi wote mnajua siasa ziko Wilayani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tulichosema kwamba mnapokuwa na *forum* ambayo ina-*involve* viongozi wa kisiasa wote na wadau wengine mbalimbali, pengine huu ni mwanya mzuri, kama kuna mahali mnasigana sigana na kwa misingi, kwa *a code of conduct* mliyokubaliana wenyewe ni mahali pazuri pa kuwekana vizuri, kuasana, kutiana moyo ili kwa kweli, demokrasia ya mfumo wa vyama vingi iweze kushamiri kama ambavyo tumekubaliana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba tu nirejee kusema nawashukuru sana, eneo hili bahati nzuri mmelichangia vizuri, lakini nimeona tu niongeze maeneo machache kadhaa kwa kuwa nilidhani ni vizuri tukayatolea ufafanuzi wa kina juu ya jambo hili. Sikupata maelezo magumu sana kuhusiana na uanzishwaji wa Halmashauri mpya, nawashukuru wote ambao mmechangia kwenye eneo hili na tunadhani litasaidia sana kuharakisha maendeleo katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ni jambo moja kuomba upewe Wilaya. Lakini ni jambo tofauti kuwa na Halmashauri. Wilaya ni Utawala, lakini unahitaji nyenzo ya maendeleo ili utawala ule uweze kuwa na maana. Ukibakia na *DC* pale na *OCD* na *DSO,* kazi kubwa mtakayoipata pale ni ya Ulinzi na Usalama. Lakini ukitaka kweli kusukuma maendeleo lazima Halmashauri iwepo. Kwa hiyo, kikwazo cha kisheria kilichokuwepo ndicho kilichopelekea tukawasilisha pendekezo hili kwenu na mimi nasema, ahsante sana, kwa bahati nzuri mmelipokea vizuri, tunajua sasa zile Wilaya ambazo zilikuwa ni utawala tu, baada ya muda si mrefu na wao pia wataanza kuona manufaa ya kuwa na Bajeti zao na Wakurugenzi wa na miradi yao, sasa kusimamiwa kwa nguvu zaidi kuliko ilivyokuwa hapo awali. Kwa hiyo, mimi nadhani kwa hili tunasema ahsante sana kwa

sababu mmelikubali bila matatizo magumu sana, mfano uliopo katika Manispaa ya Kigoma Ujiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumelazimika kuweka jambo hili kwenye Sheria makusudi kabisa. Tulipokuwa Kigoma, bahati nzuri Mheshimiwa Kabwe Zitto, alikuwepo, alitusaidia sana tena nakushukuru kweli kweli kwa sababu tulikuwa pamoja muda wote. Tumeona ni vizuri iwekwe kwa mujibu wa sheria ili kuondoa uwezekano wa hapo baadaye watu kuja na *formular* nyingine ambazo zinaweza zikaleta migogoro hasa tunapokuwa na *team* au vyama viwili vinavyolingana. Sasa ili mradi utaratibu huu umewekwa kisheria, hakuna namna ambavyo mtu mwingine ataweza kuleta kitu tofauti na hiki ambacho mmekikubali kwa sababu sikuona kwamba kulikuwa na mjadala dhidi yake, kwa kiasi ambacho naweza nikasema pengine mlikuwa na nia ya kutokubali. Kwa hiyo, mimi nasema ahsante kwa jambo hili na tunadhani sheria ikipita itarahisisha sana baadhi ya kazi ambazo tulikuwa tunaziona mbele ya safari hapo baadaye. *(Makofi)*

Naomba niseme vile vile kwamba Mheshimiwa Kabwe Zitto, katika mjadala wake, katika majadiliano, hoja zake alizozitoa wakati anazungumza hapa alieleza vile vile uwezekano wa kuwa na vyama zaidi ya viwili katika eneo moja, maana kwa sasa Kigoma Ujiji ni viwili tu, CCM pamoja na CHADEMA, kazi ilikuwa rahisi kidogo. Lakini je, mkiwa na chama kingine, akatoa mfano wa Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, alivyoeleza ni kweli kabisa na mimi nadhani ni vizuri mkaacha mambo hayo yakaenda kwa utaratibu kama huo endapo jambo hilo litajitokeza. Kwa sababu si jambo linalohitajika kufanywa mpaka liwekwe kisheria, kwa sababu baada ya pale kwa kweli hakuna aliyehoji, hivi nani hapa amekwenda upande gani, kwa sababu hapakuwa na sababu mtu alivyoamua kuunga mkono upande mmoja au upande mwingine. Kwa hiyo, mimi nilidhani badala ya kuwa na utaratibu wa kisheria tulilitazama sana, lakini tukafikiri huu ukibaki hivyo, iwe ni kitu kinatokea pale *spoteneously* kulinga na mazingira ni nzuri zaidi kuliko kama mtauwekea utaratibu ambao pengine unaweza ukawa *too rigid* na pengine usionekane kwamba una maana sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine lililojitokeza ni uwakilishi wa Madiwani wa Upinzani katika Kamati za Fedha. Sasa ilikuwepo rai hapa kwamba ni vizuri Kamati hiyo ikaongozwa na Mwenyekiti ambaye anatoka upinzani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo haliwezekani. Haliwezekani kwa sababu sheria ilivyo hivi sasa mkishapata Madiwani katika *Council,* hatua inayofuata ni kumpata Mwenyekiti wa *Council* na Mwenyekiti mtampata kutokana na kura mtakazo piga Madiwani mtakaokuwemo kwenye kikao hicho. Akishapatikana Mwenyekiti huyo, Mheshimiwa Kabwe Zitto, basi iwe bahati yako, kama atakuwa ni wa chama kingine *Alhamdulillah,* huyo ndiye atakuwa Mwenyekiti wa Kamati. *(Makofi)*

Sheria inasema Mwenyekiti wa Kamati hiyo ya Fedha, ni Mwenyekiti wa Halmashauri. Kwa hiyo, njia nyingine yoyote utakayojaribu kui-*formulate*

haitawezekana, kwa sababu Sheria ndivyo inavyosema na kwa hiyo Wenyeviti wataendelea kutokana na Wenyeviti wale wa *Council,* popote pale itakapokuwa imetokea. Sasa Mheshimiwa Kabwe Zitto, alisema niliwahi kusema kwamba hawa watakuwa wenyeviti, nikajiuliza kweli kweli, hili nimelisema wapi? Kwa sababu mimi mwenyewe ndiye ninayeisimamia sheria hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilichowahi kusema ni kwamba tunawatia moyo kokote pale kwenye Halmashauri, kama mnayo Kamati ya Fedha ambayo haina mpinzani ndani lakini mnao Madiwani, hata kama ni wachache kiasi gani ambao ni wa upinzani, hakikisheni mnakuwa na Mjumbe angalau mmoja kutoka upinzani na mimi narudia kulisema hili kwa nia nzuri tu. Bado ndiyo ninavyotazama mimi na sioni kama lina tatizo. Ndiyo maana pale nilipoambiwa kwamba yupo mpinzani mmoja au wawili, lakini Kamati ya Fedha, wameamua asiwemo hata mmoja, mnatoa hisia dhidi ya Kamati hii na pengine chama ambacho ndiyo kinatawala, hofu za bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna njama za wizi, wala hakuna njama za ubadhilifu pale, ni mipango ya maendeleo inayohusiana na hiyo Halmashauri, sasa mnaadhibiana hilo kwa nini? Na sehemu nyingi nimetembea, nimekuta wamejitahidi, wameweka Wapinzani, kunaweza kukawepo kuna Mpinzani mmoja katika *Council* yenye watu 40 hata ukimpeleka kwenye Kamati ya Fedha, *so what?*

Mimi sioni kama ni tatizo hata kidogo, ni kwamba angalau ajue kwamba hakuna kitu cha ajabu pale ambacho kinatengenezwa na njama kutoka upande mmoja. Sasa kama rai yako ilikuwa ni hiyo, nasema ni kweli nilisema na bado ninawatia moyo kokote kule waendelee kufanya hivyo. Na ninyi mnapokuwa ndiyo *majority* na ninyi mfanye hivyo, kwani mnaficha kitu gani pale? Nadhani nimejieleza kidogo vya kutosha *on this one. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee sasa na muundo wa Halmashauri ya Jiji na Sekretarieti za Mikoa. Karibu ushauri wote tulioupata mimi binafsi nasema ni ushauri wa msingi kabisa. Kwenye Halmashauri yetu ya Jiji la Dar es Salaam, tumekuwa tukipata kweli minong'ono, malalamko ya namna moja au nyingine na jambo hili tayari tumeshaanza kulifanyia kazi, kwa maana tu ya kutathmini kwamba tumeanzisha mfumo huu, kumekuwa na matatizo gani. Tumekwenda *smoothly* kwa kiasi gani. Je, kuna maeneo tunaweza tukayarekebisha na kadhalika na kadhalika?

Kwa hiyo tumelipokea, tumepokea ushauri huu, tutaimarisha tathimini hiyo ili baadaye tuweze kuja na mawazo mapya kuhusiana na muundo muafaka wa Jiji la Dar es Salaam, kabla pengine hatujaanza kufikiri miundo kama hiyo kwa maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sekretarieti za Mikoa, nalo hili nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge linafanyiwa kazi. Bahati nzuri tulipokuwa Ngurdoto, Rais mwenyewe alielekeza jambo hili litazamwe kwa maana ya kuona muundo hasa unapohusisha na Wizara za Kisekta.

Kwa hiyo, ni jambo sasa liko chini ya usimamizi wa Katibu Mkuu Kiongozi, kiongozi na timu ya Makatibu Wakuu, tujaribu kuona muundo upi hasa pale kwenye mkoa unastahili kuwepo ili tuweze kuoona *Sectorial Ministerial* tutafanyaje, TAMISEMI wenyewe uhusiano wao na Halmashauri na wenyewe uweje, ili Halmashauri zetu ziweweze kufanya vizuri zaidi. Kwa hiyo, mimi naamini hili nalo tumelipokea, tutajaribu kuona tunakokwenda ni namna gani tunaweza kuboresha maeneo yote mawili.

Eneo lingine lililojitokeza kwa nguvu sana ni hili la upungufu wa watumishi katika Halmashauri zetu na suala la kukaimu Wakurugenzi na Kukaimu Wakuu wa Idara. Tumelipokea, lakini nataka niwahakikishie Wabunge wote kwamba jambo hili Serikali imekwishalibaini na inalifanyia kazi na ninyi mnajua kwamba zoezi linaendelea.

Kwa hiyo, hatua ya kwanza iliyochukuliwa ni Idara Kuu ya Utumishi, kuruhusu nafasi zilizowazi ambazo zina Makaimu Wakuu wa Idara, popote pale kwenye Halmashauri, ili mradi Kaimu huyo ana sifa za kumwezesha kuwa Mkuu wa Idara, Halmashauri zimeagizwa zenyewe ziwathibitishe hao wote huko huko kwenye Halmashari zao. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba tu nitoe rai kwa sababu ninyi Waheshimiwa Wabunge ni watu muhimu kwenye maeneo haya, kama mtakuta jambo hili kuna jambo halijafanyika, mimi nafikiri ni kumkumbusha tu Mkurugenzi aweze kutimiza hili ili kwa kweli kuwe na watu ambao ni *substantive* wako maeneo na wanaweza wakafanya maamuzi. *(Makofi)*

Kuhusu Wakurugenzi, eneo hili kama mnavyojua ni kweli wakati mwingine inatokea wanakuwepo Makaimu kwa sababu fulani fulani. Lakini tumejitahidi sana kama Serikali, kuhakikisha wanakuwepo Wakurugenzi kamili. Hata katika zoezi la mara ya mwisho lililofanyika, baada ya kuwaengua wale waliokuwa Wakuu wa Idara, kuwavua yale madaraka ya Ukurugenzi, tulihakikisha tumeweka Wakurugenzi kamili wakati hawa wengine wanatafutiwa nafasi ya kuweza kufanyia kazi. Kwa hiyo kazi hii tunaendelea nayo na tunaamini tutaifanya kwa kasi kubwa zaidi kwa kuwa ni muhimu sana katika kuimarisha Halmashauri zetu za Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepokea rai kuhusiana na ajira za Ma-*VEO* na Ma-*WEO,* lakini nataka niwahakikisheni Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na eneo hili. Ma-*WEO,* naweza nikasema kwa aslimia kubwa kabisa wote wameajiriwa na Serikali Kuu na walio wengi wanalipwa na Serikali Kuu kwa mtindo rasmi kabisa kupitia *computer.* Lakini wako wachache ambao sifa zao kwa mujibu wa Sera ya Menejimenti na Utumishi wa Umma, sifa zao hazitoshi, lakini tumekuwa nao. Hawa hawawezi kuingi katika mfumo tunaouzungumza sasa kwa vile sifa zake hazitaendana na sera hiyo. Hawa wengi wao bado wanalipwa mshahara kupitia, *Voucher* kupitia kwenye Halmashauri zao na tumewaambia jiendelezeni, muda si mrefu itabidi tufike mahali tuamue kama huna sifa hizo basi lazima uondoke. Kwa bahati nzuri mmoja wa Wabunge hapa amelieleza vizuri sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, msipotusaidia mkafumba macho wale wasio na sifa baada ya mwaka 2007, inaisha mwaka 2007 hii. Hii *grace period* ikiisha lazima mtuunge

mkono tuhakikishe kwamba ni wenye sifa tu ndiyo wanaweza kuwa Watendaji wa Vijiji na Watendaji wa Kata, vinginevyo uwezo ule tunaujua sisi kama ndiyo utaendelea kusimamia fedha zote hizi miradi mikubwa hii tuliyonayo ni dhahiri kabisa tutaendelea kupata matatizo katika Halmashauri zetu. Kwa hiyo, tutaomba sana muda ukifika basi jambo hili tuungane pamoja ili tuweze kulimaliza vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ma-*VEO,* wengi sasa wako kwenye mishahara kupitia *computer.* Tunayo bado idadi kidogo ya ma-*VEO* kama 1,000 na zaidi kidogo ambao ndiyo tunaendelea kukamilisha taarifa zao na wenyewe watapelekwa Hazina kwa ajili ya kuingizwa katika urataibu wa kawaida wa malipo ya mishahara. Nao hawa ni kwa sababu kupitia Bunge hili hili tulifika mahali tukaamua kwamba hawa tusiwaondoe tuwaache waajiriwe na Serikal, lakini na wenyewe wapewe kipindi cha miaka mitatu. Kwa hiyo, tukakubaliana inaendelea lakini wao wamepewa muda wa kukamilisha hilo zoezi.

Mazingira ya kufanyia kazi katika Halmashauri tunalikubali, huu ni ushauri mzuri, lakini nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, juhudi za Serikali kwenye eneo hili zinaendelea. Ni kweli uwezo wa Serikali ni mdogo. Lakini tunajitahidi sana kuboresha mazingira ya kazi, hasa kwenye Kata na vijiji na mimi ninahakika baadhi yenu mnajua kwamba ziko programu wako wahisani na wakati mwingine hata kupitia fedha ya maendeleo tunayoitoa sasa ya *CGD,* tumejikita katika kujenga ofisi nzuri za kufanyia kazi katika Halmashauri zetu na programu hiyo itaendelea kwa kuwa ni jambo la msingi sana. Sasa najua bado hawana vitendea kazi, hawana hili, mambo mengi tu, lakini kadri uwezo wa Serikali utakavyoongezeka tutaendelea na sisi kuboresha maslahi yao kwa kadri itakavyowezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, liko jambo lingine zuri sana ambalo Waheshimiwa Wabunge wamelisema na mimi naomba nitoe maelezo, nalo ni la mipaka katika ya Madiwani na Watendaji kwamba wakati mwingine Madiwani wanaonekana wanaingilia Watendaji wakati mwingine Watendaji wenyewe wanaonekana kutokusikiliza yale wanayopewa na Madiwani wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utendaji wa utumishi, hili tusije tukashangaa. Katika baadhi ya maeneo litakuwepo, lakini ziko Halmashauri nyingi zinazofanya vizuri sana bila misuguano mikubwa. Lakini kwa hawa tunaendelea kuwasaidia na kubwa tunalolifanya kwanza ni elimu kwa makundi yote mawili. Kila mmoja ajue majukukumu yake na mipaka yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuko katika maandalizi ya kufanya semina moja kubwa kwa Madiwani wote maadam tumeshafanya kwa Wakurugenzi ili waweze kujua kwa kweli namna ya kuyaainisha majukumu yao kupunguza misuguano ambayo haina maana. Tutalitekeleza kwani ni maagizo ya Mheshimiwa Rais na tunaifanyia kazi kwa lengo hilo. Lakini litakapojitokeza katika hali mmoja mmoja tuko tayari kulizungumza ili tuweze kulimaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala la ushiriki wa Madiwani katika Bodi za Zabuni. Najua hili ni jambo la siku nyingi linasemwa sana. Lakini nataka nirudi nyuma kidogo, mwaka 2002/2003 ninavyokumbuka jambo hili lilikuwa linasemwa sana tena kwa nia nzuri na lilianzia Bungeni hapa hapa Waheshimiwa Wabunge ndiyo walianza kutoa rai hii kwamba kuwemo Madiwani katika Kamati hizo za Zabuni ina- *jeopardize* usimamizi wa kazi zao na utendaji wao kama Madiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunasema iko rushwa, sasa Mwenyekiti mwenyewe wa *Council* ndiyo unaambiwa wewe na Madiwani wako ndiyo mnakula rushwa wakati wa kutoa zabuni, haya nani sasa amfunge paka kengele?

Mheshimiwa Naibu Spika, limekwenda karibu miaka miwili hivi hatimaye tukasema pengine tunajifunza kutoka kwenye ngazi nyingine, ndipo tukaleta pendekezo kupitia kanuni zetu za manunuzi kwamba pengine tuwaondoe ili Madiwani sasa wafanye kazi ya kusimamia vizuri zaidi hao watendaji wao ilikuwa ndiyo dhamira ya Serikali. Lakini limeonekana lina mgogoro mkubwa na rai inayojitokeza kwa nguvu sana ni kana kwamba asipokuwemo Diwani katika kutoa zabuni *as if* zabuni ndiyo kazi peke yake pale ya maendeleo basi Halmashauri nzima inakufa.

Mimi naogopa nadhani si kweli sana, lakini liko shinikizo kubwa na mimi nasema namna nzuri ya kutazama jambo hili ni kutafuta namna ambayo tunaweza tukaifanya Kamati hii ikawa pengine na mjumuiko mkubwa zaidi kidogo kuliko watendaji peke yao au Madiwani peke yao. *(Makofi)*

Lakini tusidhani *solution* ni Madiwani kurejeshewa mamlaka ya kuwa hapo. Waheshimiwa Wabunge nyie wenyewe mnajua haya yalifanyika. Kesi tulizoanza kuzipata ni Madiwani wenyewe kuwa na kampuni na hizo kampuni ndiyo tukawa tunagawanya zile *tender*. Sasa mtu mmoja unaweza ukasema eeh, sasa wakigawana kuna ubaya gani, si sahihi? Mimi nadhani tujaribu kuangalia jambo hili kwa makini. Sisi tunakubali kabisa kwamba iko haja ya ku-*improve* Kamati hii lakini si kwa mtindo wa kusema Madiwani warejee wachukue jukumu hilo lote. Isipokuwa tuone mchanganyiko gani unafaa kutupa Kamati ambayo itakuwa inaonekana angalau kwa sura yake kwamba ina uadilifu wa namna fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili kubwa ni kuweka utaratibu ambao kwa vyovyote vile Kamati hiyo hata kama ingekuwa na sura gani ni vizuri baada ya maamuzi yao yakarudi kwenye Kamati ya Fedha na *Full Council* kueleza namna walivyofikia uamuzi wa kuteua. Kwa sababu hilo ni jambo la msingi sana. Ni kweli kwa hali ilivyo sasa Mkurugenzi akikaa pale anateua, anaanza kufanya kazi wakati mwingine hata Halmashauri haijui kinachoendelea ni nini?

Mimi nakubaliana na ninyi kabisa kwamba hili lazima lifanyiwe maboresho, lirekebishwe ili Madiwani kwa kweli waonekane wanajua kinachoendelea ni kitu gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba nimalizie kwa hili kwa kusema ziko baadhi ya Halmashauri wanafanya kazi vizuri sana na mara nyingi napenda kutumia mfano wa Meya wa Manispaa ya Dodoma. Meya wa Dodoma amesaidia kuonyesha kwamba hata kama haumo kwenye zabuni ile una uwezo wa kuhoji na wakati mwingine ukaleta matunda mazuri sana. Meya aliletewa Mkataba saini hapa mzee, akasema sisaini mpaka nijue mmempa nani na mmempa kwa vigezo gani. Ohoo, tutakuleta mzee mwezi ukapita akaenda kwa Mkuu wa Mkoa akasema hawa wana lao, kuja kuchambua chambua ikaonekana ndiyo yale mliyoyasikia, Mwanasheria wa Manispaa mwenyewe ndiyo kajipa zabuni mwenyewe, yeye mwenyewe ndiyo mtetezi. Kwa hiyo, inawezakana kabisa Mwenyekiti na Madiwani kutimiza wajibu wao vizuri hata kwa mfumo uliopo sasa, lakini tutauangalia kwa maana ya kuuboresha zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine kubwa sasa ni hili la madaraka ya Waziri kuteua Madiwani wasiozidi watatu. Sasa najua lina mambo mengi wako Waheshimiwa Wabunge hapa wamelikataa kata kata kabisa kwamba hili hata ingekuwaje hatulitaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wako vilevile waliosema hapana, kulikataa kata kata kata pengine si jambo jema labda tuli-*modify.* Tulifanyie m*odification* tuone itakuwaje. Sasa naomba nieleze pengine maudhui ya pendekezo hili kwenu ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wenzangu nyie nyote mnazijua Halmashauri zenu vizuri sana. Pendekezo tulilokuwa tumefikiria sisi tufanye kwa kujua kwamba sasa fedha nyingi sana zinakuja kwenu, lakini malalamiko hayaishi, yako malalamiko makubwa kutoka kwa Madiwani wenyewe kwamba wanaburuzwa sana na wataalam wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wake mkubwa ni kwamba kuna Mkurugenzi *graduate* pengine ana *degree* mbili, kuna Mwenyekiti wa *Council* kwa heshima yake pale kwenye Kata pengine ana elimu ya darasa la nne au elimu ya darasa la saba. Hiyo tuseme ukweli tu. Hawa tulionao tumewapa mamlaka ya kusimamia Halmashauri hizi kwa asilimia mia moja. Tulichodhani sisi kwamba pengine tuongeze kiwango cha sharti la elimu. Badala ya kusema tu kujua kusoma na kuandika tuwe na kiwango fulani. Vinginevyo hii mipango mikubwa itasimamiwa vipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *billions of money* zinakwenda kwenye Halmashauri sasa hivi. Wenye kuzijua na wenye kuzipanga, wenye kujua zinakwenda kwendaje ni wataalam wangu. *Issue* ni Madiwani wangapi wenye jicho kali na zuri la kujua kwamba hapa kweli hiki kitu ni sawa ama siyo sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikwenda kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, ataniwia radhi nikamwambia Mheshimiwa Waziri Mkuu katika mapendekezo haya nilikuwa napendekeza tuweke *form four* kama ndiyo kiwango cha chini kwamba angalau ukiwa na Madiwani wenye elimu ya *form four* hivi ukatumbukiza na wenye elimu kidogo pale pengine huu mzigo wa fedha hizi na *technicalities* ambazo wakubwa

hao wanaitwa wataalam wanazozitoa kwao tunaweza pengine tukakabiliana na tukalinda mali ya umma vizuri zaidi. Ndiyo ilikuwa hoja tuliyokuwa nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa inawezekana mtu akasema hata hiyo siyo hoja, ukiwa na Diwani wenye elimu yoyote sawa tu. Lakini mimi nasema *if you want to be truthful and realistic* hilo jambo hatuwezi kulikwepa kabisa. Bunge hili linachangamka linaonekana ni very *active, very good, very good precisely because* wasomi wapo hapa wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu akasema hutawapata hao wenye elimu ya kidato cha nne huko. Tena akawa ananitania Monduli pale utawapata wapi wengi hivyo, na baadaye nikasema kweli hata Nkansi kule nitawapata wapi? *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, baada ya mazungumzo hivi ndiyo tukasema sawa *Okay*, hebu tujaribu kutazama muundo uliokuwepo zamani, maana utaratibu wa kuteua Madiwani wasiozidi watatu siku za nyuma ulikuwepo. Tukashauriana kwamba tupendekeze kwenu kwamba basi tuweke kipengele kinachomruhusu Waziri huyo mwenye dhamana kwa msingi kwamba kama katika Halmashauri ile yupo kweli mtu msomi ambaye amefanya kazi pengine Serikalini kwenye maeneo ya uchumi, maendeleo ya jamii kwa yale maeneo ambayo yanahitaji *expertise* akipatikana hata mmoja iwe chachu hasa katika mijadala ya kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja wala haikuwa sijui kutafuta watu watakaotupigia kampeni mwaka 2010, sijui nini, hata kidogo kwa nia nzuri tulikuwa tunajaribu kusema pale itakapoonekana yupo na haja ya kufanya hivyo inaonekana ipo basi Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana apewe mamlaka hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tulipopata mwanya huo tukaongeza, mimi nikamwambia Mheshimiwa Waziri Mkuu ukienda kwenye Halmashauri hizi ukikuta mtu anaitwa mlemavu yumo humo kwa nchi hii ya Tanzania kwa ujumla wake nikasema pengine utakuta wako watano, sita nchi nzima. Nikasema *may be opportunity* hii inaweza ikatoa nafasi sasa hivi makundi haya ni *well organized,* unaweza ukapata mtu mmoja ambaye anaonekana katika eneo fulani anaweza kuwa wa manufaa akiwemo miongoni mwa Madiwani. Tutoe fursa kwa watu kama hao, sisi tumeridhia Mikataba mingi ya kuhusiana na walemavu lakini *recognition* yao jamani ni ngumu bado kwa mfumo wa demokrasia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi juzi nilipomwona yule mlemavu aliyekuja kugombea Ubunge wa *East Africa* hapa *a Lawyer, a very good one*, mimi nilikuwa mmoja kati ya watu niliokuwa naamini kwa Watanzania tulivyo *sympathetic* kwenye kozi hii ya walemavu *that man would probably have made it,* ahaa wapi *is not easy*.

Kwa hiyo, tukasema tuliweke na hili kwa nia hiyo ndiyo maana utakuta mle ndani tuna lugha ya *disadvantaged* na kundi hilo lingine. Lakini *is not automatic*

kwamba kila mahali wee tutakwenda hivyo, hapana, ni pale itakapooneka yupo mtu ambaye anaweza akawa ni changamoto katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana Waheshimiwa Wabunge wameona kiutaratibu tumekubaliana kwamba basi tupendekeze kwenu hao watu wasitokane na Waziri mwenyewe kuamka tu siku moja hivi, akaamua Mheshimiwa Peter Pinda na fulani, hapana, ulizeni vyama husika huko kwenye Halmashauri, Vyama vya Siasa. Waziri amepewa eneo hili, je, nyie huko kuna mtu ambaye mnafikiri akiwemo anaweza kusaidia? Hilo linatoka kwenye Vyama ilimradi viwe vinawakilisha katika Baraza la Madiwani. Tukasema baada ya hapo kanuni ziandikwe sasa vizuri zi-*elaborate* anapatikana patikanaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mwanzoni katika mabadiliko tulikuwa tumeliweka bayana, lakini likaonekana ni *details* nyingi. Lakini *let me say frankly* tulichokuwa tumesema Chama kikishapata majina kwa njia zake chenyewe waende wakashauriane na Kamati zao za Vyama vya Madiwani waliomo katika Mabaraza yao. Waridhiane wenyewe pale kwamba ukimpeleka Ndugu Peter Pinda, huyu tunadhani anaweza akatusaidia hasa kwenye Sekta ya Kilimo au jambo lolote ambapo huyo mtu anaonekana pengine amebobea.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, chagueni majina matatu mleteni Waziri mwenye dhamana. Waziri mwenye dhamana kutokana na *list* ambayo imetoka kwenye Vyama na kuridhia na Kamati zile za Madiwani za Vyama vyao atatoa jina mmoja kati ya yale matatu. Apeleke jina hilo kwa Mwenyekiti wa Halmashauri aliwasilishe kwenye Baraza, na Baraza lithibitishe jina hilo kama wanaona *yes* au hapana. Huo ndiyo utaratibu tuliokuwa tumeupendekeza *provided* anakuwa kweli ni mtu ambaye nyie huko mnaona *input* ya huyo mtu inaweza pengine ikatuletea changamoto nzuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa najua ziko hofu nyingi, watakuja kufanya fujo na ndiyo maana tumesema wapite huko maana si mnawajua vizuri zaidi. Waziri anachotafuta ni kuona kama ni mtaalam na mtaalam wa nini na pengine anaweza akatusaidia katika eneo hilo. Mkipata mtu *retired* katika masuala ya fedha, eneo ambalo ndilo linatuletea mgogoro, yuko pale kwenye Halmashauri yetu, lakini kila ukimwambia twende ukagombee Udiwani anafikiria ile anaona ahaa nijikalie Bwana, *after all I get my little pension*. Sasa hawa tungeweza pengine tukawa *drawn in* kwa njia hiyo na ndiyo maana tukapendekeza jambo hili kama lilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nimalizie kwa hili la Waheshimiwa Madiwani niwaondoe hofu. *(Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, samahani kidogo, naomba basi kwa hili nimalizie tu kwa kusema nia ya Serikali ilikuwa *as good as I have tried to put it* ilikuwa ni nzuri. Lakini bado Waheshimiwa Wabunge wanayo fursa ya kuona kama nia nzuri ya Serikali hii pengine haina maana ni *awkward.* Lakini mimi naamini dhamira yetu ilikuwa ni nzuri sana na nasisitiza siyo kwamba haya yatafanyika katika Halmashauri zote kwa

wakati mmoja hata kidogo itategemea *demands* za kila Halmashauri kwa kadri itakavyowezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, liko lingine moja ambalo pengine nalo nilisemea maana Mheshimiwa Kabwe Zitto, alilieleza na hatuwezi kulinyamazia. Amehoji kwamba katika Muswada aliouona ule wa mabadiliko ameona jina la Mheshimiwa Peter Pinda limewekwa pale. Kwa hiyo, akauliza kwa nia nzuri tu kwani mimi ndiyo Waziri mwenye dhamana. Waziri mwenye dhamana si Waziri Mkuu. Mimi ni nani sasa? Kwa hiyo, nilivyolipata lile nikakimbia kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu nikasema nimwambie vipi Mheshimiwa Kabwe Zitto, kwa hili? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa kifupi tu nasema mimi nafanya kazi kwa niaba ya Waziri Mkuu, Waziri Mkuu ndiye amepewa dhamana hii yote. Ndiyo maana naitwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, lakini katika eneo linaloitwa TAMISEMI. Kwa kufanya hivi, bado natimiza kazi yake ile ile aliyokuwa amenituma nimsaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini pengine baada ya maelezo hayo, Mheshimiwa Kabwe Zitto, basi atakuwa ameelewa na pengine hatakuwa na tatizo kubwa juu ya jambo hili.

Waheshimiwa Wabunge, sina jambo lingine, lakini inawezekana mambo yalikuwa mengi na mengine tumeyasahau sahau, basi nitaomba radhi na kama yatakuwepo wakati wa Kamati ya Bunge Zima basi nitayarudia rudia kuyaweka vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

### Muswada wa Sheria ya Kufanya Marekebisho katika Sheria Mbalimbali za Serikali za Mitaa kwa Mwaka 2006 *(The Local Government Laws( Miscellaneous Amendments) Bill, 2006)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kama mtakavyoona Muswada wetu ni kitabu chote sasa kanuni ya 72(3) inasema tukiwa katika Kamati ya Bunge Zima tunaweza kupitia kifungu kimoja baada ya kifungu kingine au tunaweza kwenda kwa Ibara moja baada ya Ibara nyingine yaani kinasema hivi: “Kamati ya Bunge Zima itajadili na kupitisha au kufanya mabadiliko na kupitisha Muswada Ibara moja baada ya Ibara nyingine. Isipokuwa kama Mwenyekiti akiona inafaa aweza kuihoji Kamati itoe uamuzi wake kwa kundi moja lenye Ibara kadhaa au Ibara zote zilizomo katika sehemu moja ya Muswada. Kwa hiyo, tutatumia njia hii ya pili. Tutakwenda taratibu kusudi penye mabadiliko aseme.

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2
Kifungu cha 3

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 4
Kifungu cha 5

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 6
Kifungu cha 7

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 8

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 9
Kifungu cha 10
Kifungu cha 11

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 12
Kifungu cha 13

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 14

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 15

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 16

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 17

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 18
Kifungu cha 19
Kifungu cha 20

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 21

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 22
Kifungu cha 23

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 24

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 25
Kifungu cha 26

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 27

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 28
Kifungu cha 29

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 30
Kifungu cha 31
Kifungu cha 32

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilishaunga mkono isipokuwa tu nataka nisaidiwe na Mheshimiwa Waziri kwenye kifungu cha 31 ukurasa wa 108 kile kifungu kipya 9(a) hapo nataka tukubaliane na Mheshimiwa Waziri kwamba vyombo hivi *Regional Consultative Assembly* ni vyombo muhimu sana. Sasa ni vizuri vikapewa nguvu za kuonekana hata yule mtu anayepewa hiyo kazi anajua nimegemea mahali gani. Nasema hivi kwa sababu kwa mfano, ukiangalia katika baadhi ya vifungu wanatajwa watu tu kwa ujumla. Kwa hiyo, katika kuteuliwa, watateuliwa kwa mujibu wa kifungu kilichotajwa kwa mfano, *all members of Regional Consultative Committee.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa mtu mmoja mmoja kwenye vifungu vingine hatafahamika na hatajiona ana nguvu. Kwa hiyo, nilikuwa napendekeza hapa kwamba Mheshimiwa Waziri akubali Ma-*Regional Commissioner* wakishapata orodha ya watu hao wawatangaze katika gazeti la Serikali. Utawapa nafasi sana na nguvu ya kuweza kufanya kazi vizuri.

La pili, nilitaka kukumbusha Mheshimiwa Waziri kwamba bajeti ni muhimu sana ili vyombo hivi vifanye kazi. Kwa hiyo, tungeomba hilo alichukue. Lakini katika kifungu (c) nilitaka tu nipate fafanuzi pale kifungu (c) cha wale watu aliposema *all key stakeholders* nadhani hii itatupa tatizo. Tungeondoa ile *all* tubakize *key stakeholders include* na pale pasahihishwe kidogo badala ya *include* iwe *including*. Nadhani itatusaidia sana hiyo. Langu lilikuwa hili tu la kupata ufafanuzi na kuelewana na Mheshimiwa Waziri kwa kuwa tunakwenda kufanya kazi. Mimi naviona ni Vyombo muhimu sana hivi vya kushirikisha nguvu katika Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa William Shellukindo kifungu hiki chote kimefutwa katika *schedule of Amendments*. *(Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti,ahsante. Kwanza, naomba nikusifu sana kwa kuisaidia Serikali kupitisha Muswada huu kwa haraka. Kwa sababu wengi wetu tulikuwa bado tunaangalia kifungu gani, lakini wewe tayari umeisharuka. Si uzee lakini *I think* ukiangalia *Amendments* nyingi kama hizi inaleta matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kifungu namba 30 hicho kinazungumzia juu *District Consultative Committee.* Hapa ningependa tu kupata maelezo maana yake ninajua kwa hali halisi kitapita tu. Ningependa tu kupata maelezo kwa kuwa baadhi ya mambo yatakayozungumzwa hapa yanahusu Vyama vya Siasa. Je, mbona haijawa bayana kama Vyama vya Siasa vitapata wawakilishi angalau Vyama vya Siasa ambavyo vina Madiwani katika *Council* ile ambayo inahusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilifikiri *such other persons may be invited by the Chairperson to the District Consultative Committee may b*e hapo. Lakini sasa unazungumzia juu ya Mwenyekiti, na Mwenyekiti mwenyewe anaweza kuwa Mwenyekiti wa Chama kimoja tu. Kwa hiyo, yeye ndiyo anatoa *invitation.* Kwa hiyo, akitaka kuwadhibiti hapa ni rahisi sana kutokuweza kuwaita wengine au watu wa Vyama vingine. Lakini kama kutakuwa na *Regulation* inayosema kwamba ni lazima Vyama vyote ambavyo vimo ndani ya hiyo Halmashauri viwe *represented* kwenye hii. Hili linaweza kidogo likapunguza makali. Ningependa kupata maelezo juu ya hilo.

Halafu jambo lingine Mheshimiwa Waziri amesema kwamba *Consultative Council* haitageuza maamuzi ya *Council*. Kama hiyo ndiyo dhamira yake nataka kujua kama Mheshimiwa Waziri atalitaja hilo kwenye kanuni ili baadaye lisije likatumika vibaya na watu wengine watakaotaka kudhibiti hizo *Council*. Naomba kupata maelezo juu ya hilo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nitoe maelezo ya ufafanuzi kwa maeneo mawili kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo ambalo amelizungumzia Mheshimiwa John Cheyo ni kwamba inabidi ulisome sasa na hiyo Sheria yenyewe ilikuwa inazungumza nini? Kwa sababu hii ni taarifa inayotoka kwenye Kamati ya Mashauriano ya Wilaya, *Okay District Consultative Committee* kwenda sasa Mkoani kwamba Mkoa kule ni vizuri ukajua wanapokutana hivi mambo gani wamekubaliana na wamesisitiza nini na kadhalika na kadhalika. Ndiyo maana nilikuwa nasema ni lazima sasa ujue hii inatokana na sheria ipi, anazungumza *Principal Act.*

Lakini bado rai yake ndiyo nilikuwa najaribu kuangaza hapa haraka haraka anachosema tu ni kwamba hata huko inakopelekwa hiyo ripoti, tuna uhakika gani kwamba viongozi wa Vyama vingine na wenyewe wamo ili hayo yatakayokwenda basi tuweze ku-*appreciate* wote kwa pamoja.

Kwa utaratibu ulivyo sasa, ukienda kwenye *RCC,* ambayo ndiyo *Board* ambayo iko pale Mkoani, Wadau wengi kadri inavyowezekana na pale inapowezekana na Vyama Vya Upinzani vile vile kutegemea na ajenda zenyewe zilivyo, wanaalikwa. Kwa hiyo, maadam hili litakuwa limetoka huku, kama ni ajenda ambayo inatugusa wote, za maendeleo hizi, mimi sidhani kama lina tatizo hata kidogo. Linaweza ama kwa mujibu wa sheria au hata kwa mujibu wa taratibu za kiutawala tu, likawekwa vizuri ili lisionekane pengine tuna jambo ambalo ni *hidden* agenda ya ajabu ajabu. Lakini kwa sasa wanajitahidi kuwa-*accommodate Stakeholders* wa kila aina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la pili la kumhakikishia kwamba haitakuwa hivyo. Nimeeleza katika maelezo na mimi naamini limekuwa *recorded* kwenye *Hansard*, *you can quote me*, kwa sababu wala siyo hiyo tu kwamba liwekwe kwenye kanuni, ukitazama hata zile *function* tulizo ziweka kwa ajili ya *DCC,* tumejaribu kuziweka *in such a way* kwamba zionekane ni za aina ambayo ambayo haitatengua maamuzi ambayo yameamuliwa halali na Mabaraza ya Halmashauri.

Lakini kama kuna haja ya kuliweka na kwenye kanuni, bado tunaweza vile vile tukaliweka kuzidi ku-*emphasize* kwa sababu ni jambo la msingi, maamuzi ya Baraza la Madiwani ni maamuzi halali, ni maamuzi kwa mujibu kwa sheria na yatatenguliwa kwa taratibu zake ambazo zimo kwa mujibu wa sheria.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika moja ya *functions* ambazo zimetajwa hapa za hii *District Consultative Committee is to ensure that the Local Government Authorities, execute and implement their development activities as mandated in the Development Plans* na inaendelea mpaka kwenye hiyo *to ensure adherence to the code of conduct of all Political Parties in maintenance of peace and tranquility within the District*.

Sasa, swali la kwanza, unaposema *to ensure*, wata-*ensure* vipi? *Is this another Board above, I mean* kitu ambacho kiko juu ya Halmashauri! *Because* kama wewe uko kiranja *and you say that I will ensure you perform this*, ndiyo kusema wewe unajiweka unadhani wewe ni Kilanja. Sasa ukiweka haya maneno maana yake ni kwamba hii *DCC* ni Kilanja wa *Council* hizi. *Unless* nipate maelezo unavyonimbia wata-*ensure,* wata-*ensure* maana yake nini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nieleze tu kwamba Mkuu wa Wilaya pale Wilayani ni wajibu wake kuhakikisha, narudia hili neno kuhakikisha kwamba mambo ambayo yameamuliwa katika *Council* hiyo, yanatekelezwa na mimi nauliza Mheshimiwa Cheyo, *what is wrong with that?* Kwa sababu huyu anawasaidia tu kuhakikisha kwamba msifanye, mkaamua mambo, *and then on the ground, mna-relax* tu kwa sababu mnadhani hamna *prefect*. *Prefect,* Mwakilishi wa Rais yupo. Kwa hiyo, atauliza kwa nini yale mliyokubaliana pale ninyi hamjayatekeleza? Kwa hiyo mimi ninachosema hapa, ni kusaidia tu *Council* hii itemize wajibu wake vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa liko hili la pili ambalo nalo naona ameliunganisha; *Ensure effective implementation Council decisions, ensure adherence to code of conduct*. Kwa kweli ni maneno yale yale tu kwamba mnapokutana pal, vitu mlivyokwisha kukubaliana ninyi wenyewe, sisi kazi yetu ni kufika na kuona jamani maadam mlishakubaliana hili, *why aren't you now executing them* kama ilivyokubaliwa?

Sasa mimi sioni kama lina utata mkubwa sana kwa maana ya kuzisaidia *Local Authorities* zifanye kazi yake vizuri.

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

*(Bunge lilirudia)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lilikaa kama Kamati ya Bunge Zima na kupitia Muswada wa Sheria ya kufanya marekebisho katika sheria mbali mbali za Serikali za Mitaa kwa mwaka 2006 *(The Local Government Laws Miscellaneous Amendments Bill, 2006)* kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na mabadiliko yaliyofanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Kufanya Marekebisho katika Sheria mbalimbali za Serikali za Mitaa kwa mwaka 2006 *(The Local Government Laws Miscellaneous Amendments Bill, 2006)* sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa John M. Cheyo alisema Naibu ameamua kupitia mafungu yote kwa sababu ya kuisaidia Serikali. Nafikiri siyo sahihi. Unafahamu mkiangalia mabadiliko ambayo mmeyafanya Waheshimiwa Wabunge wenyewe katika Muswada huu ni mengi sana.

Kama tungesema twende Ibara kwa Ibara, zingine namba zimeshabadilika. Kwa hiyo, fungu kwa fungu haikubadilika. Hiyo ndiyo sababu. Kwa hiyo, siyo sahihi kusema vile. Kwa hiyo, naomba hiyo ieleweke hivyo na kazi kubwa ni kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wenyewe mmefanya kazi kubwa sana kubadilisha Muswada kwa vile ambavyo mmetaka na hiyo ndiyo kazi ya watungaji sheria na ninapenda muendelee kufanya hivyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyoeleza, kesho asubuhi baada ya kipindi cha Maswali, Waziri Mkuu atatoa hotuba ya kuahirisha Bunge mpaka Kikao kingine. Lakini huu ni mwezi wa kumi na moja na tunaelekea kumaliza mwaka 2006. Kwa mujibu wa taratibu zetu za kisheria na kikatiba, napenda kuwajulisha kuwa fomu za Tamko la Viongozi wa Umma kuhusu Rasilimali na Madeni kwa mujibu wa sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya Mwaka 1995.

Napenda kuwajulisha kuwa mnatakiwa kuchukua fomu za Tamko la Viongozi wa Umma kuhusu Rasilimali na Madeni ofisini kwa Katibu wa Bunge kabla ya kurudi Majimboni kwenu ili muweze kuzijaza na kuzirudisha ofisini kwa Mheshimiwa Spika kabla ya tarehe 31 Desemba, 2006.

Waheshimiwa Wabunge, hili ni takwa la kisheria. Ikipita tarehe hiyo hujarudisha fomu, unajifuta mwenyewe Ubunge wako. Naomba nirudie tena, usipojaza itakapofika tarehe 31 Desemba, 2006, Kikatiba unafutika Ubunge wako kwa kutoku-*declare* mali zako. Kwa hiyo msilichukulie kama ni suala la kutania tu kwamba nikisahau labda nitahurumiwa, hapana! Kwa hiyo nawaombeni sana mzichukue ziko kwa Katibu wa Bunge atakuwa hapa hata Dar es salaam. Bahati nzuri wamerahisisha, unarudisha kwa Katibu wa Bunge mwenyewe fomu mbili nafikiri. Moja inabakia kwake, nyingine inakwenda Tume ya Maadili. Kwa hiyo, mkumbuke hilo, kwa sababu ni muhimu kwa upande wetu.

Waheshimiwa Wabunge, ninaahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.09 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatano,*
*Tarehe 15 Novemba, 2006 saa tatu asubuhi)*